KIU YA UZALENDO

Shaaban .Y. Shaaban

PUBLISHED BY:
SHAYU PUBLICATIONS,
MWANZA, TANZANIA.
MOBILE: +255 757 – 364 - 442
gizzoshayu@gmail.com

© Shaaban Y. Shaaban

ISBN: 978– 9976–5–1604 – 3

TYPESETTER:
Shaaban . Y. Shaaban

Chapa ya kwanza 2017

@ Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kudurufu, kutafsiri au kusambaza na kuuza bila ruhusa ya mwandishi.

Sehemu Ya Kwanza

UTANGULIZI

DIBAJI

Madhumuni ya kuandika hiki kitabu ni kuweza kuchangia maarifa ambayo ninayo kwa jamii. Nadhani ni muhimu na ni jambo lenye thamani na busara kutoa kile nilicho nacho kuwapatia wengine ili kiweze kuwasaidia.

Kwa miaka kadhaa nimekuwa nikitafakari na kuandika kwenye mitandao kadhaa ya jamii na kutoa mawazo yangu na maoni kufundisha kuhusu mambo kadha wa kadha.

Nimeamua kutoa kitabu hiki ambacho ni mkusanyiko wa fikra na maandiko mbali mbali ambayo nimewahi kuandika na fikra nyingine ambazo nitaongezea ili kufanya kitabu hiki kiwe kamilifu.

Kwa kadiri ya uwezo wangu nimejitahidi kuelezea fikra hizi katika lugha nyepesi mno, ili yeyote atakayesoma kitabu hiki aweze kupata kile ambacho nitajadili. Kitabu hiki ni mkusanyiko wa mawazo ya kifalsafa, kijamii na kisiasa. Ni kitabu ambacho mtu yeyote ambaye anapenda vitabu vya kufikirisha na kujenga anapaswa kuwa nacho.

Ni Matumaini yangu kila ambaye atapata kukisoma kitabu hiki hatatoka bila kupata chochote ambacho kitambadili mtizamo wake na fikra zake kuhusu masuala kadhaa nitakayokuwa nimejadili.

Nakiweka kitabu hiki mbele yenu si kwamba nilichoandika ndio ukweli wa mwisho ambao haupaswi kujadiliwa; bali niliyoandika yawe mwanzo wa mjadala mpana wa kutafuta suluhisho la mambo kadha wa kadha ambayo jamii yetu inakabiliana nayo kwa sasa.

Lengo ni kujadili matatizo na changamoto ambazo kizazi chetu kinazo na kutafuta mbinu mahsusi za kukabiliana nayo. Kwasababu hatupaswi kurithisha matatizo yetu kwa kizazi kijacho, bali tunapaswa kutafuta suluhisho la matatizo tunayokabiliana nayo sasa, wakati huu; na kulikabithi taifa kwa kizazi kingine kukabiliana na changamoto za wakati wao.

Kama tunataka kutatua matatizo yetu tunayokabiliana nayo sasa, tunapaswa kufikiri na kutenda sasa na tunapaswa pia kutengeneza dira ya taifa letu leo. Hili ni muhimu sana wote kufahamu; mwelekeo na dira ya taifa letu inategemea sana ni aina gani ya mawazo tunayo. Mawazo yetu ndiyo yanayojenga aina ya taifa. Kwa hiyo inategemea fikra gani tunazo kwa taifa letu. Na inategemea pia kama mawazo ya watu wetu yanaongozwa vyema na katika mkondo unaofaa ama la.

Hivyo, ni wito wangu kwa watu wa taifa hili kuangalia upya jinsi tunavyofikiri na kutenda, Haya mambo mawili ni ya kimsingi sana. Jinsi tunavyofikiri na kutenda kwa taifa letu.

 ukubwa au udogo wa taifa letu unategemea sana hayo mambo mawili.

Jinsi tunavyofikiri kwa taifa letu, lakini pia jinsi tunavyotenda, ili kuleta kile tunachofikiri kwenye matendo ili kiwe kitu dhahiri. Kwahiyo mawazo yetu ni muhimu katika ujenzi wa taifa hili. Inategemea mawazo yetu ni bora kiasi gani na utayari wetu wa kujitoa kutumikia taifa letu ili liwe kubwa.

Sisi ni wajenzi au wabomoaji wa taifa letu kwa mikono yetu wenyewe kwavile tunavyofikiri au kutenda kwa taifa letu. Maendeleo yetu yanategemea sana mawazo yetu na fikra zetu na jinsi tunavyoongoza fikra hizo katika matendo.

Tutalijenga kama tukiwa makini katika fikra zetu na kujenga mifumo imara ambayo itafanya taifa hili kuwa endelevu na kinyume chake ni sahihi; tutalibomoa kama hatutakuwa makini. Naleta kwenu kitabu hiki cha kifalsafa na kiitikadi, Ili mawazo yaliyomo humu yaweze kutafakariwa, na yatoe mwongozo na dira kwetu ya aina ya taifa tunalotaka kulijenga na matumaini tunayotaka kuyafufua kwa watanzania.

Shaaban Y. Shaaban
Mwanza, Tanzania 2017

TABARUKU

Kitabu hiki nimekitoa mahsusi kwaajili watanzania wote wakisome na kukielewa na kila mmoja wetu kuyafanyia kazi yale ambayo nimeandika kwa manufaa yetu na taifa letu kwa ujumla.

Ni Jukumu letu la dhati kulifanya taifa letu kubwa na sehemu nzuri ya kuishi. Hakuna mwingine atakayeweza kulifanya hili, bali sisi wenyewe watanzania. Sisi ndio tutakalolifanya taifa hili kuwa zuri au baya kwa nguvu zetu wenyewe. Hakuna taifa jingine litakalokuja kujenga taifa letu na kutuletea maendeleo yetu wenyewe.

Kama tukitendeana haki wenyewe kwa wenyewe tutalifanya taifa hili kuwa moja na endelevu. Kama tutakuwa na maono ya pamoja na kufanya jitihada

kuyafikia maono hayo hakika tutafika tunapotaka kufika. Ni jitihada zetu na mawazo yetu yatakayotufikisha huko kama watu wamoja wenye lengo moja. Hakuna utukufu pasipo umoja. Tutafikia ushindi wetu kama taifa tutakapokuwa wamoja. Nguvu ya taifa lolote ni umoja wa watu wake.

Aidha nakitoa kitabu hiki kwaajili wa umoja wa taifa letu. Hatuwezi kuendelea kama taifa ikiwa sio wamoja. Nguvu yetu kama taifa imelala kwenye umoja wetu na hata ulinzi wetu. Kama sio wamoja mambo yote haya hatutayafikia.

Shukrani

Hakuna kinachodumu katika maisha haya. Matatizo yetu ambayo yanaonekana kutushika na wakati mwingine kutukatisha tamaa hayadumu. Hakuna kidumucho katika dunia. Matatizo yetu ni ya kipindi. Ni kama bahari kuna wakati inatulia na kuna wakati hujawa na tufani. Mvuvi bora ni Yule anayevumilia tufani hadi bahari inapotulia kisha kuendelea na safari yake. Kwenye kila matatizo

kuna nyakati za furaha na faraja ambazo tuna tumainia mbeleni.

Zaidi ya hayo tunafurahia shida zetu; kwasababu kuhangaika kwetu huzalisha uvumilivu, na uvumilivu wetu hutufanya kuwa imara na uimara wetu huzalisha matumaini (Warumi 5:3-4)

Ukweli ni kwamba hatuwezi kuepuka nyakati za shida zitakapokuja jambo la msingi tunapaswa kutambua kila kitu kina wakati wake na majira yake.

Kwa Mama yangu na familia ya Dr Yusuf Moto Shaaban. Kaka zangu na Dada zangu wote. pamoja na wote walioshiriki hadi hiki kitabu kutoka.

SEHEMU YA KWANZA

Dhana na malengo ya kuandika sehemu hii ya kwanza ni kuelezea umuhimu wa maadili na nidhamu katika ujenzi wa taifa lolote. Lakini pia nimeelezea ni jinsi gani nidhamu hii na maadili yanavyoweza kujengwa kwa watu wetu kupitia

makuzi, elimu tunayotoa shuleni na dini ili kujenga raia wenye uwezo wa kutenda matendo ya haki na adili.

Ni wajibu wetu kujenga raia wenye adili na wenye tabia ambazo zitatuwezesha tuendelee kama taifa. Raia wenye uwezo wa kufanya maamuzi sahihi yenye faida kwa taifa lao, raia wawawajibikaji kwa taifa na wenye mwamko na utaifa.

Kwahiyo dhana nzima katika sehemu hii ya kitabu ni mabadiliko ya fikra ambayo yatapelekea watu wetu kutenda tofauti na kuwa na mtazamo chanya na mwamko kwa taifa lao.

Dhana nzima ni mabadiliko ya kitabia ya watu wetu ili tuweze kujenga taifa letu. Kwasababu kuna tabia ambazo zinaturudisha nyuma kama taifa na ni jukumu letu kuzijadili na kujaribu kuzibadilisha. Tutakapobadilisha watu jinsi wanavyofikiri kuhusu taifa lao na kuwafanya kuweza kulitumikia kwa kulifanya kuwa kipaumbele chao ndipo tutakapoweza kufanikiwa kama taifa.

YALIYOMO

Elimu na maadili……

Siasa……

Taifa……

Serikali ……

Elimu ……

Siasa ……

Utamaduni ……

Mti wa matumaini ……

Busara ……

SURA YA 1

ELIMU NA MAADILI

Msingi wa taifa lolote lile ni elimu ya watu wake, kama tunataka taifa letu liwe endelevu hatuna budi kusisitiza elimu ya watu wetu. Kukuza ufahamu wa watu wetu ni jambo la msingi sana. Hatuna budi kupambana na ujinga kwa kadiri ya uwezo wetu na nguvu zetu zote.

Ni muhimu kuwafanya watu wetu kuwa waelewa na wenye ufahamu wa kutosha kuhusu masuala mbali mbali. Hili ni jambo la msingi kwasababu Salama yetu iko kwenye kupambana na ujinga. Na kuendelea kuwepo kwa taifa letu kunategemea hilo; kupambana na ujinga, kupambana na matendo ya kijinga na kulifanya taifa letu kuwa lenye busara.

Kwa busara nikimaanisha kulifanya taifa letu kufanya maamuzi sahihi na kuwa na watu wanaojitambua, watakaolifanya taifa letu kwenda mbele badala ya kurudi nyuma. Hii ndio wajibu na kazi ya elimu. Kumkuza binadamu ufahamu wake na kumwezesha kutenda na kujiongoza mwenyewe katika usahihi, kumwezesha binadamu kuondokana na tabia ambazo ni haribifu na kumtengeneza binadamu kuwa kiumbe bora na anayetenda kwa ufanisi.

Sio kuwa na maarifa ya kazi tu kama udaktari, ukandarasi, uanasheria na hata uhasibu, bali kumtengeneza binadamu kuwa kiumbe bora mwenye dira na ambaye tabia yake imejengwa ipasavyo ili kuwa raia anayewajibika na mzalishaji. Kwahiyo elimu lazima ijenge pia tabia za watu wetu kuwa bora. Kuwa fundi mzuri wa kutengeneza fenicha au mkandarasi mzuri au daktari mzuri na hata mwanasheria mzuri, hiyo ni sehemu ya elimu ambayo taifa linapaswa kuwa nayo. Ni elimu muhimu kwa maendeleo ya taifa. Hakuna mtu ambaye anaweza kukataa ukweli kwamba; ili tuweze kuwa na maendeleo ya vitu, tunapaswa kuwa na watu wenye fani mbali mbali kama hizo.

Ili tuendelee kwa vitu; ni lazima tuwe na watu kama hao, ambao wanasaidia katika uzalishaji mali na katika utoaji huduma. Na taifa kama taifa haliwezi kujengeka pasipo hao. Ni watu muhimu sana. Ili taifa likue na liendelee ni lazima liwe na watu wenye fani mbali mbali na wenye weledi wa kutosha katika fani zao. Hili halipingiki.

Maendeleo yote ya binadamu yametokana na elimu ambayo amejikusanyia na maarifa ambayo yaliwafanya wagundue na kupiga hatua moja kwenda nyingine. Pasipo gunduzi hakuna maendeleo. Watu wanaendelea pale upeo wao wa kiakili na kimaarifa unapokua na kuwawezesha kugundua. Gunduzi hizo ndizo zilizowafanya binadamu kupiga hatua moja kwenda nyingine.

Lakini tutakuwa tunajidanganya kabisa kama tukiwapa watu elimu hiyo ya darasani alafu tukasahau maadili yao kisha tukadhani tutaendelea. Kisha tukadhani tutatengeneza raia wazalishaji ambao watalipeleka taifa hili mbele kwa kasi. Tukifikiria hivyo tutakuwa tunajidanganya kama taifa.

Tabia za watu zina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa lolote lile. Ili tuendelee lazima tujenge nidhamu na tabia za watu wetu. Taifa lenye watu wasiokuwa na nidhamu haliwezi kuendelea. Huu ni ukweli ambao tunapaswa kufahamu. Ili tuendelee lazima tujenge tabia za watu wetu kwenye mkondo fulani wa mawazo na matendo na jambo hili linahitaji nidhamu.

Kitu cha kwanza kama tunataka kuendelea lazima tujenge nidhamu na raia wanaotii sheria. Kwanini taifa letu linashindwa katika mambo mengi ni kwasababu hatujawajenga watu wetu kuwa na nidhamu. Nidhamu huleta dira. Hakuna malengo yeyote ambayo tutajipangia kama taifa tukafanikiwa, kama taifa hili watu wake hawana nidhamu na kama hawatokuwa na malengo ya pamoja .

Hizi nguvu za kiakili na kimaadili ndizo zilizofanya mataifa yakue na kuendelea. Tunaangalia kuendelea kwa jamii yeyote ile kwa vitu wanavyotengeneza, na vitu hivi ndivyo vilivyowafanya wao wapige hatua na kufanya mapinduzi kutawala mataifa mengine. Bila uwezo wa kugundua ambao uko ndani ya uwezo wa kila binadamu hakuna taifa ambalo litaweza kuendelea na pengine kutawala mataifa mengine.

Maendeleo ya kiakili ya watu hupimwa na vitu walivyogundua na uduni wa jamii nyingine hupimwa pia na maendeleo ya kiakili ya jamii husika kwa kuangalia nyenzo zao wanazozitumia katika maisha yao ya kila siku. Gunduzi hizi ndizo zinazopima maendeleo ya kiakili ya jamii husika.

Kwetu sisi bado tunatumia vitu vingi ambavyo chimbuko lake sio kwetu bali kutokana na maendeleo ya jamii nyingine za ulaya. Wao waliendelea

wakagundua mambo mengi ambayo faida zake na sisi tunazipata kama magari, ndege, simu na mambo mengine mengi yanayofanya maisha haya ya kisasa na kurahisisha maisha yetu. Kwa gunduzi zao ni dhahiri waliendelea kiakili mapema zaidi yetu. Kitu kinachotofautisha jamii zilizoendelea na ambazo hazijaendelea ni gunduzi walizofanya na maarifa ambayo wanayo.

Maendeleo yote ya binadamu yametokana na gunduzi alizofanya kwahiyo tunapozungumzia maendeleo ya binadamu hatuwezi kuepuka kuongelea gunduzi alizofanya na ukuaji wa kiakili wa jamii husika.

Huu ugunduzi na uzalishaji mali ndio ulikuwa chimbuko la maendeleo na biashara katika jamii nyingi.

Jamii zilizozalisha zaidi zilifanya biashara na kupata faida. Waliuza bidhaa walizogundua na kujiongezea mitaji na mahitaji pia ya malighafi yaliongezeka kila soko lilivyopanuka, yaliyowafanya watoke kutoka katika nchi zao kwenda nchi nyingine kuyatafuta, pamoja pia na kutafuta masoko ya bidhaa zao. Kwahiyo pasipo gunduzi maendeleo ya binadamu yangeendelea kuwa duni. Ni dhahiri kabisa kutokana na hoja hii binadamu alianza kupiga hatua katika maendeleo yake pale tu , walipoanza kugundua nyenzo. Na maendeleo yake ya kiuchumi yalitokana pia na hilo.

Harakati za binadamu kutaka kutawala mazingira yake ndizo zilizomnyanyua na kumfanya kutoka katika hali ile ambayo yenye kufanana na wanyama na kumfanya kuwa kiumbe bora na aliyejuu ya viumbe wengine. Mihangaiko hii ya kutaka kumnyanyua binadamu kuwa zaidi ya binadamu, kuwa na nguvu na mamlaka inayotaka kufanana na Muumba, ndio

iliyowafanya watu wa magharibi wanyanyuke na kutawala mazingira yao. Binadamu hawezi kuwa na nguvu ile ile kama ya muumba wake, lakini anaweza kunyanyua nguvu zake za kiakili na kiroho na kutawala mazingira yake.

Hakuna kilicho na nguvu kubwa katika maisha ya binadamu zaidi ya fikra zake. Kwenye fikra kuna nguvu zenye kujenga au kubomoa. Maendeleo ya binadamu ya mali yanaenda sambamba na maendeleo na ukuaji wa kifikra wa jamii husika kuwa na uwezo wa kugundua na kutumia vitu walivyogundua. Hii ni nguvu ya fikra. Nguvu ya fikra ya kuweka taswira katika fikra na kuumba.

Kwahiyo kupambana na ujinga ni kuwa na maarifa ambayo yatasababisha jamii husika kuendelea. Na maarifa ya binadamu yote yamepatikana kwa kutafakari. Ni nguvu ya akili kukusanya maarifa kwa kufikiri na kufanya tafiti. Kwahiyo jamii ambazo zilizohangaika na kutumia akili zao kutafuta maarifa ili kukabiliana na changamoto ambazo zinawakabili ndizo zilizoendelea. Na maarifa haya hawakupata kirahisi rahisi, walihangaika bila kuchoka wala kukata tamaa mpaka njia ikafunguka na kupita kwenye mlango wa ufahamu wa maarifa.

Mlango huu unapofunguka kuna hazina kubwa ya maarifa. Pale vikwazo vya kiakili na kiimani vinapofunguliwa, binadamu huacha kujiwekea mipaka ya kile ambacho ana uwezo wa kukifanya au kukiendeleza, na kuweza kuamini nguvu aliyonayo katika kufanya mapinduzi kwenye dunia.

Mamlaka ya binadamu ni makubwa na uwezo alionao ni mkubwa lakini umefungwa na mawazo yake mwenyewe, imani yake, na matendo yake yasiyo na dira. Kila wakati anakuwa na mashaka na nguvu na

uwezo wake, mashaka na maisha yake, kama vile alijileta mwenyewe duniani, lakini anashindwa kutambua ni Mungu ndiye aliyemuumba na dunia aliyomo ni kazi ya mikono yake, Kila tukionacho ni kazi ya Mungu.

Hakupaswa kuwa na hofu na maisha yake. Bali kumuamini Mungu ambaye alimuumba. Ni Lazima ajue Mungu aliyemuumba mbuzi ndiye aliyemuumba na yeye. Mbuzi hafanyi kazi yeyote. Huamka asubuhi na kukuta majani kibao yamejaa. Kwanini binadamu asiweke matumaini yake kwa Mungu ambaye ni mkuu kuliko vyote?

Kwahiyo tumetindikiwa na imani, tumejawa na hofu ya maisha. Hii kitu inapaswa kubadilika. Sisemi kwamba binadamu wasifanye kazi; Kazi ni kitu chenye furaha kama unapenda kazi unayofanya.

Na uvivu sio kitu chema hata kwenye macho ya Mungu. Nataka watu waamini na waweke matumaini yao kwa Mungu na sio kitu kingine chochote. Nataka watu waamini Mungu ni muweza. Nataka watu waamini maisha yetu kama taifa Mungu atayabadili kama tukimuamini na kuwa tayari kumtumikia. Na tutamtumikia kama tukitenda matendo mema. Kama tukitendeana mema wenyewe kwa wenyewe na kuwa tayari kushirikiana na kutendeana haki na kama tukijenga jamii yenye usawa.

Binadamu anapaswa kujua kwamba ameumbwa kwa mfano wa Mungu na ndani yake amewekewa uwezo wa kutawala dunia kama hatowekea vikwazo mawazo yake mwenyewe na kuwa na mashaka na nguvu zake, Yumkini tunapaswa kutii nguvu iliyo ndani yetu na kuiruhusu ituongoze. Nguvu iliyo ndani yetu ni kubwa mno. Tunaizuia nguvu hiyo kwa matendo yetu maovu na kukosa kwetu imani. Akili ambayo imekosa

umakini na jitihada, na ambayo iko njia panda kila wakati haiwezi kufanikiwa.

Imani ni kama mafuta kwetu pasipo imani hata vile vitu vidogo hatutaweza kufanikiwa kama taifa. Ili tufanikiwe ni lazima tuamini kwamba tunaweza kukua na kutanuka kuwa kama mataifa mengine makubwa.

Pamoja na ukuaji wa kiakili bila ya watu kuwa na imani na utayari wa kutaka kubadilika, hawatobadilika na kuendelea. Kubadilika ni kubadilisha matendo, mawazo na tabia zetu, ambazo zitatufanya tupige hatua mbele zaidi.

Ni lazima tuangalie matendo yetu kwa ukaribu zaidi. Hakuna kitakachobadilika pasipo kubadili matendo na mawazo yetu. Ni Lazima tuwe na imani na imani yetu ituongoze kule tunapotaka kufika.

Tusipoamini kwamba tunaweza kubadilisha maisha yetu, na tunaweza kuendelea na kukua kama mataifa mengine, hatutaweza kufika. Ni lazima tuwe na imani na imani hii ndio ituongoze na kufufua matumaini yetu kama taifa. Imani hii ituongoze kujenga baadae bora ya kila mmoja wetu.

Kwasababu hatuwezi kujenga taifa ambalo watu wake wamekata tamaa au hawana matumaini na kesho yao. Ni muhimu kujenga taifa ambalo watu wake wanafanya kazi kwa pamoja kufikia malengo fulani ya kitaifa na malengo hayo ndio yanayowapa matumaini ya kesho bora kama taifa na kama mtu mmoja mmoja.

Kwahiyo ni muhimu kujenga imani ya watu kwa taifa lao. Ni Lazima tuwajengee watu matumaini kuliko kukata tamaa. Watu ni lazima walipende taifa lao na kuwa tayari kulitumikia kwa uaminifu.

Hii ndio tofauti tuliyonayo kati ya mataifa ya ulaya na huku kwetu Afrika. Waliwekeza sana katika kutafuta maarifa. Maarifa hayo yaliwafanya waendelee na kuwa na uwezo wa kujilinda kwanza kwa kuzalisha na kugundua silaha bora na imara, na kuwa na uwezo pia wa kuvamia jamii nyingine na kuzifanya kuwa makoloni yao.

Makoloni haya yaliwafanya wajipatie utajiri mwingi kwa kuchukua malighafi kama vile dhahabu, almasi na chuma lakini pia kilikuwa chanzo chao kingine kikubwa cha kodi ambayo waliwatoza wananchi wa makoloni husika. Waliwapata wafanyakazi wenye gharama nafuu, lakini pia watumwa. Waliyaweza haya yote kwa kujenga kwanza umoja wa ndani ya nchi zao na kuwa ni watu wenye dhamira moja.

Baada ya kujenga umoja huo walikuwa na uwezo wa kutoka nje wakiwa wamejiimarisha sana na wakiwa na nguvu ya kutosha. Bila umoja wasingeweza kutawala mataifa mengine na kufanya makoloni yao. Walikusanya nguvu zao kwa kujenga umoja wao, kwakuwa na malengo ya pamoja. Kwa kuonana wao kwa wao ni watu wamoja ambao wana mwisho mmoja.

Watu wanapogawanyika taifa hukosa nguvu. Kwahiyo wao kwa kujenga umoja walifanya jitihada kwaajili ya ulinzi na maendeleo ya mataifa yao na kwa pamoja wakanyanyuka kutoka katika ujinga na umaskini.

Bila jitihada za pamoja changamoto nyingi ambazo tunakabiliana nazo hatutaweza kuziondoa. Zinahitajika nguvu za pamoja ili kuling’oa taifa kutoka hapa lilipo. Katika mazingira ya ubinafsi hatutaweza kufanikiwa. Lakini kama tukiweka maslahi ya taifa zaidi ya maslahi yetu binafsi tuna nafasi ya kufanikiwa zaidi. Walikuwa wamoja na walitafuta

maarifa kadiri ya uwezo wao ili kutawala mazingira yao. Watu bila kuwa wamoja na wenye dira moja kama nchi hawawezi kuendelea.

Kwahiyo pasipo taifa kuwa na uwezo mkubwa wa kujilinda maendeleo mengine ni vigumu kuyafikia. Taifa ni lazima liwe na uwezo kulinda uhuru wake dhidi ya mataifa mengine.

Ni lazima liwe na uhuru wa kujiamulia mambo yake yenyewe na kuwa na fikra huru. Mambo yote haya taifa halitoweza kuyafikia kama halitokuwa na uwezo wa kutengeneza silaha zake lenyewe kwaajili ya ulinzi. Kwahiyo kuna umuhimu wa kuwekeza katika utengenezaji wa silaha sio kununua tu. Kununua hakutaweza kutufanya tuwe salama zaidi.

Kwasababu mataifa ambayo yanatuuzia silaha yatakuwa yanajua tuna silaha za aina gani na zina uwezo gani. Hatutakuwa huru dhidi ya mataifa onevu. Lakini pia tutakuwa tunapeleka utajiri wetu kwa mataifa mengine ambao ulitakiwa uwekezwe humu humu ndani kwa maendeleo yetu. Lakini pia jitihada zetu za kujitegemea itakuwa ngumu kuzifikia.

Kujitegemea ni uwezo wa kutumia tunachozalisha. Hatuwezi kusema tunajitegemea kama hatutumii tunachozalisha. Tutaendelea kuwa taifa dogo kama tukiwa na uwezo mdogo wa kuzalisha.

Hatuwezi kuwa taifa la wachuuzi na kisha tukafikiri ya kwamba tutaendelea. Watu lazima wazalishe ili tuendelee. Ni lazima tuwe na viwanda ili tuzalishe bidhaa ndani ya nchi yetu. Watu wetu kwa kwenda china na ulaya kununua bidhaa na kuleta ndani ya nchi yetu ni kukuza uchumi wa nchi hizo na kupanua soko la bidhaa zao.

Soko linapoongezeka wanaongeza viwanda zaidi na ajira kwa watu wao na kujiongezea utajiri, tunahamisha utajiri wetu kwa mataifa mengine kwasababu ya kutokuzalisha zaidi. Ni muhimu kutumia tunachozalisha. Hatutaweza kujitegemea kama hatutafikia uwezo wa uzalishaji wa ndani utakaotuwezesha kutumia tunachozalisha. Tusipotumia tunachozalisha ni ngumu kwetu kukua.

Baadae wanatoa misaada ambayo inatufumba macho na kutudumaza zaidi katika jitihada zetu za kutaka kujitegemea. Misaada hawatoi bure bure kuna faida wanayopata nayo ni faida itokanayo masoko na hata maliasili. Wanarudisha kidogo kutokana na masoko wanayopata kutoka kwetu na wasingependa kuona tunajitegeemea na tukizalisha kila kitu kutoka ndani kwetu. Kama mikono yetu na akili zetu zikizalisha zaidi tutaendelea. Kwenye soko letu la ndani bado kuna mahitaji mengi mno. Ambayo kwa kutokuzalisha kwetu au kwa kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika uzalishaji yanakuja kuzibwa na bidhaa kutoka nje ya nchi yetu.

Watu lazima wajue wazungu ni wamoja wawe wajerumani, waingereza, wadenmark na kuendelea; na malengo na dhamira yao ni moja (world domination). Na mapambano yao mengi waliyowahi kupambana yalikuwa juu ya maslahi yao wenyewe. Kwahiyo tusidanganywe kuwa tunapendwa sana zaidi ya maslahi yao. Historia ya dunia ni historia ya mapambano ya kimaslahi na ya kutawala dunia. Na sidhani kama wanapenda tukue na kujitegemea. Kufanya hivyo ni kutaka sisi kupata nguvu na kujitawala na kuwa na mamlaka yetu wenyewe jambo ambalo huenda likawa tishio kwa siko zao za usoni. Ukitilia maanani mihangaiko yote katika dunia kuanzia enzi za roman empire, Persian empire, british empire ni mihangaiko ya jamii na jamii (races)

kutaka kutawala dunia. Hatuwezi kukataa hili kwasababu dunia ndio imeumbwa hivyo. Lazima mmoja awe juu na mwingine awe chini na mwingine awe na mamlaka dhidi ya mwingine.

Na ninashawishika kusema kwamba huu ni wakati wa waafrika kutawala dunia. Baadhi wanaweza wasiamini hili kutokana na akili zao kuwa na mipaka lakini ni kitu kilicho dhahiri kitakuja kutokea. Tunachotakiwa kufanya ni kubadilisha tu tabia zetu na mienendo yetu. Ninaona maono haya tuna nyakati nzuri sana mbeleni kama waafrika na kama watu weusi. Tabu zetu na mihangaiko yetu yote itaisha na kutakuwa na faraja. Lakini kwanza hatuna budi kubadilika na kubadilisha njia zetu mbovu.

Kamwe kama waafrika hatutakuwa wa mwisho hadi mwisho wa dahari. Ni lazima tunyanyuke. Ni lazima tuhusiane na watu hawa kwa akili iwe wachina au wazungu hawa sio wajomba zetu. Ni lazima tujitambue kama waafrika na kama watanzania.

Sisi waafrika tumekuwa masoko ya biashara zao kwasababu hatuzalishi zaidi na kwasababu tuna viwanda vichache.

Yumkini tuna uvivu na huu uvivu tunapaswa kuuondoa. Tutakapoanza kuzalisha zaidi kwaajili ya matumizi yetu ndipo tutakapokuwa tumepiga hatua ya kujitegemea.

Wazungu wachina na mataifa mengine hawapendi hili; kwasababu litaua masoko yao na litakaribisha umaskini kwenye mataifa yao.

Tusipozalisha wao wanafurahia kwasababu tutanunua kila kitu kutoka kwao. Hakuna taifa ambalo linataka

soko lake liuwawe na raia wao wakose ajira na waishi katika umaskini.

Kila taifa linapaswa kulinda soko lake la ndani kama linataka kukua na hatimaye kuingia katika masoko ya kimataifa, kuruhusu kila kitu kwa minajiri ya kitu kinachoitwa soko huria ni kuua mataifa madogo ambayo yanachipukia.

Lakini waafrika lazima tulifanye hili na hata kupigana kulifanikisha. Kitu wanachoita utandawazi ni domination ya mataifa makubwa dhidi ya mataifa madogo. Hatutaweza kupenya au kuwa na ushawishi dhidi ya mataifa makubwa zaidi ya kurithi tamaduni zao na katika soko linaloitwa huria kutawaliwa na bidhaa zao kila kona na uchumi wetu kuendelea kudidimia.

Tusipozalisha tutaendelea kuwa maskini na tegemezi. Ni kujidanganya kwamba katika mazingira ya uwekezaji yasiyo na usawa nchi kama yetu itaweza kutoka katika umaskini wake. Jukumu la kufanya taifa hili kuendelea sio uwekezaji kutoka nje ni jukumu letu sisi wenyewe. Mitaji ya watu hawa haibaki ndani ya nchi wanakuja kuvuna kisha faida yote wanapeleka kwenye mataifa yao na sisi tunabakiwa na kiduchu.

Ili tukue ni lazima tulinde soko letu la ndani lakini pili ni lazima tuongeze uzalishaji wetu. Ni lazima tutengeneze vitu na sio kununua tu kila kitu. Ili tuweze kutoka nje ni muhimu kuanza na ukuaji wetu wa ndani.

Ulinzi wetu ni muhimu; ili tuzalishe zaidi ni lazima tuwe na uhakika na uhuru na ulinzi wetu. Kama tunataka maendeleo yetu yawe endelevu ni lazima na muhimu kuwekeza katika utafiti na utengenezaji wa

silaha kwaajili ya ulinzi wetu. Vitu vyote hivi tutaviweza kama tukiwa wamoja.

Katika utoaji wa elimu ya watu wetu hatuwezi kuishia hapo tu kwa kuwafanya watu wetu kuwa na fani mbali mbali za utendaji kazi pekee, bila kuwaingizia elimu ya maadili na bila kuwajenga nidhamu zao. Kwa maadili namaanisha kuwafanya raia wa nchi hii kuwa na uwezo wa kuchagua kilicho sahihi na kuepukana na tabia haribifu ambazo hazina tija kwa taifa na wala kwa mtu binafsi. Kuepukana na uovu na kuwa na uwezo wa kufanya matendo mema na yenye matunda.

Kwasababu kwa njia hii pekee; kwa kuwafanya watu wetu kuwa na matendo yenye adili taifa letu litaendelea. Kuwapa maadili maana yake kuwafanya watu wetu kuwa wema na wenye uwezo wa kutenda matendo mema yatakayopeleka taifa hili mbele. Na kwa nidhamu nikimaanisha kutenda kwa kufikiri na kujua matokeo ya matendo yako kinyume cha kutenda bila kufikiri kwa kutumia matamanio. Kuongoza mawazo na matendo katika mkondo unaofaa kwa kutumia fikra badala ya matamanio. Matamanio haya hufanya binadamu kufanya makosa kila wakati nakuleta uharibifu katika maisha yake binafsi na kwa jamii kwa ujumla. Na hili ni matokeo ya fikra zilizokosa nidhamu.

Haya mambo mawili ni muhimu sana; yaani nidhamu na maadili. Watu wetu tukiwapa elimu pasipo kuwepo na nidhamu ya kutosha kama taifa hatutaweza kuwa na dira. Kwasababu matendo yetu ndiyo hupelekea aina ya taifa tutakalokuwa nalo, sisi ni zao la matendo yetu, ambayo huzalishwa na fikra zetu. Fikra ambazo hazijaongozwa vyema katika mkondo unaofaa uzalisha uovu. Hivyo kama matendo yetu hayatoongozwa vizuri kwa busara tutazalisha taifa la hovyo. Mawazo yetu ni mbegu ipandwayo ambayo

baadae huzaa matunda. Mawazo huumba. Na ni mawazo pia ambayo huzaa matendo. Kwahiyo tunapaswa kulinda jinsi tunavyofikiri.

Sisi kama taifa tunatakiwa kuwa makini jinsi tunavyofikiri, kwasababu fikra zetu ndizo ambazo zinazozaa aina ya taifa. Kama fikra zetu hazitoongozwa vizuri kwa busara tutazalisha taifa la ajabu. Na mwisho wetu kama taifa unategemea mkondo wa mawazo yetu. Na mkondo wa mawazo yetu ni lazima uongozwe na nidhamu ya kulinda kilicho chema na kuzuia kilicho kiovu kwenye mawazo ambayo yako ndani yetu na kwenye maisha ya utaifa.

Na matokeo ya nje ya matendo yetu ni lazima yazuiwe kwa kuweka sheria ambazo zitalinda na kuongoza matendo yetu. Kwasababu matendo yetu ni zao la fikra zetu; binadamu anawajibika kuyalinda na kuyaongoza katika mkondo unaofaa. Uovu wetu au wema wetu hutokana na fikra zisizo ongozwa vyema. Uharibifu tulionao katika taifa na duniani; ni matokeo ya fikra zisizoongozwa vyema. Ni mimba iliyotungwa kwa fikra mbovu kisha ikazaa uovu. Hakuna kitu kinachotokea kwa bahati mbaya kwenye maisha ya mtu au ya taifa lolote. Kinachomtokea mtu au taifa lolote ni zao la fikra zake na matendo ya mtu au taifa husika. Iwe kwa kutokuwa makini kwake au kwa kujitengenezea matatizo mwenyewe kwa kutoongoza mawazo yake vyema.

Kwahiyo kuendelea au kurudi nyuma kwa taifa lolote lile kunategemea sana fikra za watu wake. Kama wana hekima na busara kuna nafasi kubwa kwa wao kuendelea. Lakini pia kama wanaongozwa vyema na viongozi wao katika mkondo unaofaa. Kwasababu kazi ya kiongozi ni kuonyesha njia na taifa litayumba kama lina viongozi wabovu wasio na dira.

Kuwepo na maono kwa taifa lolote kunategemea sana nidhamu ya viongozi wao. Kujua sahihi na potofu, na kutambua njia ya kupita ili kufikia malengo yao kama taifa. Watu wanapoharibu njia sahihi ambayo binadamu anapaswa kupita na kuongozwa; hujikuta kwenye mkanganyiko wasijue kipi sahihi na kipi potofu, mkanganyiko huu ni hatari kwa dira na ustawi wa nchi. Kwasababu wameharibu ukweli kwa uongo; Wameharibu maadili ambayo yanapasa kuwaongoza kwa uongo.

Tunapoharibu maadili kunakuwepo na mkanganyiko; maono hutoweka. Na bila maono taifa hukosa dira. Na kukosa dira ni kukosa uongozi. Na kiongozi hupaswa kuongoza watu wake kwenye njia sahihi hivyo hupaswa kuwa na maono. Kiongozi hupaswa kuongoza watu wake kama mchungaji anavyochunga kondoo kwenye malisho yaliyobora. Kwa viongozi kujilimbikizia mali na kuwasahau anaowaongoza ni kutokujua majukumu yake.

Vilevile kiongozi hapaswi kuangalia maendeleo ya kiuchumi ya kijamii peke yake pasipo kuangalia maadili ya jamii kwasababu haya mambo mawili yana uhusiano wa karibu. Jamii huendelea zaidi pale watu wake wanapokuwa na maadili. Na maadili yanapomomonyoka; hata jamii ambazo zilizoendelea kiuchumi huanza kushuka. Kwahiyo hatupaswi kuangalia maendeleo ya kiuchumi peke yake pasipo kuangalia maadili ya watu wetu kama tunataka kuendelea kwa haraka zaidi. Taifa ambalo watu wake sio wamoja, hawaheshimiani, na hawatendeani haki watapataje kuendelea?.

kwa kutenda matendo ambayo ni sahihi tutaendelea haraka zaidi. Hatupaswi kujali utukufu wetu binafsi bali utukufu na heshima ya taifa letu miongoni mwa mataifa mengine.

Tunahitaji kulifanya taifa letu kuchipuka na kuwa miongoni mwa mataifa bora.

Hili nimeliona katika taifa letu; watu wanatafuta majina yao binafsi badala ya kutengeneza jina la taifa letu na heshima ya taifa letu miongoni mwa mataifa mengine, na hili halisababishwi na kitu kingine zaidi ya ubinafsi; na limekuwa chanzo cha migogoro na migawanyiko katika taifa. Watu kutafuta umaarufu wao binafsi badala ya umaarufu na utukufu wa taifa letu.

Hakuna mtu anayepaswa kuwa na jina kubwa zaidi ya jina na heshima ya taifa letu. Ili tuendelee ni lazima tuwe wamoja katika fikra na matendo. Katika majadiliano yetu ambayo yanayohusu taifa; ni lazima tuzungumze ukweli na kutafuta njia za kulipeleka taifa letu mbele na sio kutafuta umaarufu. Ni muhimu sana kuua migawanyiko yetu na kutafuta njia ambayo itakayotupeleka mbele na kutufikisha salama tunakotaka kufika.

Kwenye siasa sio sehemu ya kutafuta mkate bali sehemu ya watu wenye busara na hekima ambao wanafanya maamuzi kwa niaba ya raia walio wengi. Kama tutakuwa na watu wabinafsi ambao wameingia kwenye siasa kwaajili ya kujinufaisha binafsi hatutafika mbali kama taifa. Umaskini utaongezeka kwa raia waliowengi huku viongozi watakuwa matajiri wa kutupa na haki haitozingatiwa tena.

Hatutaepuka migawanyiko na migogoro kama viongozi fikra zao zikiwa kwenye kujilimbikizia mali badala ya kutawala na kuongoza watu. Na serikali inapojihusisha katika kujilimbikizia mali badala kutumikia watu huwa ni hatua ya kwanza kuwa serikali ya kikandamizaji, Haki za watu hazitalindwa

na kupatikana tena. Kazi ya serikali ni kulinda na kuongoza watu kama mchungaji anavyochunga kondoo na kuwaelekeza kwenye malisho yaliyobora. Hakuna haki itakayosimamiwa kama viongozi wataingia kwenye uongozi kwaajili ya manufaa binafsi.

Tunatakiwa kulinda mawazo yetu kwakuwa ndio huzaa matendo yetu na bila nidhamu hili hatutaweza na taifa letu halitoweza kuwa na dira. Na haki hupatikana pale viongozi wanapoweza kulinda na kuongoza mawazo yao na matamanio yao na kuweka mbele maslahi ya nchi na maendeleo yake. Ni Wajibu wa kiongozi kutawala na kuyaongoza mawazo yake, na maneno yanayotoka mdomoni mwake. Kwasababu maneno yake yanapaswa kuunganisha watu na heshima yake inategemea sana ni kitu gani kinatoka mdomoni mwake. Ni lazima awe na hekima ya kujua nini cha kuzungumza na kwa wakati gani. Wakati ni muhimu kwa kila kitu. Kila kitu kinapaswa kuzungumzwa katika wakati muafaka.

Ni lazima awe na ufahamu wa anachozungumza. Ni lazima ajitambue. Kiongozi anapaswa kujenga kuheshimiwa sio kuogopwa. Watu wakikuogopa inakuwa vigumu kupata ushauri mzuri na wa kweli. Wanaweza kukudanganya ili kukuridhisha. Kufanikiwa kwa kiongozi kunategemea sana ushauri anaoupata, na kama anaupata kwa watu ambao wako huru na wasio na hofu, na kama wana maarifa na ufahamu wa kutosha.

Kiongozi anapaswa kuwafanya watu wake kuwa huru kumshauri lakini asisite kuwaadhibu watu waovu ikiwa atawabaini hata wakiwa miongoni mwa watu wake wa karibu. Ili afanikiwe lazima aondoe uovu karibu yake. Kwasababu jina zuri la serikali uharibiwa na watendaji waovu.

Na kama anachukia uovu hawezi kuwaacha watendaji waovu karibu yake au ndani ya serikali yake. Itamkera tu kama ni mtu wa kuchukia uovu. Ili aendelee lazima awatoe watendaji waovu wote, awaingize watu wema na wenye nia ya dhati ya kutumikia watu sio kujitumikia wenyewe na familia zao.
kusudi awatumikie vyema wananchi kama kweli nia yake ni njema. Viongozi wabinafsi hawawezi kupelekea taifa kuendelea. Viongozi wabinafsi ndio chanzo cha vurugu na fujo.

kwahiyo tunampima kiongozi kwa wema wake au uovu wake kwa aina ya watu ambao wanaunda serikali yake. Ukiangalia kwa karibu aina ya watu alioteua kwenye serikali yake, utajua malengo ya serikali hiyo kama ni mema kwa watu ama sio mema. Kiongozi bora uchagua watu bora na wenye maadili kwenye serikali yake. Matumaini ya nchi hutegemea aina ya serikali iliyopo madarakani. Kama serikali imeundwa na watu wema na watenda haki nchi itakuwa tulivu na watu watapata maendeleo yao.

Kwahiyo teuzi za watu katika serikali inategemea sana busara za kiongozi na tabia yake. Kiongozi mpiga dili atachagua wapiga dili wawe watu wake wa karibu. Kiongozi mtenda haki atapenda kuwa karibu na kuchagua watu wanaotenda haki kuwa watu wake wa karibu. Ni muhimu kuangalia tabia za viongozi kwa ukaribu sana wakati tunafanya maamuzi ya kumkabidhi mtu mamlaka ya kuwa kiongozi na mtawala wetu. Ni lazima tuwe na uhakika kuwa ni mtenda haki. Umoja na mshikamano wa taifa letu unategemea sana ni jinsi gani haki inasimamiwa.

Tabia ya kiongozi ina madhara makubwa kwa jamii. Matokeo ya tabia ya kiongozi huwa hayachelewi

kuonyesha madhara yake kwa wananchi. Tunahitaji kiongozi mwenye uwezo kutawala tabia yake kwa nidhamu na kufanya maamuzi sahihi kwa maendeleo ya nchi. Ili tuendelee tunahitaji kiongozi mwenye nidhamu na busara.

Mawazo yaliyotawanyika kwa wananchi yanatokana na viongozi waliokosa nidhamu na dira. Kuwa na dira maana yake mkondo wa mawazo ya viongozi na wananchi ni lazima uwe mmoja. Bila ya hivyo maendeleo ya taifa hili yatakuwa magumu.

Wananchi na viongozi ni lazima wajue wanahitaji nini kwa taifa lao na njia za kufika huko wanakotaka kufika. Ni lazima kuwepo na maono na utii wa wananchi kwa viongozi wao. Utii wa wananchi kwa viongozi wao hutokana na dhamira njema ya viongozi, utu na wema wao. Wananchi na viongozi wasipokuwa wamoja hakuna maendeleo makubwa yatakayofikiwa. Na taifa letu halitokuwa imara.

Na maadili ndio msingi wa taifa lolote. Ni lazima wajue kati ya sahihi na potofu. Na kujua pia vipaumbele katika maisha ya kitaifa, lakini pia katika maisha ya kibinafsi na ya kijamii .
Kwahiyo ili tuendelee vitu hivi viwili hatuwezi kuviepuka, maadili yetu na nidhamu zetu. Pamoja na dira ya taifa letu lazima ijulikane kwa raia wote. Raia lazima wajue taifa lao linaelekea wapi na wajibu wao ni upi kufanikisha dira hiyo. Na wawe tayari kufanya kazi kufanikisha dira na malengo ya taifa lao. Lakini pasipo nidhamu na maadili taifa letu halitokuwa na dira.

Ni muhimu tukaua ubinafsi ambao umemea kwenye roho za watu wetu na kuinua upya roho ya utaifa ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa

lolote. Ni lazima tuvue vazi la ubinafsi kama tunataka kuendelea.

Bila umoja huu wa malengo na mawazo, hakuna taifa litakalo nyanyuka kutoka katika matope.

Ni migawanyiko yetu inayoturudisha nyuma kama taifa. Na migawanyiko hii hutokana na ubinafsi. Katika mazingira ambayo kila mtu anataka kuwa kiongozi hata kama hana uwezo, maono na maadili ya kuongoza watu, ni lazima tutagawanyika, hatutakuwa wamoja tena.

Lakini kuna vigezo vya mtu kuweza kuongoza wengine; vigezo hivi sio kila mtu anavyo. Kimojawapo ni maadili na nidhamu yake, hili ni jambo la msingi sana.

Maadili na nidhamu jinsi anavyoongoza matendo yake. Ni lazima awe na busara, kwasababu kama binadamu anashindwa kuongoza matendo yake vyema katika mkondo unaofaa, atawezaje kuongoza wengine? Kama ameshindwa kujitawala mwenyewe atawezaje kutawala wengine? Kujitawala ni kutawala matendo yako na kuyaongoza vyema na kuyafanya yazae matunda. Kujitawala ni kujizuia dhidi ya matendo yote haribifu. Na huwezi kutenda haki kama huna uwezo huu.

Na kwa hakika utendaji haki ni kigezo cha kiongozi bora. Pale haki inapotendeka amani hutawala. Kunakuwa hakuna malumbano na kelele. Kama kiongozi anashindwa kutawala mdomo wake na matendo yake, atawezaje kutawala wengine? Kama kiongozi anashindwa kujizuia kumpiga mtu, kumtukana mtu, kujizuia matamanio yake ya mwili na kuyaacha yamwendeshe ovyo, atawezaje kutawala nchi kwa haki na adili?

viongozi lazima wajitofautishe na wengine kwa maadili na mienendo yao ama sivyo hawawezi kuwa viongozi wa watu. Heshima ya nchi inategemea matendo ya viongozi wake. Hatuwezi kuwa na viongozi walevi, wazinzi na wasio zingatia haki za watu na kutimiza wajibu wao, tukafikiri tutakuwa na dira kama nchi, tukadhani tutaendelea kufikiria hivyo ni kujidanganya.

Kutawala watu kunahitaji nidhamu ya hali ya juu. Kutenda haki kwa watu kunategemea kitu kimoja tu nacho ni nidhamu. Nchi inakuwa bora pale haki inapotendeka na haki haiwezi kuwepo pasipo uwepo wa nidhamu. Kwahiyo viongozi ni lazima wajifunze kuheshimu wengine na kuonyesha tabia zenye heshima na adabu.

Kama wananchi tunawaangalia wao kama kioo chetu. Viongozi wanapokuwa hawana nidhamu na maadili na wananchi watakuwa hivyo hivyo. Kama bunge letu limekosa maadili na heshima yake, basi kuna tatizo kwenye jamii yetu ambapo hao wabunge wametoka huko kwa kuchaguliwa. Kwahiyo ni muhimu kujenga nidhamu huko chini kwenye jamii zetu na mahusiano yao. Kunapokuwepo hakuna nidhamu hata mahusiano yetu yanakuwa sio mazuri. Na mahusiano yetu yanapokuwa sio mazuri hatutaweza kujenga nchi hii.

Bunge letu ni taswira ya watu wetu na hekima zao za kufanya chaguzi za watu ambao wataenda kuwawakilisha. Tunajiona sisi kama jamii kupitia bunge letu. Uwezo wetu wa fikra kama wananchi unaonekana kwenye aina ya watu tuliowachagua na kuwapeleka bungeni kuwa wawakilishi wetu tabia zetu zinajidhihirisha kwenye aina ya bunge tulilonalo. Kama kwenye jamii hakuna nidhamu na utaratibu ni ngumu kuvipata vitu hivyo ndani ya bunge. Kwahiyo

mtu yeyote mwenye dhamira ya kubadili jamii yake ni lazima kwanza achukue hatua ya kujibadilisha yeye mwenyewe.

Kuna umuhimu mkubwa kujenga raia na viongozi wenye adabu, jambo hili limeshuka kwa kiwango cha juu katika taifa letu.

Pengine kabla ya kwenda mbali tungejiuliza adabu ni kitu gani? Adabu ni tabia njema; na tabia njema ni jinsi mtu anavyoongoza matendo yake na pengine hata mdomo wake katika njia sahihi. Mtu mwenye uwezo wa kudhibiti mdomo wake na matendo yake kwenye njia zinazofaa ndio mwenye adabu.

Na vitu hivi viwili matendo na maneno huongozwa na nguvu ya fikra ya kutawala jinsi mtu anavyowaza, kitu ambacho hupelekea mtu kutenda.

Kabla ya kuiba kwa mfano; mtu hujawa na fikra za tamaa ya kutaka kuchukua mali ya mtu mwingine, na kama asipodhibiti tamaa hizi na kuziruhusu zimtawale kinachofuata ni kitendo cha yeye kwenda kuiba na pengine kwa bahati mbaya akikamatwa kinachofuata ni aibu na fedheha kwake.

Kwahiyo ili tuwe na adabu tunapaswa kudhibiti jinsi tunavyowaza ili tujenge matendo yetu na tabia zetu. Na amani yetu inategemea hii kitu ambao ni uwezo wetu wa kujidhibiti na kutenda matendo yenye adili.

Kwahiyo adabu ni kuwa na tabia ambazo zinaongozwa na akili kutenda yaliyosahihi na mema; Kuwatendea wengine ya adili na mema inaonyesha kiwango cha adabu na nidhamu. Hivi vitu viwili vinaendana sambamba.

Kuwaheshimu watu wengine kunaonyesha pia kiwango cha adabu mtu alichonacho. Mtu mwenye adabu huongozwa na fikra kutenda jambo na sio hulka. Lakini hufikiri kabla ya kutenda katika kila jambo analofanya.

Mtu mwenye adabu hawashushi wengine chini huku yeye akijikweza, hawezi kudharau wengine. Mtu mwenye adabu ni mtu ambaye ana uwezo wa kujidhibiti jinsi anavyowaza, kuongea na kutenda. Adabu huletwa na nidhamu. Kwahiyo mtu anayetukana ovyo, mwenye vurugu na fujo, mzinzi, mwizi na asiye heshimu wengine hana adabu. Tunu hii adhimu kwenye taifa letu tumeipoteza.

Kama viongozi wajibu wetu ni kuwafanya wananchi wetu wawe wema na wapenda haki. Lakini hawawezi kuwa hivyo kama sisi hatuko hivyo. Sera zetu na sheria zetu hazitoweza kuwafanya wananchi kuwa bora kama viongozi wetu sio bora.

Hatutaendelea kama wananchi hawafanyi yaliyosahihi kwa taifa lao. Ni lazima wajifunze kujenga tabia zao kupitia shule na malezi nyumbani. Bila kujenga tabia bora na zenye manufaa kwa taifa letu hatuwezi kuendelea. Ni lazima na ni muhimu kuwajengea nidhamu, uadilifu na juhudi katika kufanya kazi. Akili za watu wetu lazima ziongozwe kuelekea katika utaifa na sio ubinafsi.

Tusipojenga roho ya kujitolea kwa taifa, kwa watu wetu tusahau kuhusu maendeleo na hata ulinzi wa taifa letu kuwa imara. Akili za ubinafsi hazijawahi kujenga taifa lolote popote duniani. Watu wanapopendana na kujaliana na wanapofanya kazi pamoja kuendeleza taifa lao ndipo wanapoendelea. Kwenye tumaini hili ni lazima tuishi na tutembee.

Mpende raia mwenzako kama unavyojipenda mwenyewe. Sisi sio wageni kwenye taifa hili sisi ni wazaliwa wa taifa hili tusipolipenda nani atalipenda kwa niaba yetu? tusipofanya kazi kulijenga nani atalijenga?

Tunadai zaidi kwa taifa letu kuliko tunavyojitolea kwa taifa letu, Tunadai kikubwa lakini tunajitoa kidogo.

Bungeni kila kukicha wanadai maslahi makubwa kwaajili yao, lakini ni kitu gani kikubwa wanacho kifanya kwa taifa hili? Wanajitoa kidogo wanadai zaidi. Taifa hili limekuwa kama ng'ombe anayekamuliwa maziwa bila kuwa na malisho mazuri. Tunakula zaidi tunafanya kazi kidogo. Yumkini kama tungeamka na kufanya kazi zaidi mapato yetu yangekuwa makubwa zaidi. Taifa hili lazima linyanyuke hakuna wakati mwingine wa kunyanyuka ni sasa. Hizi nguvu ambazo tunazo badala ya kuzitumia katika mambo mengine ni lazima tuzikusanye na kuzitumia kwa maendeleo ya taifa hili.

Watu wetu lazima wajue sahihi na potofu. Bila ya kujua hili tutakuwa hatuna dira kama taifa. Kama watu watashindwa kuchagua yaliyosahihi hatutakwenda mbele kama taifa. Na kwa hakika kuelimika ni kuachana na mambo yasiyo sahihi.

Na huo ndio mwanzo wa maendeleo pale binadamu wanapoacha mambo ambayo si sahihi. Na ujinga ni kuendelea nayo na kuyakumbatia mambo ambayo si sahihi. Mambo haya yanaharibu misingi ya jamii zetu, na misingi ya jamii zetu isipokuwa imara tusitegemee kwamba taifa litakuwa imara. Kwahiyo ni muhimu kujenga taifa ambalo watu wake ni wema na wanaotenda matendo ambayo ni sahihi. Kwa kufanya hivyo tutaona mwanga kwenye maendeleo yetu. Na

akili zetu, miili yetu na roho zetu zitakuwa na afya zaidi. Na matumaini yatarudi kwa watu wa taifa hili.

Ni lazima tutakwama kama taifa na kuwa na migawanyiko kama tutaendekeza ubinafsi. Watu wanaoenda kwenye siasa kwa maslahi binafsi ni hatari kwa maendeleo na umoja wa nchi na hata kwa amani na uhuru wa raia walio wengi. Tunahitaji mtu anayetenda kwa haki, mwenye nidhamu na uwezo wa kujiongoza na kuongoza wengine pia.

Nguvu ya kujiongoza ni nguvu itokanayo na nidhamu. Nje ya nidhamu binadamu hawezi kujiongoza kutenda matendo yaliyo sahihi na bora. Kwakuwa kiongozi hukabidhiwa majukumu ya kufanya maamuzi, mahitaji ya busara na hekima kwake ni vigezo visivyo epukika, na kama maadili yake yana walakini; hatoweza kufanya maamuzi sahihi yenye faida kwa umma.

Ili tuamue vizuri tunahitaji busara. Uwezo wa kuchagua kilichobora na sahihi miongoni mwa vitu kadhaa. Kujua mwelekeo gani taifa linapaswa kuchukua inahitaji busara na hekima. Kuleta amani umoja na ushirikiano kunahitaji busara pia. Kazi ya kutawala watu inahitaji hekima zaidi kuliko nguvu.

Furaha ya taifa au huzuni ya taifa inategemea maamuzi ya viongozi. Tunahitaji watu waliopevuka kwenye uongozi wa taifa letu. Watu waliokua kiakili vya kutosha kuongoza wengine kuelekea kwenye tija.

Tunahitaji kiongozi ambaye sio mwenye makuu na mwenye kutaka sifa, Sio muonevu na asiyependa haki, bali atakayetawala kwa haki na usawa. Lakini pia asiye na tamaa ya kujilimbikizia mali. Kwasababu kiongozi anapokuwa na tamaa ya kujilimbikizia mali,

ndio mwanzo wa kukandamiza haki za raia na kuwafanya raia watwana badala ya raia huru.

Na uhuru wa kweli watu wanaupata watakapoweza kujitawala wenyewe binafsi na kutenda matendo yaliyosahihi kwa kujizuia wasiibe, wasizini, wasifanye ufisadi na kutenda uovu mwingine wowote, ama sivyo uhuru huo utaminywa kwa sheria na nguvu kutoka ndani na nje. Nguvu kutoka ndani adhabu dhidi ya nafsi yake kutoka kwa Mungu lakini nguvu kutoka nje adhabu kutoka katika taasisi ambayo imeundwa kutawala binadamu yaani serikali.

Tunajua fika bila kuzingatia misingi ya maadili na haki hakuna jamii itakayobaki. Jamii za binadamu husimama na kuendelea pale misingi ya haki na ya kimaadili inaposimamiwa vyema. Na nguvu hii ya nje ni muhimu ili kurekebisha tabia za watu ziendane kama watu wanaofikiri sawa sawa na kuendana na jamii kwa kutendeana haki, na haki ndio huleta utengamavu. Ndio maana tuna jela na polisi. Na vyombo hivi vinatakiwa kuwa vyenye maadili. Kwasababu watu wanaopaswa kuwafanya wengine wafuate sheria, wao wanapaswa kwanza kufuata sheria.

Ili jamii iwe huru lazima mahakama zitende haki. Na watu lazima wawe wema. Ingawaje binadamu hawezi kuwa mwema kwa asilimia mia moja tunaweza kupunguza uovu wake. Binadamu amezaliwa huru. Uhuru wake huondoka pale anapotenda uovu. Kwahiyo utawala wa sheria ni muhimu kwa kiongozi ili kuleta utangamavu na haki. Na bila hekima haya mambo yote hayawezi kufanyika.

Huwezi kutoa usichokuwa nacho, kwa kiongozi kuifanya nchi kuwa yenye maadili na haki; ni lazima kiongozi huyo awe na hayo maadili na haki.

kwasababu haki huleta utangamavu katika nchi, na huwezi kuitoa kama huna katika hifadhi yako, hata kama imeandikwa kwenye sheria za nchi. Hivyo kiongozi hupaswa kuwa mtenda haki ili aitoe hiyo haki.

Ni haki inayowaleta watu pamoja na kuwa wamoja na kunapokuwa hakuna haki na utawala wa sheria, hakuna taifa litakalosimama. Kwahiyo tabia za watu lazima ziangaliwe kwa ukaribu, ili kufanya taifa linalofanya kazi vizuri na raia wanaotendeana haki. Watu wanapoona haki inatendeka na katika nchi kuna usawa, kila mtu anakuwa na furaha na watu hulipenda taifa lao.

Tunataka kiongozi atakayeongoza taifa hili kwa haki na adili na kuwapa watu stahili zao. Sio ambaye anaingia kwenye uongozi kwa sababu ya maslahi binafsi. Lakini pia lazima watu wetu waje kwenye ufahamu wa kutambua umuhimu wa taifa hili kwao na kuwa tayari kulitumikia kwa moyo wa dhati. Bila kulipenda taifa hili kwa dhati na kuwa tayari kulitumikia, hakuna maendeleo ya maana tutakayofikia. Ni lazima tujikusanye na tuwe tayari kulitumikia taifa letu. Ni muhimu na ni lazima tujenge upya tabia za watu kwenye utaifa wao. Ni muhimu kurudisha akili zetu kwenye utaifa na kujenga upya maadili ya taifa.

Kwasababu mtu ambaye hana maadili na ana elimu ni hatari kuliko yule asiye na elimu kwa ukuaji wa jamii yeyote; na elimu yetu haipaswi kukuza watu waovu bali wenye maadili, wenye uwezo wa kutenda mema na wenye ufanisi watakaokuza na kujenga taifa lao.

Kwahiyo elimu yetu inawajibika kujenga watu wetu kuwa wema na wazalishaji. Ni lazima ilenge kujenga watu bora na wanaowajibika kwa jamii zao kwa moyo

wote. Mtu aliyeelimika au tuseme anayejiita ameelimika kwakuwa ameenda shule, alafu mwovu na fisadi atakuwa na faida gani kwa taifa? Mtu ambaye badala ya kujenga jamii yake anaibomoa tutafaidikaje nae hata kama ana elimu ya darasani? Kwahiyo maadili hapa ni ya msingi sana. kwakuwa tunataka kumjenga raia anayejitambua na mzalishaji badala ya kujenga raia mwovu.

Elimu yetu inapaswa kujenga raia wema na waaminifu kwa taifa lao sio raia wasiojitambua wanaofanya chochote kile kinachokuja akilini mwao badala ya kulinda tabia zao ili kujenga jamii bora na taifa imara. Ni Muhimu kujenga tabia za watu kuwa zenye kujenga taifa lao badala ya kulibomoa. Ni lazima wawe na hiyo busara.

Kwasababu ya kukosa nidhamu huku na kukosa maadili; maisha ya kijamii yamedidimia. Maisha ya kijamii ni nguzo kwenye maisha ya utaifa. Kama watu wanahusiana vizuri chini kwenye jamii; maisha ya kitaifa huwa imara. Taifa huwa na afya pale maisha ya kijamii au mahusiano ya kijamii yanapokuwa vizuri. Hii ikiwemo pia ndoa na familia; kwasababu jamii huanza kujengeka huko kwenye mahusiano ya watu wawili mwanamke na mwanaume. Ambao hawa hujenga familia na baadae huja jamii.

Ni lazima tuwafundishe kulipenda taifa lao na kuwa tayari kulitumikia na kujua wajibu wao kwa taifa. Raia wasipojua wajibu wao tutashindwa kujenga taifa hili. Raia lazima wafikie ufahamu huo wa kujua wajibu wao na kuutekeleza ipasavyo. Wajue ulinzi na usalama wa taifa hili ni wajibu wao, na taifa hili ni mali yao na ya watoto wao ambao hawajazaliwa. Kwahiyo wanawajibika kulijali taifa hili na kuliangalia sio kwaajili yao pekee bali pia kwa vizazi vijavyo. Wajue tukiriharibu tunaharibu pia baadae ya

wasiozaliwa, kwasababu ni katika ardhi hii ndipo tulipoumbwa tuishi, hapa ndio nyumbani.

Ni mikono yetu wenyewe ambayo italijenga taifa hili au kulibomoa. Ni kwa mawazo yetu na matendo yetu. Tukikata tawi la mti ambao tumekalia hatuwezi kubaki salama. Ni muhimu kutendeana haki na kuwa wamoja. Hili ni jambo la msingi ambalo napenda kusisitiza kwa watu wa taifa hili; Hakuna taifa ambalo linapenda watu wake kuwa wakimbizi, tusipojenga umoja tutazalisha wakimbizi. Na sababu itakuwa ni kutokuchukuliana vyema wenyewe kwa wenyewe. Kwahiyo kiongozi bora ni lazima ajenge mahusiano mazuri ya watu na huo ndio msingi wa taifa lolote. Kiongozi ambaye hajali mahusiano ya watu hafai.

Ni muhimu kupendana na kuwa wamoja. Tukizalisha wakimbizi tutakuwa kama vichaa waliokata tawi la mti ambao wamekalia. Ni lazima watu wajue hili taifa ndio linalotuhifadhi, ardhi hii ndio inayotupa chakula, tukivurugana wenyewe kwa wenyewe hatutapata faida tunazopata sasa. Na kutakuwa hakuna maendeleo yeyote tutakayofikia katika mazingira ambayo taifa limegawanyika na amani hakuna.

Haki na uhuru tunaopata sasa; hatuwezi kuupata sehemu yeyote kwenye ardhi ya mataifa mengine. Ni mpumbavu pekee anayeweza kutenda matendo yenye kuweza kuhatarisha uhai na umoja wa taifa lake. Kwasababu sisi kama waafrika na kama watu weusi ni watu wamoja na chimbuko letu ni moja. Hatupaswi kupigana wenyewe kwa wenyewe, watu wenye akili wanatushangaa. Ni kama ndege anayebomoa kiota chake mwenyewe anachotegemea kupatia usingizi humo yeye na watoto wake, mtu anayeangamiza taifa lake kwa ubinafsi. Ni mpumbavu. Mbinafsi anaweza kuangamiza taifa lake na kuligawa kwa maslahi binafsi tena ya kipindi kifupi.

Mtu aliyeelimika ni nani ambaye tunapaswa kumjenga? Ni yule mwenye uwezo wa kuongoza akili na matendo yake katika mkondo unaofaa ambao ni wenye faida kwa jamii. Mwenye uwezo wa kujenga mahusiano yake vyema kwenye familia yake na kwenye jamii.

Mtu anayeongoza mawazo yake na matendo yake si kwenye uharibifu; bali kwenye ujenzi wa jamii bora na taifa imara. Yule ambaye anaepuka uovu na kuongoza akili yake kwenye kilicho bora. Kwahiyo kitu chote kinachoitwa elimu kimebebwa na NIDHAMU. Kumkuza binadamu kuwa bora, kumebebwa na kitu kimoja tu, NIDHAMU. Bila nidhamu binadamu hatoweza kuboreka, na kuwa bora zaidi ya wanyama. Jamii zote zimeimarika na kukua kwasababu ya uwepo wa nidhamu. Bila nidhamu ukuaji wa binadamu kiakili na kiroho huwa hafifu. Mtu ambaye ameenda shule lakini hana nidhamu huwezi kumuita ameelimika.

Nidhamu ni nini? Nidhamu ni uwezo wa akili kuongoza mawazo na kuyaelekeza kwenye mkondo unaofaa. Ni kuzuia mtawanyiko wa mawazo na kuyaongoza kwenda sehemu fulani. Huu ni uwezo na nguvu za kiakili kutawala mwili, mawazo na matamanio. Katika elimu na katika masuala ya kiroho, hakuna binadamu atakayeweza kukua kifikra na kimaarifa pasipo uwezo huu wa akili wa kutawala na kuongoza mawazo na matamanio ya mwili.

Ambayo hupunguza uwezo wa kiakili wa binadamu wa kufikiri na kumkosesha dira. Binadamu anapaswa kuongozwa na akili na sio matamanio yake. Mwisho wa maisha ya binadamu ni amani na harakati zake zote ambazo anazifanya katika dunia lazima zimfikishe kwenye amani, kwenye kupata amani ya

kweli, ambayo haitokani na kuwa na mali nyingi, bali akili ambayo imeelekezwa kutenda yaliyo bora na sahihi.

Haya matamanio ya mwili ambayo kila wakati hutuingiza kwenye matatizo hayana budi kutawaliwa na akili na sio kuyaruhusu yatatutawale. Binadamu anapaswa kuongozwa na akili na sio matamanio yake. Na mtu aliyeelimika ni Yule anayeongozwa na akili na sio matamanio yake. Na hili ndio lengo haswa la elimu. Kuzuia matamanio ya kimwili ya binadamu na kuruhusu akili kukua na binadamu kuongozwa na akili na sio matamanio yake. Kwakuwa pasipo binadamu kukandamiza matamanio yake hatoweza kujua kilicho sahihi na potofu.

Kuna kitu cha msingi na cha muhimu ambacho tunapaswa kutoa kwa watu wetu. Kitu ambacho kitatuunganisha na ambacho ndiyo msingi haswa wa uwepo wa taifa lolote. Bila msingi huo, hakuna taifa ambalo litaendelea kwa muda mrefu hata kama lina watu wenye maarifa ya kiasi gani katika uzalishaji mali na katika ugunduzi. Dunia unayoiona imeunganishwa na nguvu na sheria ambazo zinailinda na kuiendesha. Tunatakiwa tuzijue kama taifa na tusienende kinyume chake.

Na hili ni maisha ya kijamii, ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa jamii yeyote ile. Pale maisha ya kijamii yanapoachwa na watu kufuata ubinafsi, na sio kuangalia jamii na maendeleo yake; na kulinda maadili ya taifa, lazima shida zitakuja tu kutukabili na utatuzi wake utakuwa mgumu.

Haya yatatokea kwasababu tutakuwa tumeacha njia ambayo ni sahihi, tunayopaswa kupita, na kuchagua njia ya ubinafsi. Kwasababu hii; hatutaepuka mifarakano katika jamii na kwenye siasa zetu.

Umoja wa kitaifa utashuka kwa kiwango cha juu, hatuwezi kuepuka hili la umoja wa kitaifa kushuka kama kila mtu akiangalia maslahi yake binafsi. Na taifa halitoweza kuwa imara. Ulinzi wake hauwezi kuwa imara pia.

Kwahiyo kama taifa hatupaswi kuangalia ubinafsi wetu bali tunatakiwa kuangalia na kujali maendeleo ya jamii zetu. Na biashara ziwe ni kwa maendeleo ya kiuchumi ya jamii husika kuliko kuweka kipaumbele katika ubinafsi.

Tuangalie kwa umakini tunapotafuta maendeleo yetu ya kiuchumi yasikinzane na ustawi wa jamii zetu. pasipo kuangalia haya mambo ya kimsingi yanayotuunganisha na ambayo ndio huleta pia ukuaji wa kiuchumi wa jamii husika kuwa endelevu hatutafika mbali. Kwasababu pasipo kuwa wamoja na kufanya kazi pamoja hatuwezi kuendelea. Tutaendelea kama tutaacha mawazo ya kibinafsi na mawazo yetu tukayawekeza kwenye ujenzi wa taifa hili.

Tukitafuta maendeleo ya taifa letu kwa pamoja tutaendelea haraka zaidi. Na tutajenga utangamavu kwenye jamii. Tukiangalia ubinafsi tutakuwa na jeshi ambalo linaangalia maslahi ya watawala badala ya wananchi na ya taifa, na tutakuwa na raia ambao hawana uzalendo na wapinzani wa serikali yao na waliogawanyika.

Jamii ambayo pesa ndio msingi namba moja kuliko mahusiano yao na pesa hiyo ndiyo inayowasukuma kuingia kwenye siasa, na kwenye uongozi wa nchi, haiwezi kujenga taifa moja na bora. Lakini pia viongozi waliofuata fedha hawataweza kujenga jamii bora pia zenye maelewano na ushirikiano. Jamii bora

hujengwa pale watu watakapofanya kazi pamoja kuimarisha maisha yao bila kuangalia ubinafsi. Sisi kama taifa tumetoka kwenye msingi huu. Tumekuwa taifa la ubinafsi na sio taifa la watu wanaotumikiana.

Tumekuwa taifa la watu wanaotaka kutumikiwa, na taifa la watu wanaoenda kwenye siasa kwa maslahi binafsi na umaarufu, huu ndio umekuwa mwenendo wetu. Kwasababu hii; siasa zetu zimekosa heshima na dira. Lakini yumkini tunapaswa kujenga taifa lenye heshima na lenye maadili. Heshima yetu, maadili yetu, maisha yetu ya kijamii na kitaifa, tumeyatupa kwa fedha. Na hii sio busara hata kidogo. Kwahiyo katika utoaji wa elimu ya watu wetu hatuwezi kuishia hapo tu. Kwa kuwafanya watu wetu kuwa na fani mbali mbali za utendaji kazi pekee, bila kuwaingizia elimu ya maadili na bila kuwajenga nidhamu zao. Haya mambo mawili ni muhimu sana; yaani nidhamu na maadili. Watu wetu tukiwapa elimu pasipo kuwepo na nidhamu ya kutosha, kama taifa hatutaweza kuwa na dira.

Tumeumbwa katika taifa hili tuliangalie na kuliendeleza, lakini pia tupendane na kujaliana kama watu wa taifa moja. Hatuwezi kufanya hivi kama hatupendani, kama hatujaliani, na kama sio watu wamoja. Na tujue kwamba kwenye ubinafsi na choyo hatuwezi kujenga vyote hivi. Kama tunataka kuendelea kama taifa ni lazima tubadilike kutoka ndani yetu kwenda nje. Kama hatupendi vita ni lazima tuangalie haya mambo kwa umakini. Ni lazima tujenge mahusiano yetu na kutumikiana.

Katika taifa letu sifa isiwe kiasi gani umejilimbikizia mali, bali ni kiasi gani umeleta mabadiliiko kwenye jamii inayokuzunguka na taifa lako. Sifa iwe utumishi wako kwa taifa; sio mali. Sifa iwe uwepo wako unafaidisha nini taifa lako.

Vitu kama ufisadi na mambo mengine ni matokeo ya watu kuacha maisha ya kijamii na kujiangalia wao tu na kujilimbikizia mali, hasa kwa viongozi na watu wengine kwa njia ambazo si halali na kuacha kujali jamii ambazo wanatoka, na ambazo zinawategemea wao kuleta mabadiliko chanya. Huu ni uasi. Uasi dhidi ya jamii. Na uasi huu ukitendwa na viongozi jamii yote hukengeuka na kuwa ya kibinafsi. Hatuwezi kujenga nchi katika ubinafsi na nchi ikawa imara. Ni wajibu wa serikali kusimamia maadili, sheria, usawa na haki. Serikali lazima iwekeze akili zote kwa wananchi na kuwa yenye maadili na nidhamu.

Kubomoka kwa maisha ya kijamii ni madhara makubwa yatokanayo na ubinafsi na choyo. Hatujali tena shule za serikali za pamoja ambazo ni muhimu, zinazopaswa kutoa elimu bora kwa wote. Kwakuwa uhai wa taifa lolote unakuwepo pale tu watu wake wote, wanapopata elimu bora ambayo haina matabaka na jamii inapoangaliwa kwa ukaribu katika ukuaji wake kiroho na kiakili, kwasababu binadamu si mali peke yake; lazima aangaliwe ukuaji wake wa kiroho na kiakili ambao humfanya kuwa na afya bora ya mwili.

Kwahiyo pamoja na matatizo tuliyonayo katika elimu yetu watu wanasomeshwa. Na lengo la kusomesha watu ni kufanya mapinduzi katika jamii zetu.

Tunahitaji watu wapate elimu ili wakafanye mapinduzi. Ili watumie elimu yao kutumikia nchi yao na jamii zao. Na wawasaidie wengine kupevuka kiakili ili tuwe na jamii pana iliyoelimika. Ili tulete mabadiliko. Elimu haipaswi kuchukuliwa kibinafsi.

Taifa linapo msomesha mtu na kuweka bajeti kwaajili ya elimu, malengo ni watu wanaosomeshwa waende

na kuleta mapinduzi kwenye jamii zao. Sio kwa faida zao binafsi peke yake, ni kuleta mabadiliko katika taifa.

Tunachukulia elimu kama ni kitu cha kibinafsi; haitakiwi kuwa hivyo. Elimu yetu inatakiwa itengenezwe katika hali ile ambayo itafaidisha taifa kwa kiwango kikubwa. Na hii haitawezekana pasipo kujenga uzalendo wa watu wetu.

Ama sivyo tutajenga watu ambao wanafikiria tu kupata elimu na kuitumia elimu hiyo kwa maslahi binafsi pekee. Na hili sio lengo la taifa kusomesha watu wake. Malengo ya taifa kusomesha watu wake ni maendeleo ya pamoja kama nchi na kutatua changamoto zinazokabili maisha ya binadamu hasa maisha ya raia wa taifa hili.

Hii roho ya kujitolea tunawajibika kuijenga kwa watu wetu. Watu lazima wasome, na lengo lao liwe ni kuendeleza taifa lao, na sio kufikiria zaidi maslahi binafsi kuliko yale ya kitaifa. Ni jukumu letu kujenga taifa la watu wanaowajibika kwa nchi yao. Tunaona tatizo hili pia kwenye siasa zetu, watu kujifikiria wenyewe kuliko maslahi mapana ya taifa. Na niaminini; tutaendelea zaidi kama tutaachana na ubinafsi, tukasikilizana kwa lengo la kuendeleza taifa letu. Sisi ni watu wamoja na tuna lengo moja maendeleo ya nchi yetu. Lakini ubinafsi ndio uliotugawa na kuturudisha nyuma kwenye maendeleo yetu.

Tunatakiwa kuwa wamoja, hakuna maendeleo kama sisi sio wamoja, katika mawazo na matendo. Hakuna maendeleo kama hatutosikilizana na kutazamana kama watu wamoja, ambao mwisho wao ni mmoja.

Tumegawanyika kimawazo sio kwasababu ya kutofautiana kifikra kuhusu njia bora za kuendeleza taifa hili, bali kwasababu za ubinafsi wa uchu wa mali na madaraka. Tunatakiwa tubadilishe mtizamo wetu na kulipa taifa hili kipaumbele kuliko matamanio yetu binafsi.

Tunatakiwa kuacha kutupa maisha ya kijamii ambayo ndio msingi wa uwepo wa taifa hili, na afya yetu kama taifa inategemea ubora wa maisha yetu ya kijamii, ambayo hayawezi kuwepo kama tutafuata ubinafsi.

Na furaha yetu kama taifa inategemea sana ubora wa maisha yetu ya kijamii. Na maisha yetu ya kijamii yataboreka pale tutakapokuwa na nidhamu na dira ya kujiongoza sisi wenyewe, ya kuangalia tabia zetu kwa ukaribu, na kujizuia kufanya matendo ambayo ni yenye madhara kwa uhai na umoja wa jamii zetu na taifa letu.

Na msingi wa uhai wa taifa lolote ni maadili ya watu wake, kinyume cha hapo hakuna taifa litakaloendelea kwa muda mrefu pasipo kuangalia kwa ukaribu maadili ya watu wake. Taifa watu wake wanapokengeuka haliwezi kusimama. Tunapoacha njia ambayo ni sahihi kama taifa tusahau kuhusu maendeleo. Kama makanisa na misikiti na elimu yetu, ikishindwa kujenga raia wema na bora, tusahau kuhusu uwepo wa taifa hili. Kutakuwa hakuna amani kama watu wetu watakuwa hawana uwezo wa kutenda mema.

Tunatakiwa kujua kilichosahihi na kwa pamoja tukishike. Tunatakiwa tuwe na dira. Na katika kitabu hiki naainisha dira. Kwahiyo tunapaswa kupambana na ujinga, na ujinga ni matendo yote yanayorudisha nyuma maendeleo yetu na ukuaji wetu kama taifa, kiakili, kiroho na hata kwa mali. Kwasababu

maendeleo yetu ya mali yanategemea sana ubora wa afya zetu kimwili, kiakili na kiroho. Utendaji wa binadamu unakuwa bora pale mwili wake, akili yake na roho yake inapokuwa katika hali ambayo ni bora ambayo itamsaidia katika utendaji wake wa kila siku. Kwahiyo tunapaswa kunyanyua tumaini hili kwa watu wetu.

Watu ni lazima wawe wamoja ili wafikie malengo yao kama taifa, hatuko pamoja kifikra na hata kwa dira. Mawazo yetu hayajaongozwa katika mkondo mmoja. Yameongozwa katika ubinafsi na sio utaifa. Kwahiyo tunapaswa kuingiza kitu kwenye akili na mioyo ya watu wetu, ili walipende taifa hili, na ili wawe tayari kulitumikia. Pasipo raia kulipenda taifa hili kwa dhati ya nafsi zao na kuwa tayari kulitumikia maendeleo yetu itakuwa ni vigumu kuyafikia na hata mipango yetu. Kwahiyo tunapaswa kubadilisha mtizamo huu wa ubinafsi ambao unaliua taifa hili, na kuingiza roho mpya ya uzalendo kwa watu wetu.

Kwakuwa pasipo uzalendo kamwe hatutapiga hatua za maana katika maendeleo yetu kama taifa. Pasipo uzalendo mambo mengi yetu yataharibika hata ulinzi na usalama wetu kama taifa utakuwa kwenye mashaka. Tunahitaji watu ambao watakuwa waaminifu kwa taifa lao na ambao watakuwa tayari kulitumikia. Sasa hivi kila mtu anajifikiria yeye na familia yake. Lakini tujue kwamba tuna kitu kinachotuunganisha kinachotufanya tujiite taifa, ambacho ndani yake tunapata faida zote tunazozipata. Kitu hiki ni chenye thamani kubwa, kinapaswa kuamshwa kwenye moyo wa kila Mtanzania, ili kila mtu awe na imani kwa taifa lake. Ni pale tu tutakapokuwa wamoja kifikra na kujua nini tunataka kama taifa, na dira yetu ni nini, ndipo tutakapo fanikiwa. Mgawanyiko wetu hasa wa kisiasa

na wa kimaslahi binafsi hauwezi kutusaidia kama taifa.

Tunahitaji kukua kama taifa, na hatutaweza kukua kama hakuna kujitolea na kama tutakuwa sio wamoja katika malengo na mawazo yetu kama taifa. Na kukua kwetu kama taifa ni kufikia uwezo wa kujitegemea kwetu na kuweza kujitosheleza mahitaji yetu ya ndani kama taifa, lakini pia kujitegemea kifikra na kuweza kujiongoza wenyewe katika njia ambazo ni sahihi na zenye tija. Hii sio kazi ya mtu mmoja au wawili au serikali peke yake, ni kazi ya pamoja kama taifa, kuona taifa hili likikua na kuendelea. Kila mtu ni lazima atimize wajibu wake na kutumia kipaji chake kikamilifu kufanya taifa letu kuendelea.

Watu wanaweza kusema sasa hivi dunia ni utandawazi, na dunia ni kama kijiji, lakini hiyo haipaswi kutufanya sisi kuua utaifa wetu na maisha yetu ya kitaifa na kijamii, na hata taratibu zetu na tamaduni zetu, na kuruhusu tamaduni kutoka nje kutubadilisha, na kutufanya tufikiri tofauti na tunavyotakiwa kufikiri, na kuiga mwenendo wao wa fikra, tukifikia huko tutakuwa sio taifa huru bali tawi la mataifa hayo.

Tunapaswa kujua tunatakiwa kufikiri wenyewe na kujenga jamii zetu kwa fikra zetu wenyewe kama tunataka kujitegemea na sio kuruhusu ushawishi kutoka nje kutubadili na kutufanya kutenda na kufikiri kama wao na hata kuiga tamaduni zao.

Utambulisho wetu sisi ni nani na madhumuni yetu ya kuwa taifa hayapaswi kuuwawa. Tuna wajibu wa kujenga taifa letu kulingana na fikra na mawazo yetu wenyewe kwa kutumia nafsi na roho zetu wenyewe. Kujitegemea huanza katika fikra, pale taifa

linapokuwa linauwezo wa kufikiri na kutenda kwa kujitegemea.

Taifa letu ni lazima lijitegemee kifikra na lisiue utambulisho wake. Hatupaswi kuwa watumwa wa kitu kinachoitwa utandawazi. Ushawishi ambao unaotoka kwenye mataifa ya magharibi, ambao una nguvu kubwa, lazima usimamishwe kwa agenda imara, na itikadi ambazo zitajenga taifa hili kuwa huru na linalojitegemea. Tusipotambua hivyo; uharibifu ambao tayari unatokea katika mataifa ya ulaya na marekani wa kimaadili utatukumba na sisi, na tutakuwa hatuna nguzo za kuegemea. Hili lazima lizuiwe kwa nguvu zote ama sivyo maendeleo yetu itakuwa vigumu kuyafikia. Tunaweza kuwa na uhusiano na urafiki na mataifa mengine, lakini pia tukaendelea kulinda utambulisho wetu na utamaduni wetu. Kama taifa tunapaswa kuujenga na kuulinda utambulisho wetu. Na kuwa tayari kuupigania.

Kwahiyo ni muhimu kujenga taifa linalojitambua. Na hiki ndicho tunachopaswa kufanya sasa, kwa kufanya kila jitihada kuwafanya wananchi walio wengi wa taifa hili kujitambua. Wajue kwamba taifa lao lina thamani kubwa kuliko maslahi ya kibinafsi. Kwasababu sisi tuliopo sasa hivi tunaishi kwa muda. Kuna vizazi vingine vitakuja kuishi katika ardhi hii, na tunapaswa kuwatayarishia mazingira bora na kuwajengea taifa bora na imara. Ni muhimu kujenga utaifa sasa, ambao umeanza kumomonyoka. Hakuna utaifa pasipo uzalendo. Mawazo ya watu wa taifa hili ni lazima yajengwe katika utaifa. Na tuache kulifanya taifa hili kama tawi la mataifa ya magharibi kifikra.

Ili kutatua matatizo ya kijamii yanayotukabili hatuna budi kuja pamoja na kuongea kama watu wamoja. Tunapaswa kuwafunza watu wetu maarifa na

kuwafanya kuwa wenye nidhamu na faida kwa taifa letu.

Tunapaswa kuwafunza watu wetu maarifa ya kazi. Ni vyema na ni msaada mkubwa kwa taifa letu katika kutatua changamoto zinazotukabili. Lakini jambo la msingi pia, tunapaswa kwa umakini mkubwa mno kuangalia maadili ya watu wetu. Hakuna taifa ambalo litaendelea kuwa endelevu kwa kipindi kirefu pasipo watu wake kuwa na maadili; pasipo watu wake kujua sahihi na potofu.

Ingawaje tunapenda sana maendeleo ya kimali lakini tunapaswa kuangalia kwa umakini mno maadili ya watu wetu, kwakuwa ndiyo yanayotuunganisha. Nje ya hapo hakuna taifa. Uhuru wetu na umoja wetu unategemea maadili na nidhamu za watu wetu. Bila maadili hakuna taifa litakalo simama. Tunapaswa kufikiria hili kwa umakini mkubwa. Maadili ya watu wetu ndio yatakayofanya taifa hili kuendelea. Pale watu wetu watakapojua sahihi na potofu, na kufuata njia itakayo tupeleka kwenye maendeleo yetu na umoja wetu.

Mawazo yetu yasielekezwe huko tu, pasipo kuwajenga watu wetu kwenye msingi ya kimaadili. Hatupaswi kuangalia maendeleo ya kimali pekee pasipo kuangalia kwa umakini mkubwa nidhamu na maadili ya watu wetu, ili taifa letu liwe na dira. Tusijali mali kuliko maadili yetu.

Kwa mtu kuwa ameelimika, ni lazima awe na uwezo wa kuchanganua kati ya sahihi na potofu na kufuata njia ambayo ni sahihi. Hili ni jambo la msingi sana kutilia maanani, tabia za watu wetu. Ili tuunde taifa hili liwe imara; ni muhimu sana kuangalia kwa ukaribu tabia za watu wetu. Tufanye haya ili tujenge tabia ambazo zina faida kwa taifa letu na vijana

wanaofikiri na kutenda sawa sawa; vijana ambao wanawajibika ipasavyo kwa taifa lao na kwa jamii zao; ili kuondoa tabia zenye madhara kwao wenyewe vijana, kwa jamii inayowazunguka, lakini pia kwa taifa. Na kufanya taifa hili kuwa la wazalishaji lakini pia bora. Taifa bora hufanywa na watu bora, hatuwezi kuepuka kujenga watu wetu kuwa bora kama tunataka kujenga taifa bora. Kwasababu ni ukweli usiopingika kwamba taifa lolote linajengwa katika watu. Kwahiyo ni muhimu kuwekeza katika watu. Tabia za watu wetu zinapokuwa bora na ndio taifa linapokuwa bora zaidi.

Ni muhimu kujenga msingi huu, ambao juu yake tunaweza kujenga kitu ambacho kitakuwa imara. Kuliko kufuata mali peke yake na kusahau misingi ambayo huweka watu pamoja kama taifa. Elimu tunayotoa ni muhimu, lakini inahitaji marekebisho makubwa ili iweze kujenga maadili ya watu wetu.

Tukifuata mali tu na tukifundisha kuhusu mali peke yake, tutakuwa tumeruka hatua muhimu na ya msingi katika ukuaji wa taifa lolote; yaani maadili ya watu wetu. Na hatuwezi kuruka hatua hiyo tukawa salama, ni lazima kwanza tujenge maadili ya watu wetu yawe imara na mengine yatafuata. Huu ndio msingi kama tunataka kuendelea ni lazima tujenge msingi huu. Kuanzia kujenga familia imara na mahusiano yake na jamii inayomzunguka, na malezi bora ya watoto wetu.

Tunasahau kwamba misingi hii ya utaifa huanzia chini katika familia, majirani na kuja juu hadi kwenye taifa. Vyote hivi vinategemea mahusiano yake na kila kimojawapo. Taifa linakuwa imara pale familia kwa umoja wake zinapokuwa imara na mahusiano ya watu yanapokuwa bora. Hili linapaswa kujengwa kwenye familia zetu, shuleni na kwenye nyumba za ibada. Ni

lazima lifanyike kote huko kwa juhudi kubwa ili kujenga maadili na nidhamu kwenye taifa letu na ili kujenga taifa makini na lisilo na mizaha.

Taifa linalofanya mzaha kwenye maisha ya kifamilia haliwezi kuendelea, kwakuwa huko ndipo watoto hukuzwa, na mazao yake kuonekana baadae katika ngazi ya utaifa. Na hao huingia katika taasisi zetu, na katika uongozi wa taifa. Kwahiyo tusipoangalia kwa umakini malezi ya watoto wetu, na kujenga maisha yetu ya kifamilia na kijamii kuwa bora tusahau kujenga taifa imara na bora.

Sio lengo langu kutaja tabia mbaya ambazo zina hatarisha taasisi ya familia na kuidhoofisha, nafikiri mnajua, kwasababu wengi wetu tunaishi katika familia. ila nataka kuonyesha umuhimu wa familia katika taifa, ili tuweke mkazo katika kujenga familia zetu, na katika malezi ya watoto wetu. Watoto wetu wakiwa na tabia mbaya baadae ya taifa hili itakuwa hatarini. Kwasababu hao ndio watakaoingia kwenye taasisi za nchi yetu, na kwenye uongozi wa taifa letu, na kulifanya taifa letu kama shamba linalokuza mimea bila kupaliliwa, kwa hakika hakuna tutakachovuna. Mavuno yetu hayatokuwa mengi.

Lakini hao pia ndio watakaokuwa wazazi wa baadae, watakaolea watoto wao bila misingi na maadili, kwakuwa na wao hawakujengwa katika misingi iliyobora na imara, matokeo yake pia watoto wao watakua sio bora pia. Maadili ya nchi yatayumba na nchi itakosa dira. Lakini ukiangalia kwa ukaribu haya yote hutokana na malezi na makuzi duni katika ngazi ya familia. Mavuno yake huonekana katika jamii, na katika ngazi ya taifa. Kwahiyo kama jamii tunapaswa kuwajibika kwa pamoja kama tunataka kujenga nchi iliyo bora na imara. Ujenzi wa taifa sio nguvu ya mtu mmoja bali ni uwajibikaji wa pamoja wa kila raia

kutaka kuona nchi yake ikiendelea. Ni dhahiri kwamba tumeyatupa maisha ya kijamii na kitaifa, ndio maana Taifa letu halina uhai. Ni lazima tulinde maadili yetu ili taifa letu liendelee na watu wetu wawe na furaha.

Taifa huanza kujengwa katika familia, jamii, shuleni na katika taasisi za dini, kama tutashindwa kujenga tabia za watu wetu huko, kuwa bora na zenye manufaa kwa taifa, tusahau kuhusu amani na maendeleo ya taifa hili, na wala utii wa raia kwa sheria na kwa serikali.

Kama wazazi wameshindwa kuwatala watoto wao kuwa watii na wenye nidhamu, serikali haiwezi kufanya kikubwa kwa kutumia nguvu ya jeshi. Kazi ya kujenga taifa sio ya mtu mmoja inahitaji uwajibikaji wa pamoja katika familia na ndani ya jamii. Kwasababu utii unaanzia huko. Taifa huwa bora ikiwa watu wote ambao wameunda taifa, wakitimiza wajibu wao.

Kuna vitu ambavyo tunaviona ambavyo havitupi dira nzuri kwa mweleko wa taifa letu. Ni jambo la kimsingi sana kuvizungumzia. Kama tunataka kuliokoa taifa hili. Sio tu jinsi gani tunavyo watayarisha watu wetu kuingia kwenye uongozi wa nchi yetu, bali pia tunavyowajenga watu wetu kuwa raia bora, na kuwa walezi bora na wasimamizi wa familia zao.

Kizazi chetu kijacho kitategemea sana malezi tunayowapa vijana sasa. Majaliwa yetu yanategemea jinsi gani tunawalea vijana wetu sasa hivi. Ubora wa kizazi kijacho unategemea sana malezi yetu ya sasa. Kama tunataka taifa letu kuwa bora ni muhimu na ni lazima tuanze sasa kujenga kizazi chetu na kuangalia tabia za vijana wetu na malezi ya watoto wetu.

Kama sisi sio bora tusitegemee vizazi vyetu kuwa bora, kwasababu sisi ndio tunaowalea wao, watarithi tabia zetu na wao watakuwa kama sisi, kama hatutafanya mabadiliko sasa ya kitabia, mpaka hapo tutakapofanya mabadiliko ya kina kwenye mioyo yetu na fikra zetu, ndipo nuru kwa kizazi chetu kijacho itakapokuwepo.

Kwahiyo tukitaka kujua baadaye ya taifa letu tutaangalia tabia za vijana wetu kama ni zenye tija kwa wakati ujao. Na mimi sioni kama ni zenye tija; labda tubadilike. Mawazo yangu ni kwamba tunataka kufanya taifa hili liwe kubwa, lakini tabia zetu na mawazo yetu havitupeleki huko. Kwahiyo haina budi tukajifikiria upya. Taifa hili linauwezo sio tu kuwa taifa lenye uchumi wa kati; kitu ambacho hakipaswi kuwa dira yetu; linauwezo wa kuwa taifa kubwa duniani ikiwa tu tutajiangalia kwa ukaribu na kufanya jitihada za kufika huko.

Kwahiyo tunahitaji hekima ya kujua haya mambo. Rais Julius Nyerere aliposema tunahitaji kupambana na ujinga hakumaanisha kuwa na watu ambao wana uwezo wa kutengeneza vitu au kutoa huduma fulani kama udaktari au uhandisi pekee; bali ni kuondokana na tabia zenye madhara kwa jamii, na kumfanya raia wa taifa hili, kuwa mwenye matendo yenye faida na kuwa binadamu bora. Ni kuondokana na matendo yenye uharibifu. Ujinga ni kufanya matendo yasiyo na faida na wala mantiki. Ni kuondoka kwenye njia sahihi. Na mtu bora kwa taifa lake ni yule anayesema ukweli na kutenda yenye tija na faida kwa taifa lake. Mtu anayelinda na kuangalia haki za wengine na kujitoa kwaajili ya maendeleo ya taifa lake bila ubinafsi.

Tunaweza kuwa na madaktari na wahandisi na hata wanasheria, kama hawafanyi yaliyo sahihi, hawawezi kuwa na faida kubwa ambayo tunategemea, Kwahiyo maadili ya watu wetu na nidhamu ni muhimu, kwasababu haya mambo yanawafanya hawa watu kuwa wenye kuzalisha zaidi. Na kufanya taifa letu kuwa bora na endelevu.

Hatuwezi kutenganisha maadili na elimu. Ni muhimu kumfanya raia wa taifa hili kuwa mwenye faida kwa uzalishaji lakini pia kitabia. Kwahiyo tabia za watu wetu lazima zijengwe.

Kama nilivyosema; taifa kuwa na watu wenye fani mbali mbali, ni vyema sana na ni bora. Taifa linawahitaji watu wenye ujuzi na ufanisi katika kazi zao, lakini hatutofikia ufanisi wa hali ya juu kama hatutaangalia tabia pia na nidhamu za watu wetu. Na kama watu wetu hawatojitambua katika utaifa. Na kwamba wanawajibika kutumikia taifa lao kwa dhati na wanawajibika pia kujenga tabia zao kuwa zenye faida kwa taifa na kuwa wazalendo.

Ili tuendelee nakubali tunahitaji watu wa fani mbalimbali, lakini pia lazima tuumbe tabia zao kwenye utu wema. Elimu ambayo badala ya kujenga watu wema wengi inaongeza waovu haina faida.

Ingawaje mtu anaweza kujiita ameelimika kwasababu tu ana shahada au shahada ya uzamivu, lakini kwa matendo yake mwenyewe anaweza kuwa mjinga kwa tabia, na watu wakamdharau. Lazima tuangalie tabia pia ya mtu ambaye ameenda shule je ni mkweli? muwazi ?

Kwa mtu ambaye hajaenda hata chuo kikuu, atajifunzaje kutoka kwa wasomi hao, akiona tabia zao ambazo kimantiki ni tabia za mtu asiyefikiri sawa

sawa?. Kutokana na elimu yako tunategemea wewe kutenda kwa ufasaha tofauti na mtu ambaye hakwenda shule, kwasababu ufahamu wako umetanuliwa. Tunatumaini utakuwa unajua kati ya potofu na sahihi na jukumu lako ni kutenda yaliyosahihi.

Tunategemea wewe uwe mfano kwa watu wengine kwa maneno na matendo. Kama elimu yetu haitakuwa na uwezo wa kumtengeneza mtu bora na mwenye faida kwa taifa, haina maana. Na mtu bora ni mwenye maadili na nidhamu. Mtu ambaye huongea ukweli daima na kuitumia elimu yake kwa faida ya umma. Na sio mtu mwenye choyo na mbinafsi anayeweza kuiuza jamii yake kwa ubinafsi na ulafi.

Swali jingine la muhimu ambalo linaweza kuwa mwongozo ni kujua kwanini tunaelimisha watu wetu. Tusipojua hili tutakuwa tunajiendea tu. Ni lazima tuwe na mipango. Kukuza ufahamu wa watu wetu na maadili yao, kuwafanya watu wetu kujua wajibu wao kwa taifa lao na kwa jamii inayowazunguka, na kuwapa maarifa ya kazi ili taifa letu tulikuze kiuchumi. Kwa ujumla ni kujenga raia bora na mwenye faida kwa taifa. Na kufanya mapinduzi katika taifa. Hili liwe dhumuni la kuelimisha watu.

Kwahiyo matendo kama ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma hayapaswi kuwa miongoni mwa matendo ya mtu aliyeelimika. Mtu aliyeelimika anapaswa kuwa mtu mkweli, mwaminifu na mwenye kufikiri na kutenda kutokana na fikra sahihi. Matendo haya ya rushwa hulirudisha taifa nyuma badala ya kulipeleka mbele. Na hilo sio lengo la elimu tunayotoa kwa watu wetu. Lengo la taifa kusomesha watu wake ni ili wafanye mapinduzi na kuleta maendeleo kwenye taifa lao wenyewe. Na kuumba tabia zao kuwa binadamu bora na wenye maadili.

Watu wetu lazima wajue wajibu wao na haki zao za msingi. Lazima wafikie uelewa huu, na wajibu wao wautimize kwa nguvu zote, na haki zao zitimizwe na serikali husika. Ili tuendelee, watu wetu lazima wajitambue. Pasipo kujitambua hakuna tutakachojenga. Kama watu wasipojua wajibu wao na haki zao hatutaweza kujenga taifa hili vyema.

Raia lazima waone wanalimiliki taifa hili na ni wajibu wao kuliangalia, kulilinda, kulijenga na kuliendeleza. Tunachohitaji katika taifa letu ni kukuza kujitambua kwa watu wetu kwa taifa lao. Ili wajue wao ni kina nani na wana malengo gani ya kuwa pamoja. Ni lazima iwepo dira. Kama watu wetu wasipojua hili ni taifa lao kwa pamoja wanalimiliki na majaliwa ya taifa lao yako mikononi mwao hatutafika.

Kwahiyo elimu yetu lazima ifundishe watu wetu kufikiri na kutenda katika usahihi. Lazima ikuze ufahamu wa watu wetu na sio kumwingizia maarifa mtu kama unavyojaza maji kwenye chupa na kufunga.

Elimu ya namna hii haina faida kama haikuzi uwezo wa kufikiri wa mtu na kumfanya kufikiri mwenyewe na kujiuliza kila kitu kinachokuja mbele yake ili kupata majibu sahihi. Elimu yetu lazima imfanye mtu ajitegemee kifikra.

Hapo ndipo mapinduzi ya kweli yatakapopatikana katika taifa hili. Elimu itakayo mfanya mtu kutafuta majibu ya changamoto zinazotukabili kama taifa na kutoa majibu ya changamoto hizo. Sio elimu ya kutafuta mkate; yaani elimu tumbo.

Hata mbwa anaweza kufundishwa na akatenda kulingana na alivyofundishwa, lakini upeo wake haumwezeshi yeye kugundua na kufikiri na kupata

maarifa yake mwenyewe. Upeo wake wa kiakili una kiwango chake. Lakini binadamu ni muhimu kujiendeleza mwenyewe kiakili na kukuza nguvu zake za kiakili na sio kulishwa maarifa, anatakiwa afikie kiwango cha kujitegemea kifikra na kuamua mustakabali wake na kuwa na maoni yake mwenyewe na mtizamo wake wa jinsi anavyoona mambo.

Tunasoma sio kwamba tunapenda maarifa bali tunataka tupate mkate na vyeo. Ni lazima tubadilike. Hatuwezi kutatua matatizo ya nchi hii tukiwa na fikra za jinsi hiyo. Kwa miaka mingi tumekuwa watu wenye fikra za jinsi hiyo na tumeziambukiza kwa kizazi kingine. Watu wanaenda kusoma ili kutafuta mkate na sio kutafuta maarifa ambayo yatatusaidia ili kuongoza maisha yetu na kutatua changamoto zinazotukabili kama taifa. Kwa fikra za namna hii elimu yetu haiwezi kuwa na faida.

Kama tutatafuta kweli maarifa kwa nia ya kutatua changamoto zinazotukabili kwanini tusifanikiwe? Matokeo ya fikra za namna hii ni maelfu ya wahitimu vyuo vikuu kukaa na kusubiri ajira serikalini. Hawawezi kujitegemea wenyewe, na kuanzisha vyanzo vyao vya mapato kwasababu akili zao haziko huru. Na lakini pia hawajajengwa kutumikia nchi bali maslahi yao binafsi.

Kwasababu akili zao zimejengeka hivyo, wanasoma kusudi wapate ajira sio wapate elimu itakayowafanya wajitegemee; ili wawe na faida kwa taifa, na kujenga mienendo yao kuwa bora. Kwa wao kuwa mtaani ni matumizi mabaya ya rasilimali. Pesa nyingi zimewasomesha ambazo zingetumika maeneo mengine ili kuendeleza taifa letu.

Tunategemea kwamba wangekuwepo sasa hivi wanazalisha mali, kwa kuanzisha miradi mbali mbali

kutokana na ubunifu. Kama elimu yetu haiwafanyi wahitimu kuwa hivyo ina matatizo. Kama tunawapa watu elimu lakini haiwafanyi kujitegemea kuna tatizo hapo. Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu kila siku wanaongezeka mtaani bila ajira ni ishara kwamba kuna tatizo hapo.

Kwahiyo mwelekeo wangu ndio huo. Ili tujenge taifa imara ni muhimu kuangalia kwa umakini tabia za watu wetu. Na hili ni muhimu tukalianza kwenye malezi tunayotoa katika familia zetu na kwenye taasisi zetu za elimu. Tunavyowaelimisha watu ili kujenga tabia zao na mienendo ni jambo muhimu sana kwa baadae ya taifa.

Bila ya hivyo itakuwa vigumu sana taifa hili kuendelea na kushindana au kuyakaribia mataifa makubwa ambayo yalianza kujengeka muda mrefu kwa kuangalia maadili na nidhamu za watu wao. Na kuwajenga watu wao kujitegemea wangali wadogo. Waliwajenga watu wao kutofuata mambo ya kijinga na kuwajengea tabia ya kufanya kazi kwa kuwa na nidhamu ya kazi na maadili.

Kwahiyo juhudi, nidhamu na maadili ni jambo la muhimu kwetu. Tabia ya kupenda kazi huanza kujengwa wakati watoto wadogo. Tunaweza kujenga tabia bora na zenye faida kwa taifa watoto wetu wakiwa wangali wadogo. Na kuwajengea uzalendo wao kwa taifa.

Tukizungumzia umoja wa nchi na mambo mengine, kama tukiangalia kwa ukaribu, yanaanzia kwenye maadili yetu. Tukiisha kengeuka, mambo mengine mengi yanaharibika. Hata kuangalia haki za wengine na kuziheshimu kunakuwa hakupo tena. Na taifa letu halitoweza kusimama kama tusiposimamia misingi ya

haki na usawa kwa wote. Kwasababu haki ndio huweka watu pamoja.

Nidhamu yetu ni ya msingi sana. Nidhamu ni kujizuia hata kama kuna msukumo ambao unakusukuma kutenda jambo ambalo ni lenye faida kwako binafsi, lakini ni lenye hasara kwa jamii ambayo baada ya muda fulani linaweza kuleta uharibifu. Kuleta uharibifu katika jamii kwa faida binafsi ni jambo lisilokubalika. Kujizuia kwetu na kutenda kwa kutumia fikra badala ya matamanio ni jambo lenye faida kwetu.

Kwa mwenye hekima maisha ni fumbo ambalo linapaswa kufumbuliwa. Na dunia ni chuo ambacho binadamu anapaswa kujifunza kila siku. Kwakuwa tumezaliwa ili tujifunze na ili tukue. Wajibu ambao ni wa kipekee tumepewa na Mungu ni kujifunza.

Tusipojifunza tutarudia makosa yale yale. Kwahiyo tunahitajika kujifunza kila wakati ili kuepukana na madhara ambayo yanapatikana kama hatujifunzi. Dunia tunayoiona ni kama kitabu kikubwa ambacho kila siku lazima tukisome, hadi siku tunapoingia kaburini. Kushindwa kujifunza ni kukaribisha majanga kwenye maisha yetu. Ni lazima tujifunze. Ni lazima tuwe na hekima. Na hekima na busara vikituongoza katika maisha yetu, matatizo mengi tutayaepuka.

Binadamu tu wajinga ndio maana tunawajibika kujifunza kila siku. Kama tungekuwa werevu na wenye akili tusingehangaika kujifunza ili tupate maarifa ambayo yatatuongoza maisha yetu ya kila siku. Tumezaliwa wajinga bila maarifa ndio maana tunayahitaji; na ni wajibu wetu wa kimsingi kuyatafuta. Tunahitaji maarifa ili tuyaongoze maisha yetu na ili tuendelee kama taifa. Bila ya kuwa na

maarifa ya kutosha kamwe hatutaweza kuendelea. Taifa hukua pale watu wake wanapokua kimaarifa na busara. Bila ya hivyo hatuwezi kuendelea.

Na kila wakati tunaanguka katika makosa na kujikuta kwenye madhara. Lakini ni wajibu wetu tunapoanguka kwenye makosa kunyanyuka na kutorudia makosa tuliyofanya. Hatukuumbwa tuishi pekee. Bali tuliumbwa ili tujifunze na ili tukue.

Binadamu katika maisha yetu yote kutokea utoto wetu hadi uzee wetu tunawajibika kujifunza pasipo kuchoka. Tena binadamu hakuumbwa kwa mfano wa mti katika ukuaji wake. Bali akili yake inapaswa ikue na tabia yake ijengwe. Na aweze kuwa na nguvu ya kuchagua jema na baya. Aondokane na ujinga. Na afuate njia iliyo sahihi. Kwakuwa ni katika njia iliyosahihi ndio kwenye misingi iliyo imara. Kwahiyo ni wajibu wetu kutafuta maarifa kadiri ya uwezo wetu. Ujinga ni udhaifu. Mataifa dhaifu ni mataifa yasiyo na maarifa.

Tunakamata samaki kwasababu tuna uelewa mpana zaidi yao. Vile vile kuku na mbuzi, kwasababu uwezo wetu wa akili mkubwa kuliko wao; ndio maana tunawatawala. Na binadamu na mataifa wanatofautiana katika uelewa, pia katika utumiaji wa akili zao kukuza na kutafuta maarifa. Mataifa yenye uwezo mkubwa wa kufikiri watayatawala mataifa yenye uwezo mdogo. Wana nguvu ya kuvumbua vitu na silaha za kutawala. Watu wasiotafuta maarifa na kuwekeza katika mambo ya kijinga watatawaliwa.

Hakuna taifa ambalo litaweza kutawala mataifa mengine pasipo nguvu ya kugundua. Kwahiyo kama taifa tunawajibika kuwekeza katika sayansi. Uhuru wetu unategemea uwezo wetu wa kugundua au kuendeleza silaha zilizopo kwaajili ya ulinzi wetu.

Ili tuendelee lazima tugundue, ni lazima tutengeneze. Binadamu hawezi kuendelea pasipo kugundua. Mataifa yaliyoendelea ni mataifa yaliyokuwa na uwezo wa kugundua. Uwezo huu wa kugundua upo ndani ya binadamu yeyote yule ilimradi anaitwa binadamu. Tofauti iliyopo ni matumizi ya akili zetu.

Ni wapi tumeelekeza akili zetu. Hapo ndipo ilipo tofauti kati ya binadamu mmoja na binadamu mwingine, na taifa moja na taifa jingine. Ni matumizi ya akili zetu.

Maendeleo ni mwelekeo na dira ya mawazo ya watu, na viongozi wao. Mawazo yetu lazima yakusanywe na yaongozwe katika mkondo unaofaa, ambao ni wenye faida kwa taifa letu. Vitu tunavyosoma na kuona kwenye runinga zetu, na magazeti yetu, na radio zetu vinachangia sana kuumba akili zetu.

Kwahiyo inategemea sana watu wetu wanalishwa nini kuanzia nyumbani, shuleni na kwenye vyombo vyetu vya habari. Kama watu wetu wanalishwa ujinga ni vigumu sana kuwa werevu. Watapenya watu wachache mno wanaopenda kujisomea na kutafuta maarifa.

Tunajiuliza kwanini tuna kila kitu lakini sisi kama nchi bado ni maskini? Tatizo haliko popote; tatizo liko kwenye akili zetu na mambo gani tunayapa kipaumbele katika maisha yetu. Inahitaji akili kutengeneza mitambo ya kuchimba gesi; inahitaji akili kutengeneza mitambo ya kuchimba dhahabu. Inahitaji akili kutengeneza mfumo mzuri wa utalii.

Lakini sio tu akili peke yake na nidhamu ya utendaji kazi. Ambayo pia nidhamu hii hutokana na akili na watu wa taifa husika kujua wanahitaji nini, na

kuwekeza akili zao na mawazo yao huko. Watu wetu watakapojitambua wanahitaji nini, kama taifa itakuwa ni kazi rahisi kwetu kuendelea.

Tunapungukiwa akili ndio maana tunashindwa kuendelea. Lakini sio kwamba hatuna akili; bali hatuzitumii ipasavyo. Na pengine hatuna kipaumbele katika mambo ya msingi ambayo yatafanya taifa letu kusonga mbele na mambo ya msingi ambayo yanahusu maisha yetu ya kila siku.

Hatuwezi kupinga hili, kwasababu watu ambao wameendelea ni watu ambao wana maarifa ya kutosha kwenye hifadhi yao. Ambao wameweza kupitia sayansi na teknologia kutawala mazingira yao.

Lakini tuna uvivu wa kufikiri; hatufikiri tunasubiri kuletewa kila kitu. Tunangoja watu wengine wafikiri kisha watuletee maarifa. Wagundue silaha watuletee. Wagundue kompyuta na magari watuletee. Hatufikiri kuanzisha vitu vyetu wenyewe. Ukienda kwenye maktaba yoyote kubwa vitabu vingi hatujaandika sisi. Maarifa mengi yaliyomo kwenye vitabu hivyo siyo yetu. Wao wako juu zaidi yetu sababu ya maarifa sio kitu kingine. Hadi wanaandika mambo mengine yanayotuhusu sisi wenyewe katika mazingira yetu tuliyoishi na kukua.

Watu wachache sana ndio wamejaribu kuandika na kutaka kusaidia watu maarifa waliyonayo. Tumekuwa wategemezi hata kwa mawazo tu, achilia mbali misaada ya wahisani. Aina hii ya mtizamo katika akili zetu lazima tuifute. Si zungumzi haya ya kwamba mimi ni mzuri sana au niko tofauti na wengine.

Mimi ni Mtanzania yule yule kama wengine; lakini anayehitaji mabadiliko. Mimi ni zao la mazingira yanayonizunguka. Akili zangu na mtazamo wangu

hapo mwanzo zilikuwa zimefungwa na mazingira. Ili tuendelee lazima tuwe juu ya mazingira.

Ni kweli kwamba watu ni lazima wafanye kazi ili taifa letu liendelee, sio; wafanye kazi tu bali wafanye kazi kwa maarifa. Kwasababu pasipo kufanya kazi kwa maarifa na kutegemea nguvu tu hatutakuwa na tija ya kutosha. Hakuna njia yoyote ile nyingine kwa taifa letu kuendelea pasipo watu wetu kujishughulisha katika uzalishaji mali. Hatuna njia nyingine ya kuepuka kama tunataka taifa hili liendelee zaidi ya kufanya kazi kwa bidii na kwa maarifa.

Kwahiyo inategemea sana mwelekeo wa mawazo yetu tumeuweka wapi kama taifa, na tuko makini kiasi gani katika kutaka kuleta maendeleo kwenye taifa letu. Kama tutakuwa ni watu wa mzaha, katika kila kitu cha msingi ambacho kinahusu maendeleo yetu hatuwezi kufika. Mzaha kwenye mambo ya msingi hauwezi kutufikisha popote. Ni lazima tutilie maanani mambo ya msingi yanayohusu maendeleo ya nchi yetu. Na elimu ya watu wetu ni jambo moja wapo. Baadaye yetu kama taifa inategemea kwa kiasi kikubwa ni kiasi gani tumewaelimisha watu wetu, ili wawe na ufahamu wa kutosha kuhusu taifa lao, maadili, nidhamu na ufanisi katika utendaji kazi.

Kwahiyo ni muhimu tutambue na kuelewa kama alivyo binadamu kwasababu ya uelewa wake na maarifa yake, amekuwa na mamlaka ya kutawala viumbe vingine; ndivyo hivyo hivyo mataifa ambayo yana uelewa mkubwa na maarifa, ndivyo walivyokuwa na nguvu ya kutawala mataifa yasiyokuwa na akili sawa sawa.

Ili tuondoke kutoka huko ni muhimu kutafuta maarifa na kukuza ufahamu wetu. Lakini la msingi kuliko yote na la muhimu ni kujenga nidhamu na maadili yetu.

Taifa lisilo na nidhamu ni taifa lisilo na dira na mwekekeo na halitaweza kufanikiwa.

Kama tunataka kuendelea ni lazima tujifunze kufikiri, na sio kujifanya tunajua wakati ufahamu wetu bado ni mdogo. Ni lazima tutaabike kama walivyotaabika mataifa mengine kama tunataka kunyanyuka kama taifa. Ni lazima tutafute maarifa kwa juhudi zote.

SURA YA 2

SIASA

Siasa ni nyenzo ya kujenga na kuendeleza nchi, msingi wake ni hoja, mawazo na fikra yakinifu. Siasa si ulaghai kama inavyosadikika, au kama inavyotumika kwa sasa na wanasiasa wenye uchu na ulafi. Siasa ni ujenzi wa jamii. Siasa inahitaji akili iliyopevuka. Inahitaji kuona hatua nyingi mbali bila kiona mbali; bali kwa kutumia akili na uwezo wa ubongo kufikiri.

Kwa kutumia siasa tunajenga misingi ambayo kizazi kijacho kinakuja kunyanyua matofali. Mifumo yote ya

kijamii ni siasa ambayo inasaidia kujenga. Kwahiyo inategemea sana nchi yetu ina wanasiasa wa namna gani. Ubora wa nchi yetu utategemea wanasiasa tulio nao, na jinsi gani wamepevuka kuchukua majukumu ya kijamii. Inategemea sana fikra zao, mitazamo yao na maadili yao. Baadaye yetu kama taifa itategemea sana siasa zetu zikoje.

Kwahiyo kama tuna siasa nzuri ni wazi kwamba tutaendelea mapema zaidi kuliko tukiwa na siasa mbaya. Tutajenga jamii zetu na mifumo ya kijamii vyema zaidi kama tuna siasa nzuri kuliko kama tukiwa na siasa mbaya. Tutakuwa na amani zaidi tukiwa na siasa nzuri kuliko tukiwa na siasa mbaya. Umoja na mshikamo utaboreka zaidi tukiwa na siasa nzuri kuliko tukiwa na siasa mbaya.

Kila kitu tunachokifanya kinategemea siasa. Na hata maendeleo yetu binafsi na ya taifa yanategemea ubora wa siasa zetu. Kwahiyo hatuna budi kujenga siasa bora. Na siasa bora haziwezi kujengeka kama hatuna viongozi bora. Viongozi wenye hekima, busara na maono ya mbali. Kwahiyo ili tuwe na siasa bora lazima tuwe na viongozi bora. Kwahiyo aina ya siasa inayofanyika hutegemea sana aina ya viongozi nchi iliyonao. Na maendeleo yetu kwa hakika hutegemea siasa nchi inazofanya.

Kwahiyo ni muhimu kuzingatia hili. Mwelekeo na dira ya taifa letu itategemea sana aina ya siasa tulizonazo . Na aina ya siasa hutegemea pia aina ya viongozi tulionao. Misingi ya taifa hili itakuwa imara ikiwa tu siasa zetu zitakuwa imara.

Ni wajibu wa mwanasiasa au kiongozi kujenga na sio kubomoa. Lakini tuna tatizo katika hili; kwenye siasa zetu badala ya kusaidia watu kuwaweka pamoja, tunagawanya. Na misingi ya malengo yetu kuingia

madarakani sio maendeleo ya nchi, lakini ni maslahi binafsi. Siasa zetu zimejengwa hivyo, na kama tunataka kutoka huko kama taifa, ili kuwa na dira haina budi kubadilika.

Tunayoyaongea kwenye majukwaa ya siasa yana athari kubwa, yawe hasi au chanya. Kwa kiongozi na mwanasiasa aliyepevuka, anatakiwa kuwa makini kwa anayoyaongea. Kwasababu hutupaswi kuwagawa watu, kwa maneno yetu, ili kufikia malengo ya kibinafsi ya kupata madaraka, lakini kama viongozi; tunapaswa kuleta watu pamoja, kwa maneno na matendo yetu. Na tunapaswa kujadiliana kwa hoja na huo ndio unaotakiwa kuwa msingi na muongozo wetu. Tukishindwa kuelekeza akili zetu vyema, na kuishia kuwagawa raia wa nchi yetu, kwa misingi ya kisiasa au misingi yeyote ile hatutafikia malengo yetu ya kujenga taifa bora na imara.

Naamini kazi ya siasa ni kutoa suluhisho la matatizo yaliyopo katika jamii; na siyo kuonyesha tu, kila mtu anaweza kuonyesha tatizo. Lakini si kutoa suluhisho la tatizo. Sio kila mtu anaweza kuonyesha watu njia ambayo yatupasa kupita. Tunapofikiria kuhusu mambo yote haya; tunapaswa kujua na kuchukulia kwa umakini mkubwa, suala la uongozi wa nchi yetu. Na kuzingatia ni watu gani ambao wanaingia katika uongozi wa nchi yetu, na kushika nafasi za maamuzi, kwasababu baadae yetu kama taifa itategemea aina ya viongozi tulionao na maamuzi wanayoyafanya. Hili ni jambo la kimsingi na muhimu.

Kazi ya siasa au uongozi ni kuwaleta watu pamoja; siyo kuwagawanya. Kuwaleta watu pamoja ili wawe na malengo ya pamoja yaliyowaunganisha. Hiyo ndio kazi ya siasa. Na wala sio ubinafsi na kuangalia maslahi binafsi. Kama tukiangalia hivyo na mawazo yetu tukiyaelekeza huko tutalivuruga hili taifa.

Kuna huu mtizamo ambao upo miongoni mwa wanasiasa wengi wa kudhani kwamba kwenye siasa ni sehemu ya kuchuma. Ni mtizamo mbaya sana kwa majaliwa ya taifa letu. Wanasiasa wakiwa na mtizamo wa namna hiyo hawataacha kuwakandamiza raia. Hawataweza kusimamia haki. Ili kiongozi aweze kusimamia haki nia yake na dhamira yake ni lazima iwe kuongoza watu na ujira uwe baadaye. Huwezi kuongoza bila kukandamiza watu kama umeingia kwenye uongozi sababu ya uchu wa mali.

Ili viongozi wetu waweze kusimamia haki katika nchi hii ni lazima na ni muhimu kubadilisha mitizamo yao kuhusu mali na uongozi. Ni lazima wawepo pale sio kuchuma, bali kuongoza na kusimamia haki. Madhara ya kuwa na viongozi ambao wameingia kwenye uongozi kutafuta mali ni kutengeneza raia wanaojali mali kuliko utu. Na itakapofikia hapo taifa sio moja tena. Kila mtu atajali maslahi yake peke yake. Na migawanyiko ndani ya jamii itaongezeka sana.

Na mitafaruku ya ndani ya nchi ya kisiasa na kijamii itaongezeka. Kwasababu kila mtu atakuwa anaangalia maslahi yake binafsi, na maslahi ya makundi, badala ya maslahi mapana ya taifa na umoja wetu. Na hii sio nzuri kwa taifa letu. Hatuhitaji mitafaruku isiyo na msingi ya mara kwa mara katika taifa letu.

Ili tuendelee tunapaswa kujitambua na viongozi wetu wanapaswa kujitambua kwanza, kwasababu kiongozi hawezi kuongoza watu pasipo yeye kujitambua, na kujua kazi ya uongozi sio kazi ya mzaha sio kazi ya mchezo mchezo ni kazi ambayo inahusu maisha ya watu na majaliwa ya baadaye ya taifa hili.

Kuna watu wengi wanataka kuingia kwenye uongozi ni lazima wajipime na wajue sio kazi rahisi. Na

inatupasa tuombe kila siku ili tupate viongozi wenye hekima na busara.

KAZI YA MIKONO YETU

Kazi ya Mungu ni ya kiwango cha juu zaidi ya kazi ya mikono ya binadamu. Ushahidi huu uko dhahiri machoni kwetu. Angalia angani na uniambie. Angalia pia ardhi.
Pengine tunaweza kusema kazi zetu sisi ni bora zaidi. Lakini hata zile kazi tunazoziita zetu sio zetu. Kwasababu Mungu ndiye aliyetuumba akatupa akili, macho, miguu na mikono ya kufanyia kazi.

Miguu kutusaidia kutoka sehemu moja kwenda nyingine, na macho kutuongoza tunakoelekea. Midomo kuwasiliana na masikio kusikilizana. Tunaposhindwa kusikilizana wakati tuna masikio yaliyo na afya na midomo inayoongea lugha moja tatizo ni nini? Sio ubinafsi wetu? Tunatakiwa tuwe na usemi mmoja na dira moja. Bila ya hivyo hatuwezi kuendelea.

Kama hatuwasiliani vyema, na kusikilizana vyema, tuna matatizo makubwa. Tukiwasiliana vyema na kusikilizana maisha yanakuwa mepesi zaidi. Na maendeleo yetu yatakuja kwa haraka zaidi. Kwasababu tutakuwa wamoja katika mawazo na matendo.

Ubinafsi wetu ndio unaotutenga miongoni mwetu. Hila na hadaa ndizo zinazotufanya tusiendelee. Tunatakiwa tusiwe na hila wala hadaa, bali kuwa watu ambao wanaongea ukweli. Hatuna budi kuutafuta ukweli na kuongea ukweli kila wakati.

Kutumia hila au hadaa kufikia malengo ni mbinu za watu dhaifu. Kujenga himaya kwa hila na hadaa ni mbinu za watu dhaifu. Bali wajibu wa mtu mwenye busara, hekima na nguvu ni kusimamia haki. Mikono, miguu, macho, masikio na mdomo, ni nyezo ambazo tumepewa ili tujenge dunia yetu. Kuna nguvu isiyoonekana katika hili. Nayo ni nguvu ya mawazo katika kuumba. Vitu vyote tunavyoviona kwa macho yetu ambavyo sio vya asili, ni zao la mawazo. Mwanzoni havikuwepo vimeumbwa na binadamu kutokana na nguvu aliyopewa na Mungu ya kuwaza na kugundua.

Kazi yoyote njema na nzuri hutoka kwa Mungu. Huwezi kufananisha kazi ya mikono ya binadamu na ile ya Mungu katika ubora na ufanisi.

Kuna falme mbili zinazopingana; ufalme wa nuru na ufalme wa giza. Na falme zote hizo hujengwa na mawazo yetu na mikono yetu. Pale binadamu wanapoenda kinyume na njia iliyo sahihi na njema, wanajenga ufalme wa giza na nuru hutoweka miongoni mwao.

Matendo mema humuita Mungu na matendo maovu humuita shetani kujenga ufalme wake. Ni muhimu kwetu tukatafakari ni njia gani tunapaswa kupita. Je tumfuate Mungu ama shetani? Matendo yetu ndiyo yatakayotuweka moja ya sehemu hizo mbili.

Kwa kutenda kwetu mema tunakuwa wema na kwa kutenda kwetu maovu tunakuwa waovu, na hivyo kuwa mbali na Mungu aliyetuumba. Hakuna njia nyingine yeyote ya kupata amani kama tutatenda maovu.

Mungu atapata faida gani kwa kutenda kwetu mema au maovu? Kutenda kwetu mema au maovu ni kwa

faida yetu au hasara yetu. Uovu wetu haumgusi Mungu, bali sisi wenyewe wenye nyama na damu. Lakini ukweli ni kwamba hataki tuangamie au tupotee. Anataka tuwe na amani na furaha. Bali matendo yetu ndiyo yaliyofanya dunia tuliyonayo sasa. Dunia tuliyonayo ni zao la matendo yetu na fikra zetu. Iwe dunia tuliyonayo ni mbaya au nzuri.

Kwahiyo kazi ya mikono yetu ndio itakayotengeneza baadaye yetu kuwa nzuri ama mbaya. Kwa mawazo yetu na fikra zetu tunazaa matendo yetu. Na tumetengeneza taifa tulilonalo kwa mazao ya fikra na matendo yetu. Taifa letu litakuwa bora zaidi kama tukibadili fikra zetu na mwelekeo wa matendo yetu.

Kwahiyo, taifa letu linatutegemea sisi kulijenga. Uzuri wake au ubaya wake unatutegemea sisi. Ni sisi ambao tunaweza kufanya taifa hili kuwa sehemu nzuri ya kuishi ama mbaya. Hekima zetu na busara zetu ndizo zitakazojenga taifa hili. Na kama tutapungukiwa hekima na busara, kwenye taifa hili hapatokuwa sehemu nzuri ya kuishi.

Tuchotakiwa kujua kama tunataka kujenga taifa hili pawe mahala pazuri pa kuishi kwanza tujenge mahusiano yetu. Hili ni jambo la msingi sana. Ni lazima tujenge kuheshimiana na kuthamini utu wa mtu. Ni lazima pia tupendane kama watu wa taifa moja.

Wale ambao wako kwenye madaraka ya kutawala watu, ni lazima watumie madaraka yao kwa busara. Nguvu waliyopewa ambayo iko mikononi mwao ikitumiwa vibaya huleta uharibifu. Wanatakiwa kutafuta busara ili iwaongoze katika maamuzi yao. Nguvu waliyopewa ina pande mbili; ikitumiwa vibaya inaweza kuwarudia wenyewe.

Kwahiyo wasitumie madaraka yao kuonea wengine na kutenda yasiyo na haki. Waangalie maskini na wasiojiweza, watawale kwa haki na wajue kuna aliye juu yetu wote, yeye aliyetuumba, ambaye ndiye mtawala wetu wote. Yeye ambaye uhukumu kulingana na matendo yetu na asiye na upendeleo. Lazima wajue kila mtu ni zao la matendo yake na tutavuna tunachopanda.

Kwahiyo matumzi ya madaraka vyema ni mazuri kwa faida ya nchi. Nchi huendelea pale viongozi wake watakapotumia vyema madaraka waliyonayo kwa busara na hekima. Kinyume chake nchi ni ngumu kuendelea. Kwahiyo viongozi wana wajibika kutumia hekima na kufikiri vyema kabla ya kufanya maamuzi na hata kuongea. Taifa ambalo linatawaliwa vyema lina amani ya kweli na sio amani itokanayo na hofu bali itokayo moyoni.

Viongozi bora sio wepesi wa kutumia nguvu badala ya hekima; Wale wenye nguvu na mamlaka ya kweli sio wepesi wa kutumia nguvu kwa raia wao, Wanatumia nguvu waliyonayo kwa busara na kuongozwa na hekima katika maamuzi yao. Kiongozi anayependa kutumia nguvu ovyo hana maarifa ya kutosha.

Kiongozi wa namna hii mwisho wa siku atashindwa kuongoza watu. Huwezi kuongoza watu kwa kuwatia uwoga na hofu. Utii haupatikani kwa kutumia nguvu peke yake. Lakini hekima inaweza kukufanya watu wakakutii na kukuheshimu. Na kazi ya uongozi ni kuongoza watu njia ambayo wanapaswa kupita. Kwahiyo kiongozi ni lazima ajue wema maana yake nini. Yeye ambaye hawezi kujiongoza mwenyewe katika mambo sahihi na ya kweli hawezi kuongozi wengine. Atapeleka taifa lote shimoni. Na siyo kwenye mwanga ambao tunauhitaji.

Katika jamii huru na nchi huru watu wana uhuru wa kutoa maoni na uhuru huu unalindwa. Wana haki ya kuongea jinsi wanavyoongozwa na kuelezea matumaini yao na matarajio yao kwa serikali yao. Kama matarajio yao hayakutimizwa wana haki ya kuongea.

Ni jamii ambazo haziko huru pekee, uhuru huu unakuwa haupo. Lakini kutokuwa huru kunatokana na jamii yenyewe kutokujitambua, hivyo kushindwa kudai haki zake za kimsingi kwa serikali na pengine kuona serikali inawafanyia fadhila tu mambo yale ambayo kimsingi ni haki yao. Hivyo jamii hii inakuwa haiko huru kifikra kutokana na kutokujitambua kwake. Kwasababu ya raia kutokuwa na elimu ya kutosha ya uraia na kutolipenda taifa lao kwa dhati. Na kushindwa kudai au kuongea pale haki zao za kimsingi zinapokiukwa.

Kutokuwepo kwa ufahamu huu wa utaifa ni chanzo chao cha kutokuwa huru. Kujitambua wao ni kina nani na wana haki gani katika taifa lao.

Kujitambua kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu uraia na wajibu wao, pamoja na nafasi yao katika kujenga jamii zao na taifa lao. Kwa jamii inayojitambua inahitaji nini na mwelekeo wao ni upi kuwanyima uhuru huu ni kazi sana. Mara nyingi uhuru wa kuongea na kutoa maoni huminywa kwa jamii ambazo hazijitambui.

Ni vigumu kwa jamii zilizoendelea na kujitambua kuminya uhuru huu. Lakini ili taifa hili lipate uhuru huu kwa ukamilifu halina budi kuupigania na kuufahamisha umma kuhusu haki zao na wajibu wao kwa taifa. Watakapokuwa na ufahamu wa kutosha uhuru huu hawataweza kupokonywa tena.

Ni serikali pekee za kikandamizaji ndizo ambazo zinanyima uhuru watu wake wa kutoa maoni, wa kuongea na kuandika, lakini wanafanya ukandamizaji huu kwa watu wasiojitambua kwasababu ni vigumu kukandamiza jamii za watu wanaojitambua. Kwasababu wanajua umuhimu wa uhuru huu na mahusiano yao. Pamoja ya kwamba tumepata uhuru kutoka katika wakoloni hatuko huru bado.

Bado tuna tabia zile zile za kikoloni ambazo zimezama kwa viongozi wetu. Badala ya kuelimisha watu wetu kujua haki zao na wajibu wao ili kujenga jamii bora tunatumia nafasi hiyo ya kutokujua haki zao kuwakandamiza. Kwahiyo ukombozi bado haujapatikana ikiwa bado watu wetu hawajakombolewa kifikra. Ikiwa bado hatujajenga jamii ambazo zinaangaliana kama watu wa taifa moja na wenye majukumu ya pamoja na dira moja. Ikiwa tunaangaliana kwa ubinafsi hatutaweza kujenga jamii bora.

Vitu vyote elimu ya watoto wetu, maendeleo ya jamii zetu na afya za watu wetu vinategemea sana mashirikiano yetu na umoja wetu.

Jamii inayokandamiza haki hizi ni jamii itakayodumaa. Uhuru huu lazima uwepo mashuleni na vyuoni na kwenye vyombo vya habari watu wajadili na kutafakari mambo mbali mbali na changamoto zinazokabili taifa lao na namna gani ya kuzitatua. Kwa fikra na sio hisia. Ni lazima tuwajengee uwezo wa kifikra watu wetu. Kwasababu watu wetu wasipokua kifikra uendeshaji wa nchi hii utakuwa mgumu.

Wajibu wetu wa kimsingi na wa viongozi wetu ni kufanya taifa hili kuwa sehemu nzuri ya kuishi ambapo kila mtu ataheshimiwa mchango wake pamoja na maoni yake yatathaminiwa. Lakini

hatuwezi kufikia hapa pasipokuwa na elimu nzuri na pasipo watu wetu kujitambua. Ni lazima tufanye taifa hili kuwa sehemu ya kufariji na hatutaweza kufanikiwa hili bila kujenga mahusiano yetu.

Raia yeyote katika nchi yeyote akiogopa au wakiogopa kutoa maoni yao au pengine kuiogopa serikali yao ni hatua ya kwanza ya kuuza uhuru wao. Kwenye uwoga hakuna uhuru watu huru sio waoga. Uwoga ni utumwa. Hivyo wasiogope kutoa maoni yao na kuikosoa serikali. Watu lazima waongee wanapoona wanavyoongozwa sivyo. Ni haki yao ya kimsingi kama raia.

Lakini uhuru huu unapaswa kutumiwa kwa kuwajibika. Raia wanapaswa kukataa mambo ya kipuuzi yanayofanywa na serikali yao kwasababu inahusu maisha yao ya sasa na ya baadae ya watoto wao. Kama kuna jambo la kipuuzi linafanywa na serikali yao wasiogope kupinga. Raia kama wanaona serikali yao inawapeleka wasipotaka kwenda ni wajibu wao kuwapinga.

Kama kuongea kwake anakandamizwa na kunyamazishwa kulikuwa na umuhimu gani wa kudai uhuru kutoka kwa wakoloni? Kama hayuko huru kutoa maoni kwenye taifa lake mwenyewe na kukosoa anapoona mambo hayaendi sawa? Kuwa raia huru kwenye taifa lolote ni lazima pia uwe na uhuru wa kutoa maoni wa jinsi unavyoongozwa bila woga wala hofu.

Lakini pia raia wakawajibika kwa kile wanachoongea. Tutajengaje hili kuwajibika kwa watu wetu? Ili wawe na uhuru wa kuongea na kuutumia kwa kuwajibika? Hatuwezi kuwanyima uhuru huu ni haki yao, lakini tutawajengaje kuwa raia wanaowajibika wanaojua cha kuongea chenye manufaa kwa taifa lao? Kwasababu

bila raia wetu kuwa na ufahamu wa hili, taifa letu halitoendelea. Tunakubaliana wote uhuru wa kuongea bila kuwa na mipaka na wajibu kwa taifa unaweza kuharibu pia taifa. Tutajengaje nidhamu hii?

Sio busara kuwanyima watu uhuru huu au kuwafanya watu kuwa na hofu kutoa maoni yao au kuikosoa serikali yao. Raia wana haki ya kumkosoa kiongozi yeyote lakini pia wana haki ya kumtendea haki kwa yale ambayo ni kweli.

Msingi ambao utajenga taifa hili ni kujadiliana kwa hoja na kuheshimiana. Watu wasiogope kwenda jela sababu ya kusema ukweli. Ni bora ufungwe kwa kuonewa kuliko kufungwa kwa kufanya makosa. Usiposema ukweli usaliti utakusuta. Na utakuwa hujalisaidia taifa lako kusonga mbele. Kwasababu taifa lolote linatakiwa kutafuta ukweli utakaolifanya taifa hilo lisonge mbele hatupaswi kuficha ukweli kwa hofu ya kuiogopa serikali. Kama unajua ukweli na unataka kurekebisha taifa lako simama ongea utakuwa umelifanyia huduma bora taifa lako na utakuwa mwenye faida kwa taifa lako. Kinyume cha hapo hautafika kama taifa kwa kuogopa kusema ukweli kwa kukumbatia uongo na matendo maovu.

SURA YA 3

TAIFA

Kila taifa linapaswa kuwa na misingi na linapaswa kuwa na vitu ambavyo wanaamini ndivyo vinavyowaunganisha pamoja kama taifa. Taifa lolote bila ya kuwa na uelewa mpana kwanini wako pamoja na misingi yao ni nini, ni vigumu kuendelea.

Kama nyumba inavyojengwa ambayo ni lazima iwe na msingi ili iwe imara, ndivyo taifa linavyopaswa kuwa na misingi. Pasipo misingi hii hakuna taifa ambalo litaweza kuwa imara lenye mpangilio na endelevu.

Nitajaribu kadiri ya uwezo wangu na kwa lugha rahisi sana kuelezea misingi hii, ili kila mmoja aweze kunielewa. Na mtakaponielewa tutakuwa na ufahamu mpana wa kwanini tuko taifa. Na pengine tutaweza kuweka dira yetu kama taifa sawa sawa. Na Baadaye yetu kama taifa itakuwa na mwangaza zaidi kuliko ilivyo sasa.

Taifa lolote lile lazima liwe na maono. Ni lazima ijulikane ni aina gani ya jamii na taifa watu wanapaswa kulijenga.

Mioyo yao na akili zao lazima zitengenezwe na maono haya. Kila kitu tunachokiona katika dunia hakikutokana na kitu kinachooneka, bali kilitokana na wazo kwanza na wazo likafanyika kitu halisi. Kwahiyo mifumo ya kijamii hujengwa, na ubora wake unategemea sana busara, maono, maarifa na uwezo wa kiongozi au viongozi.

Taifa lolote lililoratibiwa vizuri linategemea busara ya viongozi, ili sehemu zake zinazounda taifa ziwe na mahusiano mazuri na amani, katika kufanya kazi zake. Bila ya hivyo hakuna taifa litakalojengeka na kuwa bora.

Kitu kikubwa ambacho taifa lolote linacho kwa ajili ya maendeleo yake ni watu wake. Watu ambao wanaishi katika ardhi au sehemu ya ardhi katika dunia ambayo ina mtawala wake, au pengine watawala wake kulingana na aina ya tawala tulizonazo kwa sasa za kidemokrasia katika dunia za kupishana kutawala. Na kitu cha pili ni ardhi ambayo watu huitumia katika kulima, kujenga na mambo mengine ambayo hufanyika juu ya ardhi kama kufuga.

Ni dhahiri kabisa maendeleo ya kwanza kabisa binadamu kuanza kuyapata yalitokana na kilimo. Na ugunduzi wa kwanza ulitokana na changamoto za binadamu kutaka kuzalisha zaidi kupitia kilimo. Kwahiyo kilimo kina nafasi kubwa sana katika historia ya maendeleo ya binadamu.

Watu wameumbwa na akili na kadiri binadamu anavyotumia akili yake kukabiliana na changamoto ambazo anakumbana nazo katika dunia ndivyo anavyokua kiakili.

Maendeleo ni matokeo ya akili isiyochoka kufikiri katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili dunia. Maendeleo tuliyonayo kwa sasa katika dunia ni zao la akili za binadamu. Vitu vyote hivi tunavyoviona kwa macho yetu ambavyo tunavitumia kwa ajili ya matumizi yetu ya kila siku mwanzo havikuwepo. Vyote hivi vya asili na visivyo vya asili. Vya asili ni vyote ambavyo havijaumbwa na mikono ya binadamu, bali kwa nguvu ya Mungu na visivyo vya asili vyote vinavyotokana na gunduzi za binadamu. Vinavyotokana na binadamu kugundua siri iliyofichwa

kwenye asili, kwa maana nyingine siri zilizofichwa na Mungu kwenye upeo wa binadamu.

Visivyo vya asili ni zao la fikra zetu; fikra ambazo zimetufanya tuitawale dunia na kila kilichomo kwenye dunia. Hapo mwanzo ilikuwa vigumu mtu kuamini kwamba binadamu anaweza kusafiri angani kwa ndege, au ardhini kwa motokaa, au kupita chini ya bahari kwa kutumia nyambizi. Lakini akili ya binadamu imeweza haya. Na binadamu wote wana akili sawa. Kama iliwezekana kwa wazungu tunaweza kufanya mambo makubwa zaidi kama tukitumia akili zetu vyema. Ni jinsi tu tunavyoelekeza mawazo yetu.

Mawazo yetu tunayaelekeza wapi? Je ni kwenye vitu vyenye manufaa na tija kwetu? Kila kitu kinategemea mwelekeo wa mawazo yetu. Ni wakati sasa wa kufikiri kuhusu jambo hili. Binadamu na taifa ni zao la fikra zake. Hakuna zaidi ya hilo. Sisi ni zao la fikra zetu.

Kama tutakuwa na uwezo wa kufikiri sawa sawa tutajenga taifa hili vyema. Mikono yetu, macho yetu na miguu yetu ni nyezo tu ambazo akili hutumia kufikisha malengo yake; yawe malengo hasi au chanya.

Watu wameumbwa na akili na uwezo wa kujenga taswira kwenye akili ili kuweza kubuni na kugundua vitu ambavyo vitawasaidia kujiletea maendeleo na kurahisisha maisha ya binadamu hapa duniani.

Lakini maendeleo yao yanategemea sana kama watu hao ambao wanaishi kwenye taifa hilo wanajitambua na kama wameratibiwa vizuri na kupangwa vizuri katika mahusiano yao. Nikisema wanajitambua nazungumzia mtu mmoja mmoja na kwa pamoja kama wanajitambua kama taifa. Hili ni la muhimu na la kwanza.

Kujitambua kwa watu wetu kwa taifa lao. Kujua kwanini wako taifa na malengo yao nini na ni nini wajibu wao kwa taifa, nitachanganua kadiri ya uwezo wangu ili kuweka picha vizuri .

Familia ni sehemu ndogo ya taifa lakini ni muhimu sana. Familia katika udogo wake ndiyo inayounganisha taifa na jamii. Na misingi ya taifa lolote lazima ianzie huko. Maadili ya taifa lazima yaanzie katika familia. Kama tukishindwa huko chini, hatutaweza kufanikiwa katika ngazi ya taifa.

Kwasababu malezi ya raia huanzia katika ngazi ya familia, maendeleo yetu yanategemea sana vijana wetu wanalelewaje. Na hili ni jukumu la wazazi kutawala familia zao katika misingi iliyo bora. Serikali ina sehemu yake. Lakini msaada mkubwa katika kutawala nchi unategemea sana utawala katika familia.

Kama tunataka kujenga raia walio bora hatuna budi kuangalia familia zetu kwa umakini mkubwa na kuratibu watu wetu katika ngazi za chini. Lakini familia pia inategemea mahusiano yake yakoje katika jamii; kwa sababu familia inaunganishwa na jamii. Na kuna mambo ambayo yanawaunganisha pamoja kama jamii katika ngazi ya chini ambayo ni maslahi ya pamoja yaliyowaunganisha.

Maslahi haya hawawezi kuyapata kama hawako pamoja au kama hawana umoja. Kwa mfano shule, huduma za maji na umeme, hospitali na miundo mbinu. Mambo haya yote jamii haiwezi kukabiliana nayo kama hawana umoja. Na ni muhimu kufahamu kwamba tusipojali familia zetu hatutaweza kujali jamii zetu wala taifa letu. Huu ndio msingi ambao tunapaswa kuujenga; na kiongozi yeyote mwenye akili atautizama kwa umakini mkubwa.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya nidhamu kwenye familia na katika taifa. Wakati umefika sasa sisi kwa sisi kuelewana na kutambua kilicho bora na chenye maslahi kwetu ndani ya familia zetu na katika taifa letu.

Tusipowapanga watu wetu katika ngazi ya chini hatutaweza kupata maendeleo. Maendeleo yatakuja kirahisi ikiwa tutawapanga watu wetu vyema.

Kuna familia, kuna jamii inayozunguka familia na kuna taifa. Mahusiano ya vitu hivi vitatu ni muhimu sana. Na lengo letu ni kujenga raia wanaowajibika na hatutaweza kujenga raia wanaowajibika kama tutapuuzia malezi katika familia.

Adabu na heshima ni muhimu kwa taifa lolote. Kunapotoweka adabu na heshima hatutaweza kujenga taifa la maana. Na hatutaweza kujenga taifa kama tutakuwa na ubinafsi na tusipokuwa tayari kujitolea.

Hatuwezi kujenga taifa hili kwa nguvu, tunahitaji watu waelewe kwanini sisi ni taifa na malengo yetu ni nini kama taifa. Wajue faida ya kuishi katika taifa. Tunatafuta kujenga taifa bora la watu wenye furaha na upendo na wenye mashirikiano. Wajue hapa ni nyumbani kwao na hawana sehemu nyingine ya kuishi. Kujenga taifa la watu wenye nidhamu na dira.

Huu ndio mwelekeo ambao tunapaswa kuujenga kama taifa. Tunapaswa kujenga mahusiano yetu. Kuleta upya umoja wa taifa hili na uwajibikaji wa pamoja. Ni Muda muafaka kuacha ubinafsi na kuangalia maslahi mapana ya taifa. Tukijua kwamba tunakuwa bora zaidi tukiwa wamoja. Kujenga upya heshima na adabu ambayo imetoweka kwa kasi katika taifa letu.

Nguvu pekee haiwezi kuondoa hii kitu. Inahitajika busara na maarifa kujenga taifa hili na kuleta watu wake pamoja. Nidhamu haiwezi kuletwa na nguvu peke yake. Watu wetu wanapaswa kuelimishwa ili wajitambue kwamba tunajenga taifa hili kwa ajili yao na kwa ajili ya vizazi vijavyo. Na tunatumaini kwamba tutajenga Tanzania bora kwa ajili ya vizazi vijavyo. Tanzania ya watu wanaoelewana na wenye malengo mamoja.

Watu ambao wanajitolea wenyewe bila kusukumwa ni watu ambao wana uwezo wa kufanya vizuri zaidi kuliko wale wa kusukumwa. Tanzania haina watumwa wa kusukumwa. Tuko huru. Tunahitaji kujitolea wenyewe nafsi zetu bila kusukumwa kwa faida ya taifa letu. Tuna uwezo wa kufanya mambo mazuri kwa pamoja. Tuuzike ubinafsi wetu na tuje pamoja kama taifa.

Ni tumaini langu kwamba tuna uwezo wa kujenga taifa la watu wanaopendana na kuheshimiana lakini pia la watu wanaowajibika kwa taifa lao. Na wanaowajibika kila mmoja kwa mwenzake. Hii ndio Tanzania ninayowaza na ambayo niko tayari kuijenga. Inayonifanya usiku na mchana nisilale nikitaka kuona watu wa Tanzania wakiboreka kiakili na katika mahusiano yao.

Tanzania ambayo watu watakuwa tayari kulipa kodi kwasababu wanajua umuhimu wake katika maendeleo ya nchi na viongozi wanaowajibika kwa raia kikamilifu. Tanzania ambayo mahakama itatimiza wajibu wake kwa kutenda kwa haki na kwa mujibu wa sheria na bunge linalowajibika na lenye heshima. Tanzania ambayo kila mtu atatimiza wajibu wake na kujua umuhimu wa taifa lake. Tanzania ambayo kila mtu ataheshimiwa na kuthaminiwa.

Tanzania ambayo familia zitakuwa zimeimarika na heshima ya wazee ikarudi. Vijana wakaishi kama vijana kwa adabu na nidhamu na ndoa zikaheshimiwa na watu. Tanzania ambayo watu wanaheshimu majirani zao, kuwapenda na kuwa na uhusiano mwema.

Tanzania ambayo tutaunda taasisi ambazo zitawahudumia kwa moyo mmoja raia wa nchi hii. Tunahitajika kubadilisha tabia za watu wetu ili kujenga taifa hili. Sio tu katika serikali watu wote tunapaswa kubadilika tumepinda. Tunapita njia ambayo si sahihi.

Tunapambana na utandawazi lakini hatupaswi kufanya utandawazi kutumeza ni lazima tusimamie misingi. Na misingi hii ndio haswa chimbuko la ukuaji wa taifa lolote lile pamoja na amani.

Na watu watapenda vilivyo vyao na kuviangalia kwa ukaribu kama mali yao binafsi. Watajua miundombinu na taasisi mbali mbali ni mali yao na wanawajibu wa kuviangalia, kuvijali na kuviendeleza na kupenda nchi yao na taasisi zao.

Watu hujali vitu vile wanavyovipenda tusipopenda taifa letu hatutaweza kulijali. Na hatutaweza kulijali taifa letu kama hatujaliani wenyewe kwa wenyewe.

Tusipojaliana wenyewe kwa wenyewe tutafanya mambo yenye kudhuriana, kama hatutajali maslahi ya mtu mwingine tutajali maslahi yetu binafsi pekee. Kama hatutaona kumdhuru mtu mwingine ni sawa sawa na kujidhuru mwenyewe na kudhuru taifa tutawezaje kufika kama taifa? Kama tunajali maisha ya mtu mwingine hatuta mwingiza kwenye mambo yenye madhara.

Leo tunaongelea kuhusu madawa ya kulevya raia mmoja kwenda kumuuzia raia mwingine wa taifa hilo hilo madawa ya kulevya ni jambo lisilokubalika lakini tunapaswa kujiuliza na kutafuta ufumbuzi wa haya matatizo ni nini chanzo chake? Kwanini hatujali?

Kumekuwepo na vita inayoitwa ya madawa ya kulevya vyovyote tutakavyoita ikiwa kama wapiganaji wanapigana sababu ya kupata umaarufu wa kisiasa, au kwasababu ya nia yao ya dhati na dhamira ya dhati ya kutaka kuona vijana wetu hawapati madhara yatokanayo na madawa ya kulevya, vyovyote vile vita hii ni muhimu, lakini ni pana mno ni zaidi ya kupambana na wafanyabiashara ya madawa ya kulevya.

Matumaini yetu ya kushinda vita ya madawa ya kulevya ni madogo kama hatutapambana uovu wote. Madawa ya ulevya ni zao la uovu mwingine ambao upo katika jamii. Kama tunataka kupambana na madawa ya kulevya kwa kutumia nguvu pekee hatutashinda ni lazima kuwe na mtizamo zaidi ya moja.

Ni lazima tuangalie tunavyoishi ndani ya familia zetu, wazazi lazima wawajibike ipasavyo katika kuwalea watoto katika njia zilizobora na kujua wajibu wao kwao binafsi na kwa jamii inayomzunguka. Vijana wasipojua wajibu wao kwa kijamii na wajibu wao wa kitaifa hakuna cha maana tutakachojenga.

Vijana wetu kuuza madawa au kufanya mambo mengine yenye madhara kwa jamii ni kutokujua wajibu wao au kutokuwa na elimu ya kutosha na kutokujua nafasi yao katika jamii. Order katika nchi yetu itategemea sana jinsi tunavyowalea vijana wetu. Nidhamu yao inategemea hilo pekee. Kwa kijana kujiingiza kwenye uuzaji au utumiaji wa madawa ya

kulevya kuna matatizo katika malezi na katika jamii, tatizo ambalo tunatakiwa kuliangalia kwa ukaribu sana kwenye mifumo yetu.

Sawa tuna polisi lakini tusipoelimisha watoto wetu na kuwalea vijana wetu vyema kila siku tutaongeza pesa kwenye bajeti na kuongeza polisi na vituo vya polisi, kuongeza mahakama na kufunga vijana wetu wengi. Haya matatizo ya kijamii lazima yaelezwe na yatafutiwe njia ya kuyatatua ili yasiwe yanaibuka ibuka. Swali ambalo tunapaswa kujiuliza ni tufanye nini ili raia wetu wawe wema na watii wa sheria. Hatuwezi kupambana na madawa ya kulevya kama raia walio wengi hawajui nini maana ya kuwa wema au haki maana yake nini. Tutapambana vyema na madawa ya kulevya kama familia zetu zitakuwa imara na nzuri lakini zenye maadili na zinazojua haki.

Hatuwezi kumaliza suala la madawa ya kulevya kwa nguvu peke yake. Matatizo ya kijamii ambayo tunayokabiliana nayo sasa ni lazima tunayaangalie katika mifumo yetu ya makuzi na malezi na mahusiano yetu.

Lazima tuangalie katika tabia tunazozijenga kwa watoto wetu na vijana wetu. Kuwafunga watu kwasababu ya kutenda visivyo sahihi pasipo kuwa na mifumo mizuri ya malezi na makuzi ni kuendelea kila siku kuongeza gharama katika kujenga vituo vya polisi na jela wakati tunaweza kuzuia haya mambo kama tukiwa na malezi na makuzi mazuri.

Na kama tutatoa elimu bora ya maadili kwa watu wetu. Ni lazima tufanye hivi ili kupunguza uhalifu na matumizi ya hela nyingi kwenye kudhibiti uhalifu.

Ni lazima tuangalie upya mahusiano yetu na mashirikiano yetu. Kwasababu bila kuwa na

mahusiano mazuri na mashirikiano mazuri matatizo mengi ya kijamii hatutaweza kuyatatua ikiwemo suala la madawa ya kulevya ambalo linahitaji nguvu ya pamoja ili kulimaliza.

Hatutaweza kumaliza matatizo ya kijamii ikiwa kila mtu atajifungia nyumbani kwake na kama hakutakuwepo muda wa kuyajadili na kutafuta ufumbuzi wake. Kama tunataka tutibu matatizo ya jamii yetu hatuna budi kuwa watu wamoja katika mawazo yetu na matendo yetu. Kama hatutakuwa wamoja katika mawazo yetu na matendo yetu, changamoto nyingi ambazo zinatukabili kama taifa hatutaweza kuzitatua kama mawazo yetu tutayaelekeza kwenye ubinafsi na sio kwenye utatuzi wa changamoto zinazotukabili pamoja kama taifa.

Kama kila mtu akiangalia maslahi yake binafsi na sio maslahi ya taifa hatutaweza kujenga hili taifa na hapatakuwa sehemu nzuri ya kuishi. Kama tunataka kujenga jamii nzuri ni lazima tuangalie tabia za watu wetu na mahusiano yao.

Mahusiano yetu ni muhimu katika ujenzi wa taifa imara. Ni lazima tuangalie malezi ya watoto wetu kwa ukaribu na kuwafanya wawe watii kama wazazi wakishindwa kuwaongoza na kuwatawala watoto wao vyema hakuna jamii itakayobaki na mfumo mzima wa kijamii utaharibika.

Ni lazima wazazi wawe na uwezo wa kuwatiisha watoto wao na kuwaongoza katika njia yenye maadili. Kama wazazi wakiwa wamekengeuka tutegemee nini kama jamii? Sio kuharibika kwa taifa letu na mfumo mzima wa kijamii? Leo tunahangaika kuhusu madawa ya kulevya na hata kuongezeka kwa tabia mbaya ndani ya jamii ni malezi yetu yaliyotufikisha hapa.

Tumeshindwa kuwatiisha watoto wetu kuwa na adabu na nidhamu na kuheshimu masuala ya msingi yanayohusu maisha. Kama ndoa zetu haziko imara tusitegemee kwamba ndoa za watoto wetu zitakuwa imara. Tunawafunza nini watoto wetu kama hatuheshimu ndoa zetu? Kama tusipokuwa wakali kwa watoto wetu tusahau kitu kinachoitwa maadili.

Tuongeze tu vituo vya polisi na mahakama badala ya kuwalea vizuri tukawafunge huko lakini matatizo yataendelea kuwepo kwakuwa hatujatoa kiini cha matatizo yetu.

Tatizo jingine ni ubinafsi kila mtu anajiangalia mwenyewe na sio jamii na matatizo yanayohusu jamii. Kama kitu hakijakutokea wewe hujali. Kama mtoto wako hatumii hujali. Tunaona kitu ambacho si sahihi kinatokea mitaani kwetu hatuchukui hatua hata kama bhangi zinauzwa kwenye mitaa yetu. Ili haya mambo yaishe ni lazima tuwe na dhamira ya dhati ya kutaka kuondokana na uovu na dhamira hii ni lazima itoke ndani yetu wenyewe. Na wenyeviti wa mitaa ambao wamepewa wajibu wa kuona haya mambo hayapo lazima wawajibike.

Kama uovu ukiongezeka na kama hatua hazitachukuliwa mapema, kila wakati njia ambazo zitakuja kuchukuliwa baadae huwa ni ngumu za kusikitisha za kuogofya. Ni muhimu kuzifanya roho za vijana wetu kuwa nzuri na njema kabla njia kali na za kusikitisha hazijaja kuchukuliwa wakati jamii itakapokuwa imeharibika sana. Tunajifunza hili kila wakati na historia ni mwalimu mzuri.

Naungana mkono na mapambano ya madawa ya kulevya lakini zaidi ya yote elimu ya maadili ipewe kipaumbele kwenye mashule yetu na katika familia zetu kwasababu misingi ya utaifa wetu inategemea

maadili yetu. Kufanya mambo yenye adili, yenye haki na usawa. Ikiwemo kutokumuuzia madawa raia mwenzako na kutokujali maisha ya mwenzako.

Kila mtu ana haki ya kuwa na mali. Ni haki ya kimsingi ya kila raia wa taifa hili kumiliki mali. Ambayo inatokana na kazi na juhudi za mikono yake na fikra zake.

Kama binadamu ambaye amekamilika anawajibika kufanya kazi ili kuboresha maisha yake ya kila siku. Binadamu maisha yake lazima yaende mbele na sio kurudi nyuma. Na moja ya maendeleo ambayo binadamu anapaswa kuwa nayo ni umiliki wa mali.

Kwahiyo ni jambo la kimsingi na la muhimu kwa haki hii kutoporwa. Pamoja na mengine mali ni utambulisho wa mtu. Utambulisho wa juhudi na maarifa yake. Ingawaje sio kila wakati iko sawa; Kuna watu wanapata mali visivyo halali kwa rushwa na ufisadi na uuzaji wa madawa ya kulevya.

Nazungumzia juhudi za mtu. Na sio zile kazi ambazo sio halali. Bali kazi ambazo mapato yake yamepatikana katika misingi ile halali. Lakini tatizo kubwa ambalo tulilonalo na ambalo tunakabiliana nalo kama taifa ni fikra za watu kuhusu mali lakini sio mali zenyewe, mali au utajiri hauna matatizo yeyote.

Tatizo tunatumiaje mali hizo na tunazipataje na tabia za watu kuhusu mali. Binadamu anatakiwa atawale mali na sio mali zimtawale na azitumie mali zake katika njia za haki kubadili jamii iliyomzunguka. Pesa ni nzuri ikitumiwa vizuri ina faida nzuri na yenye manufaa. Kwahiyo kama binadamu tunatakiwa kuwa makini na tunavyotumia pesa ili ilete mabadiliko chanya katika jamii zetu.

Kwa mtu anayefanya kazi kwa bidii na kwa haki bila kumdhulumu yeyote mali ni faida ya juhudi zake na maarifa yake. Ametumia juhudi zake na maarifa yake kuzalisha hivyo anapata alichokipata.

Wakati huo huo hatupaswi kuwa watumwa wa mali. Ni lazima tujue haki ni nini na maisha yetu lazima yajengwe kwenye mizani ya haki na wajibu.

Wajibu wetu kwa binadamu wenzetu. Hatupaswi kuweka mali juu ya ubinadamu. Kufanya hivyo ni kuabudu mali na mali tunapaswa kuitawala na sio kututawala na kutuondoa kwenye misingi ya ubinadamu.

Binadamu kuwa mkamilifu lazima aondoe choyo . Kwasababu dunia haiwezi kuwa salama kama kila mtu akiwa na choyo. Choyo huleta kujilimbikizia bila kujali wengine. Kwahiyo tunawajibika kusaidia maskini ili kujenga jamii yenye utulivu kwa wale ambao wamebalikiwa kingi.

Ni muhimu kubadilisha tabia zetu kuhusu mali. Mali ni chombo kinapaswa kutumika kuleta mabadiliko chanya katika jamii na sio kuharibu jamii. Tunapaswa kuwa wenye busara katika hili. Jinsi tunavyotumia mali zetu. Hatupaswi kuabudu mali na kuipa umuhimu na uzito kuliko hata ubinadamu na kuifanya kuwa Mungu wetu na kutaka kutawala wengine na kuharibu maisha ya wengine.

Pesa ni kitu kizuri kama ikitumika vizuri lakini ikitumika vibaya ina madhara makubwa. Tunatakiwa kuwa na busara jinsi tunavyotumia pesa. Lakini ni ukweli usiopingika ukipata pesa kwa busara utazitumia kwa busara na manufaa yake yatakuwa makubwa kwa jamii.

Watu wanalinganisha kufanikiwa kwa mtu ni wingi wa mali alizonazo. Wamekuwa wakishindana kupata mali nyingi. Na imekuwa sifa kuwa na mali nyingi na mali kupewa kipaumbele kuliko kitu chochote kingine. Kwa jamii ambayo fikra zake ni kwenye mali peke yake, pasipo kutazama misingi mingine ya haki na wajibu kwa ubindamu na maadili. Jamii ya aina hii haitadumu muda mrefu.

Lakini si kweli kwamba kufanikiwa kwa mtu ni kuwa na mali peke yake. Japo mali ina umuhimu wake na sehemu yake katika maisha ya binadamu. Lakini kuna mambo mengine ya kimsingi tunapaswa kuangalia zaidi ya mali peke yake. Heshima ya mtu haipaswi itokane na mali peke yake bila kuangalia tabia ya mtu.

Mali inaweza kupatikana kwa madawa ya kulevya, mali inaweza kupatikana kwa ujambazi na hata kudhulumu watu na hata inaweza kupatikana kwa unyonyaji. Anayepaswa kuheshimiwa ni anayemuogopa Mungu, anayetenda haki na kusema ukweli. Na sio kuwa na mali peke yake iwe chanzo cha heshima hata kama tabia yako ni mbovu.

sehemu ya pili

DIBAJI

Uzalendo ni roho ya ujenzi wa taifa lolote. Kwa uzalendo watu hulinda mataifa yao. Kwa uzalendo hupigana vita kuyatetea.

Pale uzalendo unapotoweka kunakuwepo jamii yenye mgawanyiko na isiyokuwa na lengo moja. Na ulinzi wa mataifa hayo huwa dhaifu, kwakuwa uimara wa taifa lolote uko katika umoja wake.

Ni katika nguvu hii, watu hujenga na kuendeleza mataifa yao. Ni ukweli usiopingika kwamba bila kulipenda taifa letu itakuwa vigumu kulijenga. Hatua ya kwanza kwa taifa lolote kuendelea ni kwa raia kulipenda taifa lao. Nguvu yoyote ya taifa hujengwa katika uzalendo wa watu wao.

Tunaweza kujadili matatizo yetu kutoka asubuhi hadi jioni; hilo halitoondoa matatizo yetu. Bila kutenda. Taifa hili litaendelezwa na watu watakao weka suluhu mezani nakusema sasa tunasonga mbele; watu wenye matumaini na dhamira ya dhati kuleta mabadiliko. Bila tumaini hili, taifa hili haliwezi kukua. Kwa maamuzi magumu mataifa yalipiga hatua. Kwa ushupavu yaliendelea.

Ni katika jitihada hizi zisizofifia ile ndoto iliyoonekana kama kitu kisichowezekana ilikuwa kitu kamili na dhahiri machoni mwa watu. Ujenzi wa taifa jipya lazima uje. Ndoto yetu lazima itimie. Pasipo uzalendo jitihada za kulijenga taifa hili zitakuwa ngumu.

Uzalendo ni maana halisi ya kulileta taifa pamoja katika lengo moja na jitihada za pamoja kwenye mwelekeo wetu wa kujenga taifa bora na imara.

Shaaban Y. Shaaban
Mwanza, Tanzania 2017

SURA YA 1

SERIKALI

Kuongoza na kutawala, ni jukumu la serikali. Kutawala ni kama kulinda, kutotawanya, kukusanya na kutoruhusu kutawanyika. Kulinda binadamu dhidi ya uharibifu na uovu ni jukumu la serikali. Kulinda na kuhifadhi ubinadamu ni jukumu la serikali.

Kuongoza ni kuonyesha njia ni wapi taifa linapaswa kuelekea, kwahiyo ni lazima uweze kutawala na kuongoza kwa pamoja. Serikali haiwezi kukamilika pasipokuwa na vitu hivyo vyote viwili. Kimoja ikiwa ni dira na kingine kukusanya na kulinda. Ili serikali ifanye kazi vizuri ni lazima iwe na uwezo huo. Lazima ikusanye, ilinde na iongoze. Kwa kukusanya namaanisha ni kuweza kujenga umoja wa wananchi na kuwafanya kuwa na dira moja.

Mfano mzuri wa kutawala na kuongoza ni mfano wa kondoo na mchungaji. Mchungaji ni lazima akusanye kondoo katika kundi moja ili awaongoze kwenda malishoni. Na kila aliyetoka nje ya mstari ni lazima amrudishe katika mstari ili kondoo wote wafike na wawe na mwelekeo mmoja. Mchungaji ni lazima ajue anapowapeleka kondoo. Na ili nchi iende sawa kiongozi ni lazima awe na uwezo wa kutawala na kuongoza kwa pamoja.

Taifa lolote ni lazima liwe na mwelekeo kukosa mwelekeo ni kukosa uongozi. Kutawala peke yake hakusaidii pasipokuwepo na dira. Na ili dira iwepo ni lazima watu wakusanywe pamoja katika lengo moja ambalo litakuwa ni ujenzi wa jamii bora zaidi kwa faida ya wote. Akili za wananchi ni lazima zielekezwe

katika mwelekeo fulani, akili zilizotawanyika hazitaweza kujenga taifa. Kwahiyo kiongozi ni lazima awe na maono, na kujua ni wapi anataka kupeleka watu wake na taifa.

Ni lazima ajue kuratibu watu wake katika serikali kulingana na maono aliyonayo ili maono ya serikali yawe pia ni ya wananchi. Kwa njia hii pekee taifa huweza kuwa na dira.

Lakini hii inahitaji uongozi wenye roho moja, akili na jitihada za pamoja katika kufanya kazi ili kufanikisha maono na sera ambazo wote ni lazima waziamini. Ni lazima kiongozi awe na timu inayofanya kazi vizuri na kwa pamoja.

Ni muhimu kuwa na viongozi hodari na wanaoamini katika maono na itikadi ambayo kiongozi wao anayo na kusambaza maono hayo kwa wananchi ambao nao kwa upande wao ni muhimu kuyapokea kama ni mazuri kwa mustakabali wa taifa.

Hapa unakuja umuhimu wa chama katika kusaidia itikadi na maono haya kwakuwa serikali peke yake bila kuwa na chama kinachoamini maono hayo serikali haitoweza kufanya kazi vizuri na nchi kwenda mbele. Chama ni muhimu sana katika kutumika kusambaza maono haya ambayo ni muhimu kuwafikia wananchi.

Ninapo zungumzia itikadi ni ile nguvu ambayo itatumika kusambaza maono. Kwakuwa naamini maono na itikadi ni vitu viwili tofauti. Maono ni taswira ya kitu ambacho bado hakionekani kiko katika fikra, kitu kinachohitaji kutekelezwa ili kuwa kitu dhahiri. Lakini maono haya yanahitaji nguvu ya utekelezaji wake ni lazima watu wayaamini na wafanye jitihada ya kuyakamilisha ili kujenga kile kitu

wanachohitaji na hapo ndipo itikadi inapounganishwa na maono.

Itikadi mara nyingi haitumii akili ni kuamini tu katika kitu, lakini maono hutokana na fikra za kina, lakini hizi fikra zinahitaji msukumo hivyo ni lazima tuunganishe maono hayo na itikadi. Ni lazima vitu hivi viwe na uwiano. Baada ya kutafakari kwa muda mrefu na kupata uhakika wa jambo na pale fikra zinapojengeka hapo ndipo itikadi inapojengeka, itikadi inapojengeka katika maono hutengeneza dira. Kwahiyo ufanyaji kazi wa kitu chote kinachoitwa taifa ni lazima uendane na maono.

Kuna tofauti kubwa sana kati ya mipango na maono. Ni lazima kwanza uwe na maono alafu ndio uweke mipango ya kufikia huko. Kuwa na mipango bila maono ni kukosa mwelekeo. Ni lazima tujue tunafanya nini na kwasababu gani na kama kila tunachofanya kitatufanya kuyafikia maono yetu.

Mfano wa maono na mipango ni kama nyumba na matofali. Maono ni nyumba lakini mipango ni matofali. Kimoja kinakupelekea kufanikisha kuwa na kingine. Lakini kupanga bila kutenda, kunafanya mipango na maono kutokamilika. Kwanini tunashindwa kama taifa? Ni kwasababu tunakosa maono ya pamoja na hivyo tunakosa dira. Tuna mipango mingi tu bila maono. Maono ni picha kubwa lakini mipango ni vitu vidogo vinavyokamilisha picha kubwa.

Ili kujenga nyumba kubwa ni lazima uwe na matofali, mbao, mabati, misumari nk. Hivi vyote navifananisha na mipango. Nyumba naifananisha na maono. Sisi tunafikiria misumari, mabati, mbao na matofali badala ya kufikiria nyumba.

Kwa mfano ni lazima tujue tunataka kujenga taifa la namna gani, ni lazima tuwe na taswira ya namna ya taifa hilo litakavyokuwa ili tuunganishe nguvu zetu kulijenga. Ni lazima elimu yetu ielekezwe kujenga taifa la namna hiyo. Bila kuwa na mwelekeo huu hatutajenga chochote. Ni lazima tuwe na ramani ya kile tunachotaka kukijenga kama nyumba ilivyo ili kile kilichopo akilini kiwe kitu bayana na kinachoonekana. Ubora wa taifa letu utategemea sana taswira tulizozijenga akilini mwetu.

Kufikiria kuondoa umaskini peke yake si sahihi ni lazima tufikirie kujenga nyumba, tujue rangi gani tutaipaka na itaonekanaje ni lazima tuijenge ivutie.

Ni lazima tuwe na jamii iliyounganishwa na kitu fulani na hicho ni maono. Tukifikiria kuhusu umaskini akili zetu zitafungwa tutashindwa kuwa na maono yatakayotupeleka mbele. Umaskini ni mapito tu ambayo jamii na watu hupitia, umaskini si wa kudumu. Kama miti na wanyama wanavyokuwa na mataifa pia hukua kutoka katika umaskini wao kuelekea kwenye kujitegemea na utajiri na mamlaka. Mataifa yote yalianza kwenye umaskini. Kwahiyo umaskini ni mchakato tu wa kuelekea sehemu bora zaidi. Kama watu wana maono umaskini si kitu cha kudumu.

Kuna aina mbili za mataifa maskini; Kuna taifa ambalo ni maskini lisilo kuwa na matumaini na kuna taifa ambalo ni maskini lakini lenye jitihada. Taifa lolote maskini na lenye jitihada ni lazima liongozwe na maono na matumaini ya kufanikisha hayo maono. Kwakuwa wanaamini umaskini sio kitu cha kudumu ni cha kupita. Wanajua utajiri ni zao la akili, busara, jitihada na maarifa.

Kuwa maskini na kukosa matumaini hupelekea kuwa na ufukara. Kwahiyo taifa fukara ni lile maskini na watu wake wamekosa matumaini na baadae yao. Hili kamwe halitoendelea. Mataifa mengi ya afrika yapo hapa.

Kwetu sisi kama watanzania kuna matumaini kama tutabadili mwelekeo wa fikra zetu wa sasa. Kama tutaacha utapeli na kuheshimu wafikiriaji.

Serikali na jamii, inaunganishwa na kitu kimoja tu haki. Pale serikali inapokiuka misingi yeyote ya haki inaharibu misingi ya uwepo wake. Watu katika taifa hugawanyika na malengo ya pamoja hupotea. Serikali kama dereva na wananchi kama gari, Ubora wa taifa lolote utategemea sana ubora wa viongozi walionao.

Maisha ya nchi ni kama safari ndefu, wote tukiwa tumepanda kwenye basi kubwa na lengo letu likiwa kufika sehemu moja. Ni lazima tutafute dereva makini na bora ili tufike salama na sio dereva yeyote Yule. Tunajua magari hupinduka na gari linapopinguka safari ya watu huishia njiani.

Embu tuangalie kwa makini tabia za wasafiri tujifunze kutoka kwao, jinsi wanavyoshirikiana wakiwa safarini, hii ni kwa sababu tu wao ni safari moja. Sisi ni kaka na dada tunaojenga taifa moja. Katika taifa letu kuna nembo ya mwanamke na mwanamme kama nembo ya taifa.

Sisi wote ni lazima tuungane kujenga taifa moja tunajua ni kwakuwa wamoja tu bila kujali uanamke wetu na uanamume wetu ndipo taifa hili litakapo songa mbele ikiwa kila mmoja wetu atashiriki katika ujenzi wa taifa hili kwa moyo wake wote.

Iwe katika malezi ya watoto wetu na ujenzi wa uchumi wetu. Au iwe katika kujenga maadili ya taifa.

Nembo yetu ya taifa inasisitiza juu ya uhuru na umoja. Lengo ni kufanya jitihada kuleta watu wetu pamoja baada ya kupata uhuru wetu. Kwakuwa kama tungepata uhuru bila kufanya jitihada za kufanya watu wetu kuwa wamoja ingekuwa haina maana. Umoja wetu ndio utakaopelekea mwelekeo wetu kama taifa. Ni katika umoja huu ndipo tutakapoweza kulinda uhuru wetu. Ni umoja huu ndio uliotufanya kupata uhuru wetu kutoka kwa waingereza.

Lakini taifa letu ni lazima lisiwe taifa la kiimla watu wetu ni lazima wawe na uhuru wao, wasikandamizwe na serikali kwa namna yeyote ile na ni lazima tuunganishwe kama taifa na haki, wajibu, umoja na uhuru wa mtu. Lakini pia ni lazima tulinde uhuru wa taifa.

Sisi ni wasafiri tunaoongozwa na picha kubwa. Picha kubwa ya aina ya taifa tunalotaka kulijenga, aina za jamii tunazotaka kuzijenga na aina ya familia tunazotaka kuzijenga. Vyote hivi havitawezekana kama hatutakuwa wamoja na tunaoongozwa na picha kubwa.

Kila taifa lazima lijue mwisho wake ni upi. Kila taifa ni lazima liwe na mwelekeo. Hakuna ghorofa litakalo jengwa na kutokuwa na mwisho. Mchora ramani huchora na kujua mwisho wake. Hata pale tunapoangalia asili, mti huchipua ukua na mwisho wake hufa. Vilevile kwa maisha yamekuwa hivi kwa binadamu.

Tofauti na kwa wenzetu sisi bado tuna cha kujenga. Hatujafika kileleni bado. Lazima tuwe na tumaini hili.

Mataifa hujengwa kwa juhudi, maarifa, hekima na busara.

Msingi wa majadiliano katika sehemu hii ni serikali. Kama dereva wa jamii na taifa. Kama ilivyo kwa dereva yeyote yule, lazima awe na mwelekeo isipokuwa kama amelewa, gari itayumba na kukosa dira. Na lengo letu sisi ni kufika salama.

Jamii bora na taifa bora hujengwa na serikali makini ambayo akili zao zote ziko katika ujenzi wa Taifa na jamii. Ni kujitolea huku kwa upande wa serikali ndiko kutakakofanya taifa liendelee. Na hili linahitaji nidhamu ya hali ya juu. Na dhamira ya dhati ya kutaka kuona mabadiliko.

Serikali na jamii ni vitu viwili tofauti na wala sio kitu kimoja. Vina asili tofauti. Utapoangalia kwa ukaribu utagundua hili, Kwa serikali ni lazima wawe na uwezo mkubwa wa kiakili na nguvu kuliko jamii ili wawe na uwezo wa kutawala. Vingenevyo jamii haitoweza kulindwa kwasababu asili ya binadamu ni uovu na serikali iko kulinda haki ya kila mmoja. Hakuna serikali yeyote iliyosimama kwa muda mrefu kwa kutenda uovu kwasababu asili yeyote ya serikali ni kulinda haki.

Kwahiyo serikali ni kiini cha Taifa lolote. Serikali imara hutengeneza Taifa imara na kinyume chake. Kwahiyo jamii na serikali sio kitu kimoja kamwe haiwezi kuwa kitu kimoja. Ingawaje serikali ni sehemu ya jamii.

Chumvi na maji ni kitu kimoja? Ukiweka chumvi kwenye maji hubadilisha radha yake lakini chumvi hubaki chumvi. Kama kulivyo na bwana mwema na bwana mwovu vile vile kuna serikali ovu na serikali njema. Ubwana uliopo katika serikali sio ubwana wa

kujikusanyia bali ule wa kufanya kazi kwa faida ya umma, wa kuhakikisha jamii inazalisha na kuwa endelevu na wa kuhakikisha haki inatendeka, inalindwa na inaendelezwa. Kuhakikisha pia umoja wa nchi unaendelea kuwepo kama nyenzo ya kuharakisha maendeleo.

Ninapozungumzia umoja sio huu wa kutokuwepo mifarakano miongoni mwa sehemu za jamii zinazounda Taifa. Bali umoja wa kiakili na kimalengo, umoja wenye nia moja. Umoja ulio huru dhidi ya ubinafsi. Umoja unaoleta hisia za utaifa. Unaoleta hisia za mimi ni wa taifa fulani.

Hisia hii ni muhimu kwa ujenzi wa taifa lolote. Pale hisia hii inapoondoka na jamii inaposhindwa kutambua wana wajibu kama walivyokuwa na haki kwa taifa, ile asili ya utaifa huondoka na kuwa kundi la watu wanaoishi pamoja na sio taifa, kila mtu akiongozwa na ubinafsi wake na dhamira yake binafsi na ile hisia ya utaifa huondoka na dhamira ya taifa katika mioyo ya raia huondoka.

Tukizungumzia ya kwamba kwa kutokuwepo kwa vita ndani ya taifa kwamba ni wamoja tutakuwa tunakosea. Umoja wa taifa lolote utaupima katika ushirikiano wa watu wake, na utayari wa watu wake kulitumikia taifa kwa faida ya wote.

Watu wanaweza kutofautiana katika taifa lakini ni katika kuboresha taifa na sio katika misingi ya ubinafsi. Msingi wa umoja utauona katika kujitolea kwa watu kwa faida ya umma.

Kwahiyo serikali inahusika moja kwa moja katika ujenzi wa umoja wa taifa na kulinda umoja huo. Umoja huu ambao msingi wake ni malengo ya pamoja.

Ni lazima umoja huu uangaliwe kwa jicho moja. Taifa hupitia hatua kama nyoka ambavyo anavyojivua gamba. Ni lazima liwe jipya kila muda unavyokwenda likienda likibadilika kutoka katika picha kubwa ya Taifa na kutokana na hali inavyoenda kwa wakati huo. Picha kubwa ni taswira ambayo taifa limeweka kuifikia. Taswira ambayo ni lazima juhudi zifanyike ili iwe kitu halisi kinachoonekana.

Hatua ya kwanza kwa Taifa lolote kuendelea ni kujitambua kwake. Taifa halitoweza kujitambua pasipo serikali kujitambua na wananchi kujitambua. Na kujua uhusiano wao, uhusiano wa Taifa, wananchi na serikali.

Pasipo kujitambua huku, hatutaweza kuendelea na kujitambua huku kutakuja tu kama tukiwa wenye malengo mamoja. Hisia hii ya mimi ni mtu wa taifa fulani na kujua wajibu na haki zako.

Hisia hii ya kumuona mtu mwingine kama sehemu yako, ambaye mna sehemu katika taifa, mna haki na wajibu ndio msingi wa uraia. Kujitambua huku ndiko kutakako tufanya kuwa taifa lililo kamilika, kumuona raia mwenzako kama ndugu yako.

Utaifa hufanyika kwa miaka mingi na msingi wa utaifa hujengwa katika mioyo na akili za watu na ubomolewa pia katika mioyo na akili za watu. Turudi katika fikra nyepesi katika familia, Hisia hii ya kuwa mtu wa familia fulani kila mtu anaijua.

Familia ambayo inaundwa na baba, mama na watoto. Familia kama sehemu ndogo ya taifa ambayo baadae inaunda jamii na taifa. Hisia hii ya utaifa ni sawa na ile ambayo mtu anatakiwa ahisi kama ni mtu wa familia fulani.

Hali hii huweza kuharibika na hisia hizi zote za utaifa, ufamilia na hisia za ujamii huondoka. Na mfumo wote wa kijamii kuanguka.

Kuanguka kwa hivi vyote hutokana na uongozi mbovu wa kila sehemu husika na upungufu wa nidhamu na maadili katika jamii. Na taifa kama taifa haliwezi kulindwa pasipo vitu hivyo. Ili kulinda vitu vyote hivyo na jamii iwe na mpangilio mzuri, nidhamu inahitajika.

Ni vigumu kwa serikali kutawala pasipo kila kiongozi husika katika ngazi ya jamii, familia na taifa kutimiza wajibu wake. Lakini mzigo mkubwa lazima atwishe viongozi kwasababu wana wajibu wa kuunda na kulinda kile walichounda. Hii inahitaji kiongozi makini anayejua anachokifanya.

Vijana wanazaliwa na wanakua, wanakuta wazee wakiishi, wanategemea uongozi kutoka kwao. Uongozi unaotokana na fikra sahihi. Jinsi gani waishi katika taifa. Lakini hawakuti hilo. Walitegemea kupewa muongozo kuhusu utaifa na uzalendo, kutoka kwa watu waliotangulia kabla yetu. Walitegemea watakuta dira ya jinsi gani kijana aishi katika taifa lake.

Tabia za wazee kwa taifa lao walitegemea ziwe za unyoofu, wawe rula ya kuwajenga vijana katika utaifa. Ni muhimu kufahamu kama wazee waki kengeuka juu ya utaifa na uzalendo na juu ya maadili na nidhamu ya taifa, taifa na jamii itakosa mwelekeo.

Kama wazee wetu wangekuwa na fikra chanya juu ya taifa hili, vijana wangefuata nyuma kama maji yanavyofuata mkondo wake. Vijana wanaokua wanahitaji mfano, na wanapozaliwa na kukua

wanategemea kuupata mfano huu kutoka kwa wazee wetu. Ingekuwa rahisi sana kwetu kama tungekuta msingi mzuri umejengwa ili safari yetu isiwe ngumu sana bali tuwe na majukumu mengine ya kufanya.

Ni dhahiri kabisa tunapokea taifa lisilo na umoja na uzalendo na ni jukumu letu kuileta nchi pamoja upya. Ni lazima sasa tujenge uzalendo na uwajibikaji katika taifa ili tuwe na fikra chanya. Katika mtazamo huu, tunaweza kulijenga taifa hili na kurithisha kizazi hata kizazi katika jitihada ile ile na uzalendo ule ule wa kulijenga.

Bila hisia hii ya uzalendo na uwajibikaji kwa taifa hatutaweza kulijenga taifa hili. Hatutaweza kulijenga taifa hili katika ubinafsi. Roho hii ya jitihada za pamoja katika kujenga nchi ni lazima ijengwe. Jitihada za mtu binafsi kujiendeleza lazima ziende sambamba na jitihada za taifa kujiendeleza. Hili taifa ni lazima liwe na sehemu katika kila moyo wa mwananchi.

Wajibu wa mtu wa kujiendeleza mwenyewe na familia yake bila kuingiliwa, wajibu huu usiingiliane na wajibu wa mtu kwa taifa lake. Maslahi ya binafsi na yale ya Taifa ni lazima kuwe na mipaka.

Hili tunaweza kufanikisha kama tukiwekeza katika elimu, na kuelimisha watu wetu kuhusu wajibu na haki zao na kama tukitekeleza ipasavyo sheria zilizopo ili kulinda maslahi ya umma.

Msingi huu wa wajibu na haki ni muhimu sana. Tusipojenga misingi hii ya wajibu na haki hatutaweza kufika popote kama taifa. Hatutaweza kujenga taifa hili katika misingi ya ubinafsi.

Tutaweza kulijenga taifa hili ikiwa tu tutakuwa na mahusiano mazuri miongoni mwetu. Na kama tukiwa na malengo ya kujenga jamii zetu na taifa letu kwa pamoja na katika mwelekeo sahihi unaotokana na fikra sahihi na kuongozwa na uzalendo kwa taifa letu.

Ni kujitolea huku tu ndio kutakako lipeleka taifa hili mbele. Kujitolea pasipo kuweka ubinafsi mbele. Wengi wetu tunashangaa bunge lilipofikia. Hadhi na nidhamu yake, lakini tunashindwa kuangalia chimbuko lake kwa undani zaidi kwa kuangalia jamii yetu na mfumo wake, ambako wabunge wametokea huko.

Pasipo kuangalia familia zetu na uhusiano wetu miongoni mwa jamii jinsi ulivyo, Upendo wetu kwa majirani na kwa jamii, na mashirikiano yetu. Nidhamu katika familia zetu na katika jamii. Kuwajibika kwetu miongoni mwetu katika ngazi ya chini ya familia, na katika jamii.

Heshima yetu na nidhamu yetu kwa jamii ikoje na vitu kama hivyo. Kama tukitafakari kwa makini sana tutaona matatizo haya yameanzia chini kabisa. Kwenye uwajibikaji katika familia na katika jamii na imefikia katika ngazi ya taifa.

Jamii inayowajibika itamtuma mtu anayewajibika kwenda bungeni akifanya mchezo haitamwachia ni lazima itamwadhibu. Kwahiyo ili tujenge taifa hili ni lazima tutengeneze tabia ya uwajibikaji na tusiache mambo yaende tu. Hili ni jambo muhimu litakalo saidia taifa letu kupiga hatua ya kimaendeleo.

Jambo hili linahitaji nidhamu. Ni dhahiri watu wenye nidhamu wakimtuma mtu kwenda kuwawakilisha bungeni ni lazima mtu huyo atawaheshimu.

Kwasababu ametoka kwenye jamii yenye nidhamu. Jamii isiyochekelea rushwa na ufisadi kwa matendo. Jamii iliyoratibiwa na kupangiliwa, jamii inayojiheshimu, yenye nidhamu na utaratibu na inayoishi kwa ushirikiano ili kuleta maendeleo ya jamii nzima.

Kama nilivyosema awali serikali kazi yake ni kukusanya, kupanga na kulinda kile inachokijenga ili kiwe endelevu. Jambo la kujiuliza je hii nidhamu ilikuwepo kwenye jamii yetu na katika serikali yetu? Kama ilikuwepo na sasa inabomoka ni nini chanzo chake? Na kama pia ilikuwepo ilikuwepo kwa kiwango gani?

Kitu ninachoona tuna mahitaji makubwa ya kutengeneza nidhamu katika taifa letu. Nidhamu hii ni lazima ijengwe kwa jicho la lenzi ili kuleta taifa letu katika mpangilio na katika uwajibikaji.

Kuna mahitaji makubwa ya kuwajenga watoto wetu katika nidhamu na katika wajibu. Ni lazima watambue wanawajibu kwa taifa. Wazazi wawafundishe watoto wao wajibu huu muhimu. Ili taifa hili liendelee kuwepo ni lazima nidhamu ijengwe. Ni lazima tuwajenge watoto wetu kujitambua wao ni kina nani na wanawajibu gani kwa taifa.

Kama wazazi wakishindwa kuwatawala watoto wao itakuwa vigumu sana kwa serikali kutawala nchi. Ni lazima wazazi wawalee watoto wao katika nidhamu ni lazima wawatiishe. Nchi haiwezi kuzalisha chochote bila nidhamu na uwajibikaji. Ni lazima tufanye kazi kama kitu kimoja ili taifa hili liendelee. Matatizo tunayoyaona sasa hivi yanatokana na uzembe unaofanyika katika ngazi za chini wa kutokutimiza wajibu katika malezi.

Baadae yeyote ile ya taifa lolote lile itategemea sana nidhamu, uwajibikaji na elimu ya vijana wake. Na kazi hii ni ya kizazi baada ya kizazi, ni kazi ya kila siku ya ujenzi wa taifa. Huu muunganiko wa sehemu hizi ndogo unaounda taifa utakapo fanya kazi vizuri katika utengamano ndio utakaopelekea taifa hili kuendelea. Familia ndio zinazounda jamii na nchi, uhusiano huu kati ya familia na jamii pamoja na taifa kwa ujumla kama ukiwa wenye dhamira na malengo mamoja utafanya taifa hili kuendelea. Kila kimoja wapo kikitambua uwepo wa mwenzake na umuhimu wake katika kujenga taifa imara. Na serikali ikiwa kama nyenzo ya kuleta maendeleo ya pamoja.

Ikiwa sehemu hata moja ya uhusiano wa sehemu hizi ukibomoka ni vigumu kwa taifa kuendelea. Huu ni mtandao ambao ni lazima ufanye kazi kwa pamoja. Ni lazima kuwe na mipaka kati ya maslahi binafsi na yale ya taifa yanayo tuunganisha kwa pamoja kama taifa.

Bila nidhamu hatutaweza kujenga taasisi yeyote ikaimarika na ikaleta tija. Ni lazima tujiangalie upya na hili linahitaji nguvu kwasababu sio jambo la mchezo. Bila hilo taifa hili halitoweza kuendelea. Na hiki ni chanzo kikubwa cha kutokuendelea kwetu kama taifa.

Serikali yeyote duniani hutengeneza nchi na raia wanaofanana na asili ya serikali yenyewe. Serikali isiyo na nidhamu itatengeneza raia wasio na nidhamu. Na kinyume chake ni sahihi. Kwahiyo tabia ya nchi inategemea sana tabia za viongozi wake. Kwa sababu raia wanaangalia viongozi kama mfano. Mzabibu utazaa zabibu kamwe hauwezi kuzaa mapera. Kiongozi mwovu hawezi kuzaa raia wema. Nchi bora hujengwa na viongozi bora. Ni lazima tujenge tabia ya nchi.

Hatuwezi kujenga taasisi yeyote ikaendelea bila kuwa na nidhamu. Tusijidanganye. Wito wangu mimi ni kutaka mabadiliko katika taifa hili. Mabadiliko ya jinsi tunavyofikiri. Ni kutaka kuleta mwamko juu ya masuala ya kimsingi yanayohusu taifa hili. Kwasababu bila uelewa huu hatutaweza kulijenga taifa hili.

Uhusiano wa serikali na raia au wananchi ni lazima uwepo katika wajibu. Raia lazima waione serikali kama mtetezi wao na kama baba yao. Na si kama adui. Hapo ndipo upendo wa wananchi kwa serikali utakapo kuwepo. Ikiwa watu wa serikalini wataona kuwepo serikalini ni njia ya kujitajirisha badala ya kutumikia wananchi ni lazima chuki itakuwepo itakayotokana na hali ya wananchi kuwa duni na ile ya viongozi wao kuwa yenye utajiri na hii italeta matabaka.

Kwa serikali kubadilisha mwelekeo wake wa asilia wa kusimamia haki na kuleta maendeleo na kwenda kwenye kujilimbikizia mali kwa viongozi, mali inayotokana na ufisadi ni hatua ya kwanza ya serikali hiyo kuwa ya kibwanyenye na ya kigandamizaji.

Wataendelea kuridhisha tamaa zao na kukandamiza haki za raia na katika mazingira hayo ni lazima chuki itajengeka kati ya wanaotawala na wanaotawaliwa. Na jamii itavurugika na kuwa ya waovu na watu wabinafsi. Kutokana na serikali kutokujali raia.

Serikali inaposahau majukumu yake na kuendeleza anasa ni hatari kwa nchi. Haki haitetendeka. Wakati watu wakifa njaa na wengine kukosa madawa katika hospitali serikali za namna hii hutumia pesa ovyo katika mambo yasiyo na msingi, mambo ya kustarehesha nafsi. Serikali ya namna hii haiwezi

kujali raia hata kidogo ni lazima kwanza ijiangalie yenyewe kabla ya raia.

Ni lazima tubadili mwelekeo huu wa fikra kwasababu sio fikra sahihi na zenye tija kwa taifa. Ni lazima tujenge taifa lenye upendo na matumaini kwa wote.

SURA YA 2

ELIMU

Kuendelea kwa taifa lolote hutegemea sana nguvu kazi iliyo nayo na elimu mahsusi kuleta maendeleo jamii inayo yahitaji kwa ujumla ili kufanya taifa liendelee.

Misingi ya elimu hii lazima ijengwe katika kuendeleza taifa na si vinginevyo. Ni lazima ijengwe katika misingi ya uzalendo na wajibu. Jamii au taifa linapofundisha mtu si kwaajili yake tu, bali ni kwaajili ya taifa, ni kwaajili ya maendeleo ya wote. Ni kwaajili ya watu wote wapate uelewa utakaosaidia katika ujenzi wa taifa hili.

Watu wote watakapopata uelewa ndipo ukombozi wa kweli utakapopatikana. Uelewa huu ni muhimu kwa ukuaji wa taifa. Kuishi katika ujinga ni sawasawa na

kuishi katika kiza kinene, ni elimu pekee itakayotutoa katika kiza hiki.

Na elimu hii ni lazima iende kwa watu wengi zaidi ili wapate kujielewa. Kwakuwa pasipo kujielewa huku hatutaweza kujenga taifa hili. Ni lazima tujielewe sisi ni watu wamoja na elimu yetu tunayotoa kwa watu wetu ni maalum kwaajili ya ujenzi wa taifa hili na ni kwaajili ya ukombozi kwa watu wetu dhidi ya ujinga. Na sio kwa mtu binafsi tu. Hivi ndivyo tutakavyo jenga taifa kwa kujitolea. Tukitaka kujenga jamii yenye furaha ni lazima tufanye mambo haya. Bila ukombozi huu dhidi ya ujinga kwa watu wetu wengi zaidi hatutaweza kuandelea wala kuondoa uhalifu nchini.

Tukiwa na fikra hizi zitatufanya tujenge shule bora zaidi na kujitolea zaidi. Kwakuwa tutajenga shule si kwaajili ya faida ya mtu binafsi, bali kwaajili ya faida ya taifa. Sisi kama taifa tuna kitu tunataka tukijenge kuna sehemu tunataka kufika, hatutafika huko kama hatutakuwa wamoja. Elimu hii sio kwasababu ya ajira ni kwaajili ya kuongeza ufahamu wa watu wetu ili waelimke kutokana na ujinga, ambao ni hatari sana kwa maisha na maendeleo ya taifa. Wakiisha elimika vya kutosha na kujua malengo ya taifa lao na wajibu wao, juu ya malengo hayo, tutakuwa tumepiga hatua moja kubwa. Ni muhimu kujenga huku kujitambua kwetu. Tukiisha jitambua kama taifa mambo mengi yatakuwa marahisi.

Tukitoa elimu bora serikali itaepuka mambo mengi kwakuwa tutajenga raia wawajibikaji na wanaojitambua kwa taifa lao. Ni lazima tujenge roho hii ya uzalendo miongoni mwa watu wetu. Ni lazima elimu yetu imwezeshe kijana kuwa na fikra sahihi kwa kujenga nidhamu yake ili awe mwenye kufanya maamuzi sahihi kwa taifa lake. Na kumjenga kuwa

kijana mwenye dira. Tusipojenga raia wawajibikaji katika kiwango cha juu na wanaojitambua bado hatutaweza kupiga hatua muhimu kama taifa.

Nidhamu hii ni muhimu. Shule ni sehemu ambayo binadamu hutafuta maarifa ambayo yatamwezesha kuishi vizuri na kwa utaratibu. Sio tu sehemu itakayo mtayarisha kupata maarifa ya kazi peke yake, bali sehemu itakayo jenga tabia yake kwa jamii na taifa.

Elimu bila nidhamu ni sawasawa na mto bila kingo haina faida yeyote. Misingi ya elimu yetu lazima ilale hapo. Kwenye kutumikia watu na kwenye nidhamu. Malengo ya elimu yetu ni lazima yawe wazi kwa watu wetu wote. Malengo ya elimu ni maendeleo. Tunaelimisha watu ili wachangie katika maendeleo ya taifa lao. Watumie ujuzi wao na ufahamu wao kwa maendeleo ya nchi yao. Hili ndilo linalopaswa kuwa lengo kuu la elimu yetu. Maendeleo ya taifa letu. Kwahiyo ni muhimu kuelimisha watu wetu kulingana na dira ya taifa letu. Kama taifa ni muhimu kujua wapi tunataka kwenda na tuelimishe watu kulingana na huko tunakotaka kwenda. Maendeleo yetu yanategemea sana ubora wa elimu yetu pamoja na uzalendo na uaminifu wa watu tunaozalisha. Lengo la maarifa ni maendeleo, na watu wanasoma ili waendelee. Wajenge nchi yao na jamii zao kuwa bora. Hakuna maendeleo pasipo elimu. Tunasoma pia ili tuhudumie watu wengine.

Na kwa kila mfanyakazi lazima kuwe na ujira. Mshahara ni malipo ya kazi iliyofanyika. Na kazi ndio maendeleo yenyewe hakuna maendeleo pasipo kufanya kazi. Na ni lazima tuwe na elimu na ufahamu wa kile tunachofanya.

Kwahiyo tunasoma ili pia tupate ajira. Na ajira itasaidia taifa letu kusonga mbele. Kila mtu hupata

ajira kulingana na utaalamu wake, hivyo hulisaidia taifa kwenye Nyanja aliyosomea. Watu wasiokuwa na maarifa na utaalamu hulazimika kuwa vibarua na husimamiwa na watu wenye utaalamu. Lakini wote vibarua na wenye utaalamu hufanya kazi kufikia lengo moja.

Kama vile mtaalamu wa ujenzi na vibarua wake wanavyofanya kazi kufikia lengo moja ambalo ni ghorofa kama wanajenga ghorofa. Na ubora wa kazi huonekana katika lile lengo lililofikiwa. Kwahiyo kama mambo tunayofanya kutokana na elimu tuliyopata, hayana ubora unaotakiwa na hatuendelei kama tunavyopaswa tunapaswa kuangalia upya kwenye elimu yetu.

Kwakuwa lengo la elimu linapaswa pia kutufanya kujitegemea. Kuwa na ujuzi wa kuzalisha na kutumia vitu ambavyo tumetengeneza kwa mikono yetu wenyewe. Kutokuwa na uwezo huo ni kupungukiwa na maarifa.

Kwa watu kutokuwa na ajira ni matumizi mabaya ya nguvu kazi. Kwasababu ili taifa liendelee lazima liwe na ardhi lakini liwe na watu. Na watu lazima watumie nguvu zao na akili zao katika kuleta mabadiliko. Kwahiyo ni muhimu kujua ni jinsi gani tunatumia watu wetu tulionao kuleta mabadiliko. Kwa nchi yetu tuna mambo mengi ya kufanya ambayo hayawezi kumwacha mtu bila ajira kama tutatumia akili zetu na nguvu zetu vizuri.

Misingi yetu ya sasa ya elimu ni katika kutafuta kazi, ni elimu ya kutaka kuajiliwa, na sio katika msingi wa kujielimisha, na kutafuta maarifa ambayo yatatumika kwa faida ya ujumla kwa taifa.

Sio katika kukuza ufahamu, mawazo yetu yameelekea kwenye ajira. Lakini kukuza ufahamu ndio jambo muhimu na la msingi. Tukiisha kuza ufahamu wa watu wetu kwa kiwango kikubwa haya mambo mengine yatafuata.

Na Tutaweza kumtengeneza mtu anayefikiri na kutenda kwa kujitegemea, mwenye maadili, dira na mwenye kujitambua. Mtu asiyeyumbishwa na upepo, anayefikiri kwa kujitegemea, lakini pia mtu anayewajibika kwa matendo yake. Kwasababu tunahitaji watu wanaojitambua, na wanaofikiri kwa kujitegemea, ambao kwa matendo yao ya kujitambua watafanya taifa hili kuendelea.

Hawa watu wenye misimamo na wanaojitambua, na wenye uwezo bora wa kufikiri ndio tunaowahitaji. Watu hawa wenye nguvu za kiakili, kimaadili na kiroho, wenye uwezo wa kuleta watu pamoja kwenye lengo moja ndio tunaowahitaji kwa sasa. Wenye uwezo wa kuvunja mgawanyiko uliopo sasa wa kimaslahi, na kichama na kuleta watanzania wote kuwa kitu kimoja. Kwasababu ni kwa njia hii pekee Tanzania itakuwa nguvu isiyoshikika.

Kama wote tukiungana kwa mawazo na akili zetu kuwa kitu kimoja. Hili ni lazima liwe lengo la kila mzalendo wa kweli.

Na ni wajibu wetu pia kutafuta ufahamu kwakuwa pasipo kutafuta ufahamu kama nilivyosema mwanzo, taifa letu halitoweza kuendelea. Tutaendelea ikiwa tu tutatumia nguvu zetu zote na dhamira yetu yote kutafuta ufahamu. Ni muhimu tukajielimisha na kufanya tabia yetu ya kila siku kutafuta maarifa yatakayofanya taifa letu kuendelea.

Kujielimisha ni kutafuta ufahamu ambao utakufanya uishi vizuri. Mbali na stadi za kazi raia wetu ni lazima wawe wameelimika. Tuna elimu ya utafutaji hela lakini sio elimu ya kutafuta jinsi ya kuishi.

Kuwekeza elimu yetu katika stadi za kazi peke yake, zitakazo pelekea watu wetu kupata ajira na fedha za kujikimu sio sahihi, ni lazima elimu yetu iende mbali zaidi katika kumfunza kijana kuishi katika jamii na katika taifa, kwakuwa bila uhusiano miongoni mwetu itakuwa vigumu sana kulijenga taifa hili. Kwasababu naamini amani yetu itategemea sana nidhamu ya watu wetu na mahusiano yao.

Lakini pia siamini kama kuachia taasisi kama polisi na mahakama, kushinikiza tabia na mienendo ya watu wetu inatosha. Tungehitaji raia wanaojiongoza wenyewe kutenda yanayostahili kutokana na ufahamu wao. Ingawaje vyombo hivi ni muhimu katika kurekebisha tabia za watu wetu ili kujenga jamii bora na zenye amani.

Vijana wetu wakiwa na mtazamo huu hawatapenda elimu, itakuwa ngumu na mzigo kwao, na watatumia nguvu nyingi katika kuelewa, elimu yetu itajawa na uwoga na hofu ya kufeli na ya maisha. Ni muhimu kuwaondolea hofu hii vijana kwa kuangalia upya misingi na mazingira ya elimu yetu.

Tunapenda watu wetu wawe na ufahamu na wawe huru. Waweze kujua yaliyo sahihi kwao. Waweze kujenga familia zao katika ubora, na wawe wenye manufaa kwa jamii na kwa taifa. Tunapenda watu wetu wawe kwa asilia wenye kupenda maarifa, ni lazima tujenge tabia hii na ni lazima tuondoe fikra hizi zilizojengeka kwa miaka mingi mongoni mwetu. Tukifanikiwa tutajenga jamii bora na yenye uwajibikaji.

Ni lazima wafundishwe kulithamini na kulipenda taifa lao na ya kwamba wanapewa elimu ili waweze kuliendesha taifa hili katika ubora. Ni muhimu kutambua ya kwamba binadamu anapata faida kubwa anapoishi na jamii nje ya jamii maisha ya binadamu yasingekuwa kama yalivyo sasa.

Tuna wajibu wa kujenga jamii zetu na familia zetu lakini pasipo elimu bora hatutaweza vyote hivi. Ni lazima tujenge familia zetu na jamii zetu katika nidhamu na katika utaratibu.

Elimu yetu pia lazima ilenge kukuza fikra na uelewa wa watu wetu. Na sio tu kumwingizia maarifa kichwani, imfanye aweze kufikiri na kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia ubongo wake na sio kuelekeza tu, bali kukuza ufahamu na wala sio kukariri. Aweze kufikiri mwenyewe na kuamua yaliyo sahihi.

Elimu hii itamfanya kuwa huru zaidi na bila elimu ya namna hii hatutaweza kujenga nchi ya kidemokrasia. Kwasababu demokrasia inahitaji uelewa wa watu katika kufanya maamuzi sahihi kwa manufaa ya nchi.

Kwasababu demokrasia inawataka wananchi kujiamulia mambo yao wenyewe kwa faida yao wenyewe na hii inahitaji elimu. Bila elimu na hatutaweza kujenga demokrasia.

Ni baba anayejua kilicho bora kwa mtoto wake lakini mtoto atakapokua na kupata uelewa hujua anachohitaji. Ni lazima elimu yetu iwafanye watu wetu wapate uelewa huu. Ni muhimu sana kama tunataka kujenga taifa la kidemokrasia ambalo pia huhitaji nidhamu ya hali ya juu. Ni lazima tujenge watu wetu katika fikra sahihi.

Kwahiyo elimu ni mafunzo yahusianayo na nguvu za kiakili, yaani kuendeleza akili na maadili, kwa kusoma na nidhamu, ili kumfanya binadamu kutenda katika usahihi. Elimu hii ni lazima iunganishwe na maarifa ya kazi bila hivyo elimu yetu itakuwa haijakamilika.

Kwahiyo mtu aliye elimika tutampima katika matendo yake. Ina niwia vigumu kuamini na kutia akilini mtu asiye kuwa mwaminifu na mwizi kuwa ameelimika. Tutamuona mtu aliyeelimika anavyoendesha familia yake na anavyoishi na jamii inayomzunguka. Tutampima katika nidhamu yake. Elimu bila nidhamu ni maarifa tu. Haina faida yeyote.

Haiwezi kujenga kitu chochote endelevu. Elimu bila nidhamu ni sawa sawa na mto bila kingo. Mto bila kingo hukosa mwelekeo na huleta uharibifu. Kipimo cha mtu aliyeenda shule ni nidhamu. Ni jinsi gani navyotumika katika jamii kuleta mabadiliko, nidhamu hii ndio inayomwelekeza kutenda yaliyosahihi kwa kujizuia ili awe wa manufaa kwa jamii na kwa taifa. Bila nidhamu hii mtu binafsi hana mwelekeo hata taifa halina mwelekeo bila nidhamu.

Kama madhumuni ya elimu ni kumuongezea uelewa na maarifa binadamu na kumfanya kujitambua, kutambua mazingira yake, kutengeneza tabia yake na mahusiano yake na jamii, kumfanya awe na nidhamu na awe mwenye faida kwa umma na kwa jamii, bado kwa kiwango kikubwa hatujafanikiwa katika dhamira hii, kwakuwa dhumuni la kuwa na taifa sio tu ni kupata faida za kimali, bali pia kujenga mahusiano yetu na mashirikiano yetu kama binadamu.

Na huu ndio msingi wa jamii yenye furaha. Jamii ambayo inahangaika kwenye kutafuta mali tu bila pia

kujenga misingi ya mahusiano yao, kamwe haitoweza kuwa na furaha. Kwasababu pesa itakuwa ndio msingi wa maisha yao na uhusiano wao utakuwa duni. Jambo la mahusiano katika jamii ni jambo la muhimu sana ndilo lililo tuleta pamoja kama taifa na ili taifa hili liendelee mahusiano haya ni lazima yalindwe. Kama tunavyojua taifa letu ni la watu wa aina tofauti.

Wajibu wa kujenga nidhamu hii na maadili huanzia nyumbani na kuendelezwa shuleni, Na kuendelea kulindwa katika jamii. Jamii inapowajibika kwa pamoja katika malezi ya watoto, huimarika na taifa huwa na baadae nzuri, na vile vile kinyume chake.

Nidhamu hutokana na nguvu ya kiakili, nguvu inayoelekeza akili kufanya yaliyo sahihi na kuzuia mihemko, kuzuia hulka na kuachia fikra kutamalaki badala ya hisia. Tutaendelea tu kama taifa kama tutafanya maamuzi sahihi kwa wakati wote.

Hatutaweza kuongelea elimu bila kuongelea walimu. Wao ndio wanaofundisha watu wetu na kunyanyua uelewa na kukuza akili zao. Ni sehemu muhimu katika jamii. Ni watu ambao wanatakiwa kutumia muda wao mwingi kujielimisha na kuelimisha wengine. Na hili linatakiwa kuwa jukumu lao la kila siku.

Uelewa wa watu hawa unatakiwa uwe mkubwa kama nidhamu zao zinavyotakiwa kuwa. Ni sekta ambayo inatakiwa kuangaliwa kwa umakini kwakuwa maendeleo ya taifa lolote hutegemea sana uwekezaji katika elimu ya watu wao na kujitambua kwa watu, kwa taifa lao.

Katika sekta hii kumetokea kutokuridhika kukubwa kutokana na jinsi inavyoendeshwa na pengine mabadiliko yanahitajika ili kuleta maridhiano katika

jamii, suala la elimu sio la serikali ni la jamii, na ni la mwelekeo wa taifa.Kutokuridhika huku sio kwa walimu tu bali hata sekta nyingine.

Jamii ina haki ya kuamua walimu walipwe kiasi gani kulingana na majukumu yao na kulingana na mapato ya nchi. Jamii ina haki ya kuwalazimisha serikali iwalipe walimu stahili zao, kwakuwa wao ndio wanaoathirika, wao kama taifa. Serikali inawajibu wa kutumia maliasili vizuri na kutafuta vyanzo vya mapato ili kuendesha sekta za umma.

Inawajibika kudhibiti mapato na ufisadi ili kuhudumia wananchi. Maisha ya walimu ni lazima yasiwe ya shida. Ni lazima aishi maisha yenye nafuu yatakayo mwezesha kufundisha vyema.

Mwalimu mwenye njaa hawezi kufundisha vizuri. Ni kutokana na haki hizi watu hupenda mataifa yao. Ni lazima heshima ya mwalimu irudi. Ni lazima mwalimu aishi maisha yenye nafuu. Wakati serikali ikitimiza haki za walimu na walimu pia wawe tayari kutimiza wajibu.

Ni lazima serikali ipunguze matumizi yasiyo na msingi ile fedha ielekezwe kwenye mambo ya msingi kwa faida ya nchi. Kama elimu na afya.

Jukumu la kuinua hali za kiuchumi za walimu ni jukumu la lazima. Tunahitaji wao wafanye kazi yao. Ni lazima tu thamini walimu. Kwakuwa kama taifa hatutaweza kuendelea pasipo elimu. Ni lazima tujenge misingi imara kwa watoto wetu kwa kuwapa elimu iliyo bora. Baadae yetu imelala hapo. Kama walimu watakata tamaa watoto wetu hawatapata elimu iliyo bora.

Huu ni wito kwa watanzania wote ni lazima tuilazimishe serikali inyanyue hali za walimu nchini bila mzaha. Taifa hili litanyanyuka kama wote tutafanya kazi pamoja na kuidai serikali itimize wajibu. Hii ni kwa maendeleo yetu na baadae ya watoto wetu. Haki za walimu lazima ziangaliwe. Hatuna shida nyingine na serikali zaidi ya kuidai kutimiza wajibu wake. Ili kuleta maendeleo ya Watanzania.

Wazazi wa familia zinazounda taifa hili ni lazima waungane kudai elimu nzuri kwa watoto wao na pia kudai uwajibikaji wa serikali katika elimu ambayo ndio msingi wa jamii imara na endelevu. Ili kujenga jamii bora na taifa imara ni lazima kuwepo na kujitolea huko. Taifa hili litasonga mbele ikiwa tu kila mtu atajitolea kuona taifa hili likiendelea.

SURA YA 3

SIASA

Siasa ni nyenzo ya kujenga na kuendeleza nchi, msingi wake ni hoja, mawazo na fikra yakinifu. Siasa sio ulagahai. Siasa ni ujenzi. Siasa inahitaji akili iliyo pevuka. Inahitaji kuona hatua nyingi zaidi bila kiona mbali, bali kwa kutumia akili na uwezo wa ubongo kufikiri. Siasa ni mahusiano ya jamii. Mwanasiasa ni mtu anayeshughulika na mahusiano ya jamii. Siasa ina husiana na maendeleo ya watu.

Siasa hukusanya na kulinda kile ilichokusanya, siasa hujenga utaratibu. Kwa kutumia nguvu ya fikra na maneno ya mdomo siasa huimarisha msingi wa Taifa. Kuna mwana ‘‘si hasa’’ na mwanasiasa. Mwanasiasa hukusanya lakini mwana si hasa hutawanya. Mwanasiasa hujenga na mwana si hasa kazi yake kubomoa.

Mwanasiasa hutumia ukweli kuingia madarakani mwana si hasa hutumia ulaghai na uongo. Tabia mwana si hasa ni ulaghai. Hupenda anasa na kujinufaisha nafsi, hujiangalia mwenyewe kwanza kabla ya kuangalia jamii.

Asili ya mwanasiasa ni busara na hekima anajua anachokijenga. Huangalia maslahi ya jamii kabla ya kuangalia maslahi yake.

Turudi katika mada yetu ya ujenzi wa siasa imara katika taifa letu. Siasa itakayojengwa katika misingi ya wajibu na uzalendo. Siasa za watu waliopevuka na wanaojali mustakabali wa Taifa kuliko maslahi binafsi.

Ni jinsi gani tutajenga siasa zetu katika misingi imara na ya kuheshimiana? Hii yote itaturudisha nyuma tena katika misingi iliyojenga jamii zetu na familia zetu nidhamu na taratibu. Kwakuwa watu walioko

kwenye vyama wanatoka kwenye familia na katika jamii. Ubora wa vyama vyetu utategemea sana ubora wa familia na jamii kwa ujumla.

Ni muhimu kwahiyo tunapounda vyama vyetu ni lazima tuangalie nidhamu na misingi ya kuanzisha vyama vyenyewe. Msingi wa kuwepo chama chochote ni ujenzi wa jamii na sio kuingia madarakani kama lengo kuu. Chama cha siasa ni lazima kijue kinakwenda kufanya nini madarakani.

Ni lazima ijulikane mabadiliko ya wananchi ndio lengu kuu ya uwepo wa vyama vya siasa. Na vyama hivi ni lazima viwepo hai wakati wote na vishiriki katika ujenzi wa taifa.

Fikra hii ya kusema lengo la chama cha siasa ni kuingia madarakani tu sio sahihi. Chama cha siasa ni lazima kiwe na malengo mapana zaidi na kiwe hai wakati wote katika ujenzi wa taifa. Isiwe chama cha siasa kinapanga wakati wote ni jinsi gani ya kuingia madarakani kuliko jinsi kinavyopanga fikra za kuleta maendeleo.

Kije na hoja mbadala na fikra mbadala na kile chama kilichopo madarakani. Lazima kione udhaifu wa kile chama kilichopo madarakani, kuuongelea kwa faida ya Taifa. Chama chochote ni lazima kiingie madarakani kwa uzuri wake na sio kwa ubaya wa mpinzani wake. Kukosoa tu haitoshi, ni lazima chama cha upinzani kijengwe katika ubora na katika fikra zinazoonekana dhahiri zitakuwa mkombozi.

Sio tu kwasababu ya wananchi kuchoshwa na rushwa na kuchagua chama kingine mbadala kinachoonekana kukemea rushwa lakini hakionekani kuwa ni bora kwa nidhamu, maadili na sera.

Lakini ambacho kinaonekana kabisa hata kikiingia madarakani hakitafanya chochote kikubwa cha kuleta mabadiliko kwa watu na kwa taifa kwa ujumla. Ni sawa kumpa mtu vitu vibovu viwili na kumwambia achague chenye unafuu. Lakini ukweli ni kwamba vyote ni vibovu.

Chama tawala kina wajibu ya kulinda uhuru wa vyama vya upinzani wa kueneza fikra zao na kuzisambaza. Lakini fikra hizi ni lazima tuziangalie kwa mustakabali wa taifa.

Fikra za chuki ni mbegu mbaya katika taifa na mazao yake kila wakati huwa ni mabaya. Wanasiasa wanatakiwa kuwa makini kwa kila kitu wanachoongea.

Kila wanachoongea kitajenga au kubomoa. Tusibomoe nchi kwa faida binafsi na za muda mfupi na kuacha faida za muda mrefu za taifa.

Ni lazima tujenge taifa hili katika ukweli wa nafsi. Tuwe na matumaini ya kujenga jamii njema na taifa bora. Ni lazima tubadili mwelekeo wa fikra zetu.

Naogopa kutumia neno itikadi ni kali linaonekana kufuata hisia zaidi kuliko fikra. Ubora wa serikali yetu utategemea sana ubora wa vyama vyetu vya siasa na ubora wa serikali utatengeneza taifa bora.

Ni lazima tuendeshe siasa zetu katika misingi ya kuheshimiana. Tuweke akilini misingi bora ya vyama vyetu vya siasa ndio vinavyopelekea serikali bora.

Tuondoe hili suala la kuingia kwenye siasa kwa manufaa binafsi. Kila mtu apewe nafasi ya kuongoza kama ni kipaji chake na ana uwezo, ni lazima tujenge

mazingira ambayo kila mtu ataweza kushiriki katika uongozi wa kisiasa bila uoga.Bila kuogopa matusi ambayo yatamvunjia heshima yake. Kwahiyo tunahitaji Taifa hili lisonge mbele lakini bila vyama imara itakuwa ndoto.

Juhudi zetu ni lazima iwe kujenga vyama hivi katika misingi ya kidemokrasia. Ili kila mtu awe na uwanja mpana wa kushiriki katika uongozi wa nchi yake bila kuogopa.

Misingi mibovu ya kutokufuata sheria na taratibu hujenga kutokuaminiana miongoni mwa vyama vya siasa hasa kati ya wale walioko madarakani na wapinzani, ni lazima tuiondoe.

Ni lazima yajengwe mazingira mazuri ya ushindani. Ni lazima kuwepo na nidhamu katika uendeshaji wa shughuli za kisiasa. Ni lazima tutambue tunajenga taifa moja. Na mustakabali wetu kama taifa ni mmoja. Na kila mtu na kila chama kina haki ya kushika uongozi wa nchi. Ni lazima tujenge taifa letu katika misingi imara.

Kwa mazingira yaliyopo sasa hivi inaonekana kama kutoa serikali moja na kuiweka nyingine ni kama mtu anafanya mapinduzi inatumika nguvu kubwa chuki na mifarakano badala ya kujenga hoja. Unatumika ulaghai badala ya kusema ukweli.

Ni lazima ifike wakati vyama vyetu vikue na vitambue wajibu wake kwa taifa na kwa amani na mustakabali wa taifa letu. Hatutaweza kuendelea pasipo kujenga siasa bora na vyama imara vya kisiasa. Ni lazima tukue na tuwe wenye fikra sahihi na zinazoona mbali kwa faida ya kizazi kijacho.

Darubini yetu ni lazima iwe maendeleo ya watu wetu na mustakabali wetu kama taifa bila dira hii tutapotea. Ni lazima tufikirie kuhusu raia. Ni muhimu tukabadili mitazamo yetu. Kwanini unataka kwenda madarakani? kwanini unapambana? Kwanini unatukana hivi ni kweli ni kwasababu unataka kutumikia wananchi ndio maana unapambana, ndio maana unatukana na kudhalilisha wengine?

Hatutaweza kujenga taifa hili katika misingi hiyo ni muhimu na ni lazima taifa hili kujengwa katika misingi sahihi. Misingi ya kuheshimiana na wajibu.

Serikali inastahili heshima yake, lakini pia lazima iwajibike kwa wananchi ni kwa kuwajibika tu na kutenda haki, pamoja na kuzuia ufisadi ndipo itakapo heshimika kwenye macho ya raia.

Kuhakikisha raia wanapata huduma wanazo stahili kama raia. Kazi ya ujenzi wa taifa hili ni yetu sote. Taifa hili litarekebika pale tu, tutakaposema makosa yake bila kufumbia macho.

Lengo letu ni lazima liwe kujenga taifa la haki. Ni kwa kujenga taifa la haki tu ndio raia ataheshimika na kulipenda taifa lake. Taifa ambalo haki za raia zinavunjwa raia hawataweza kulipenda, watajitenga nalo watajihisi sio wamiliki.

Lengo hili tutalifikia kama tukijenga vyama imara vinavyozingatia haki na ukweli. Na sifikirii kama kuna lengo kubwa kama hili la kujenga Taifa la haki. Kwakuwa furaha yetu itategemea sana jinsi tunavyotendeana haki.

Ni wakati sasa wa kusema ukweli na kujenga taifa hili katika ukweli. Ni wakati wa kuzungumza mambo

yanayohusu taifa hili kiutu uzima na kama watu tuliokomaa kiakili.

Tukitambua mustakabali wa taifa hili wa kesho unategemea na maamuzi tunayofanya sasa. Ni lazima tufanye maamuzi katika fikra sahihi bila msukumo wa faida za kisiasa na bila kuangalia uchama bali kuangalia maslahi ya Taifa na baadae yetu.

Busara ni kufanya maamuzi sahihi, na hekima ni kuona mbali na kuepuka hatari inayotukabili kutokana na vitendo vyetu vya sasa, hekima ni tabia ya kila siku ni jinsi mtu anavyoishi sahihi.

Ni busara kujenga baadae ya watoto wetu iliyo nzuri na ni hekima pia. Wote sisi tuna haki miliki katika taifa hili na tuna wajibu wa kujenga taifa bora na imara.

Tabia za udini na mgawanyiko wa kiasiasa sio sahihi kwa mustakabali wa taifa hili. Ubinafsi hautatupeleka mbele kama taifa. Umoja katika jitihada utalinyanyua taifa hili.

Ni lazima tujenge taifa ambalo mmoja akianguka mwingine ana mnyanyua. Hii ni roho ambayo italifanya taifa hili liwe kubwa. Kufanya kazi kwa bidii kwajili ya taifa na kwajili ya baadae yetu. Ni lazima tujenge uzalendo na uwajibikaji. Ni lazima tujenge kuaminiana, hatutafanya kazi pamoja pasipo kuaminiana.

Kwa miaka mingi busara amekuwa mjenzi, mlinzi na muongozaji wa mataifa. Pale busara inapotoweka baadae ya mataifa huwa matatani.

Mwenge wa busara uwake na uangaze kila kona ya nchi hii, umulike sehemu zenye kiza na uangaze, ulete

matumaini pasipo na matumaini, hulete furaha na ari ya ujenzi wa taifa hili kwa watu wetu wote.

Kwa jitihada zetu pekee na maarifa tutalinyanyua taifa. Tujenge upya roho ya utaifa wetu. kwa maamuzi yetu tutalifanya taifa hili kuwa kubwa au dogo, kuwa lenye amani au fujo.

Tujenge baadae ya watoto wetu pamoja tufanye huu uwe mwelekeo wetu. Huu ni ujumbe kwa viongozi wote wa kisiasa tuna kazi ya kufanya kwa taifa, ni wakati sasa wa kujivua unafiki na kuvaa ujasiri na kuonyesha kwamba kwa pamoja tunaweza. Na panapokuwepo matumaini kuna njia.

Tuchague busara na hekima kuwa dira na mwongozo wetu kama wimbo wetu wa taifa unavyosema basi tuakize wimbo huu unaotusisitiza busara na hekima katika ujenzi wa taifa letu, Na katika maamuzi yetu. Bila woga ni lazima tujenge taifa hili.

SURA YA 5

UTAMADUNI

Taifa lisilo na utamaduni linakosa utambulisho wake, utamaduni ni kiini cha utaifa.

Taifa lazima liwe na utamaduni wake, utakaotofautisha kati ya taifa moja na jingine, na sio ngozi ya watu wanaoishi katika taifa hilo pekee, ngozi ni jambo mojawapo lakini lazima iwe zaidi ya hapo.Taifa lisilokuwa na utamaduni wake ni taifa mfu.

Ni taifa ambalo halijajitawala bado. Utamaduni ndio unaotofautisha taifa moja na jingine. Lakini utamaduni pia hujengwa na imani na matendo ya mara kwa mara yatakonayo na imani hiyo. Utamaduni sio ngoma au sanaa pekee yake, pengine tunavyodhani. Utamaduni ni vitu vyote ambavyo vimezalishwa na vimekuwa dhahiri machoni kwetu kwa nguvu za kiakili za watu wa mataifa husika, vitu ambavyo vimejenga maisha yao.

Ni jinsi watu wanavyofikiri, kutenda na kuamini. Ni muelekeo wa fikra na itikadi wa jamii husika. Itikadi hizo na fikra ndizo zinazoongoza maisha yao ya kila siku. Kwahiyo taifa lisilo kuwa na mizizi kwenye utamaduni wake, ni taifa ambalo halijitambui, linapeperushwa na kila upepo kwasababu halina itikadi.

Taifa lazima lijenge na lilinde utamaduni wake. Ni lazima lijue ni nini linasimamia na ni wapi linataka kuelekea. Kama Taifa, ni picha basi utamaduni ni rangi. Taifa lisilo kuwa na mizizi kwenye utamaduni wake ni taifa lisilo kuwa na itikadi ambalo huyumbishwa na kila upepo.

Ni lazima tujitambue na kushikilia pamoja na kuthamini kilicho chetu. Tukikubali kushawishika na tamaduni za mataifa ya nje tutakuwa rahisi kutawaliwa, tusikubali ni lazima tujijenge. Tusikubali ushawishi wowote.

Sisi kama watanzania tuna staha zetu na jinsi tunavyoona mambo. Tusikubali taifa lolote kutuletea mambo yeyote tunayaona hayana faida kwetu. Ni lazima tulinde heshima yetu na utambulisho wetu ikiwepo lugha yetu ya Kiswahili. Ni lazima tukiheshimu. Ni muhimu sana jambo hili. Ni jambo la utaifa.

Ni muhimu pia kutunza maadili yetu na kuzuia ushawishi ambao utabomoa maadili yetu na staha. Ni lazima tujenge jamii ya wafikiriaji na kuamua mambo yetu kwa kutumia fikra zetu wenyewe. Kwakuwa sisi ndio tunajua tunachohitaji. Ni lazima tupange mipango yetu wenyewe na kuitekeleza wenyewe ni lazima tulinde uhuru wetu.

Uhuru na umoja ni nembo ya Taifa letu tusipoteze uhuru huu. Ambao baba yetu wa taifa aliupigania, pamoja na wazee wetu wengine. Hili ni jukumu tulilonalo sisi wa kizazi hiki. Kunyanyua taifa hili kutoka hapa lilipo kulifikisha mbali zaidi.

Hatutafanikiwa kama hatutakuwa wamoja na wazalendo. Ni lazima turudishe akili zetu kwenye taifa hili. Ni lazima tulipende taifa hili. Huu ni wajibu wetu wa dhati.

Upepo wa kisulisuli umechukua vijana wetu, upepo wa kimagharibi na kuwafanya wasahau taifa lao na kutukuza mataifa mengine. Wamesahau wajibu wao kwa taifa lao. Tunapaswa kurudisha akili za watu wetu ndani ya nchi yetu ili waweke akili zao hapo zote kulijenga.

Ili kulijenga taifa hili ni lazima tulipende.Hatua ya kwanza ya maendeleo ya taifa hili ni pale tutakapoamua kulipenda, tutakapoamua kuhamisha akili zetu kutoka katika ubinafsi kuja katika utaifa.

Tunaweza kuwafanya watu wetu kuwa bora na nyota wanaong'aa ulimwenguni ni jitihada zetu, umoja wetu na uzalendo wetu. Tunaweza kulisukuma taifa hili mbele.

Tunahitaji kubadilisha fikra zetu, hatutaweza kuendelea kwa fikra hizi tulizo nazo sasa ni lazima tubadilishe mioyo yetu na tujenge taifa jema na lenye misingi mizuri ya ki utamaduni na watu wenye uhuru. Ni lazima tutilie maanani zile tabia nzuri ambazo zitafanya taifa letu kuwa bora na endelevu. Ngoma zetu, miziki yetu, sanaa zetu zingine ni lazima zijengwe katika nidhamu na maadili ili kuilinda jamii.

Ni lazima zilenge katika kumuongezea maarifa na ufahamu na burudani kidogo. Ni muhimu sanaa zetu kutohamasisha vitendo viovu na hatari kwa jamii. Kama ngono, uvutaji bhangi na mambo mengine maovu ambayo yatawafanya vijana kukengeuka kwakuwa tunajua fika hatutaweza kuwajenga vijana katika misingi hiyo taifa letu likaendelea.

Lazima sanaa zetu zihamasishe utendaji mema na uzalendo kwa taifa. Sanaa ina umuhimu mkubwa sana katika ujenzi wa taifa imara. Sanaa hizi huburudisha katika sherehe mbalimbali na kufurahisha roho.

Ni lazima tulilinde taifa hili kwa njia yeyote na kwa gharama yeyote ikiwemo kutumia sanaa ili kujenga tabia na nidhamu za watu badala ya kuzibomoa. Ni lazima nyimbo zote zichunguzwe ujumbe uliomo kwenye nyimbo hizo kama una faida kwa taifa ama la vile vile katika filamu lengo ni kulinda jamii na uharibifu. Kwa njia hii pekee tutaweza kuwafanya vijana wetu na watoto kuwa na nidhamu. Na kuwafanya waishi kwenye mazingira mazuri yasiyo na madhara kwao.

Ni muhimu pia kutumia sanaa katika kujenga uzalendo wa vijana wetu kwa taifa, njia ambayo itakuwa bora sana katika ujenzi wa taifa hili kwakuwa wakati ikiwaburudisha itakuwa pia ikiamsha hisia za uzalendo kwa taifa lao. Itajenga moyo wa kulitumikia na kujitolea kwa taifa lao.

Mtakumbuka bendi zetu nyingi zilishiriki katika mapambano ya kuhamasisha ukombozi wa nchi nyingi za kusini mwa Afrika. Hata pale nchi yetu ilipokuwa ikipambana na nduli Idd Amin, nyimbo hizi zilituika kwenye uhamasishaji. Tusiishe kuwatumia tu katika uchaguzi bali kwenye malengo yenye faida zaidi kama yale ya uhamasishaji wa uzalendo na kuwajengea ujasiri watoto wetu kwa kuandika nyimbo na filamu za aina hizo, ambazo zitawavutia watu wengi na kuwajengea uzalendo kwa taifa.

Mambo haya ni ya muhimu sana katika ujenzi wa taifa letu hili ambalo tumaini letu lazima lilale. Mtu lazima aheshimiwe kutokana na mchango wake katika jamii kutokana na jinsi alivyosababisha taifa lake lisonge mbele.

Kuna mambo mengine mengi sana ambayo yatasaidia kufanya taifa hili lisonge mbele ikiwa tutajipanga ikiwepo suala la uandishi wa habari na vitabu. Ambavyo vitatumika kumwingizia tabia fulani mototo ambazo zitakuwa na manufaa kwa taifa. Ambazo zitamjenga mtoto katika maadili na katika nidhamu.

Binadamu ni anavyoona na anavyosikia, vitu hivi ndivyo vinavyojenga tabia ya mtu kwa asilimia kubwa kuliko anavyofikiri makini. Haya mambo ni muhimu kwa ulinzi na nidhamu. Hasa katika umri mdogo ili kulinda maadili ni lazima tuwe ya Taifa. Ni muhimu kutoachia kila kitu ni lazima tuwe na udhibiti. Ili

kujenga tabia za watu wetu na tunajua kwamba tusipo dhibiti tabia za vijana wetu leo tutakuwa tumechelewa na baadae ya taifa hili itakuwa kwenye hatari.

Nidhamu itatoweka na nidhamu ikitoweka kutakuwa na vurugu na fujo. Tusiache haya mambo yajiendee ni lazima tuyadhibiti. Hatutaweza kujenga familia bora, baba bora na mama bora kama hatuta thibiti tabia za vijana wetu na kuangalia kwa makini elimu yao.

Vyombo vyetu vyote vya habari ni lazima vijengwe katika misingi uzalendo na nidhamu. Uhuru huu wa kuachia kila kitu sio uhuru. Ni lazima kuwe na udhibiti. Ili tujenge jamii bora na endelevu. Hii sio kazi ya kanisa peke yake wala msikiti ni kazi ya wapenda mema wote. Kwa wote wanaoitakia mema Tanzania na kwa wote wanaojua ukweli na kuamini.

Kwa tabia ninazoona sasa kwenye vyombo vya magharibi kama tusipojitayarisha sasa na kujilinda dhidi ya uharibifu wa tabia za kimagharibi jamii yetu itamezwa na maadili yake yatapotea. Vitendo vya kishoga vinavyohamasishwa huko huenda vikaja kuwa na madhara kwetu na jamii yetu kama hatuta kuwa na uthibiti kila hali hiyo itakapo tokea na kama hatuta thibiti tabia za watu wetu tutajikuta kwenye madhara makubwa.

Ni muhimu taifa hili kuandika na kuhifadhi historia yake. Ni muhimu kwakuwa hii inatukumbusha tuliko toka. Ni ukweli usiopingika kama kizazi kisipojua kilipotoka hakitajua kinapoelekea ni lazima watoto wetu wafundishwe historia ya taifa.

Ili wajue hali ilivyokuwepo wakati uliopita na hali ya sasa. Ni muhimu kujua hili kwakuwa linawajengea kujua wanapoelekea na kufahamu kama jamii inatengemaa au inaharibika.

Kizazi kipya ni lazima kijue yaliyopita. Ni muhimu kuweka rekodi ya historia yetu hata kama sio nzuri sana na ya kujivunia. Tunaweza kujifunza makosa yetu kutokana na yale yaliyotendeka nyuma na kujenga taifa letu upya katika dira na mtazamo tofauti.

SURA YA 6

TAIFA KAMA MTI

Taifa hili ni kama mti ambao unatakiwa uanze ukiwa mdogo kutokana na mbegu iliyopandwa na kukua kisha kutoa matawi ambayo yataleta matunda. Ni muhimu watu wa Taifa hili kufahamu Taifa hili sio tawi la nchi yeyote ile. Taifa hili ni mche ambao lazima ukue ili utoe matawi na matunda.

Mti huu lazima ukue kutoka ndani yake wenyewe na upeleleke matawi yake sehemu nyingine. Hili ni muhimu sana kwa ukuaji wetu na ustawi wa dunia. Je mbegu hii ni mbegu gani? Pengine tungependa kujiuliza ambayo itaota na kuwa kubwa na matawi yake kwenda sehemu nyingine?

Mbegu hii ni tabia ambazo tutapanda kwa watu wetu. Fikra ambazo tutawajengea watu wetu. Huu ndio utakao kuwa msingi imara utakaojenga taifa hili. Ni muhimu kutambua ubora wa taifa lolote lile unategemea sana ubora wa fikra za watu wa taifa hilo.

Tutapanda mbegu njema ambazo nina uhakika zitaleta mabadiliko katika dunia nzima. Tunataka kujenga taifa lenye misingi ya haki. Tunataka kujenga taifa litakalo ongozwa na busara na hekima.

Tunataka kujenga taifa litakalo pelekea mabadiliko katika dunia nzima na kujenga jamii ya watenda haki na inayowajibika katika ubinadamu.

Tunataka kujenga taifa litakalopelekea amani ya dunia kupatikana. Tunataka kuwa mfano kwa mataifa mengine kuiga kama maji ya mto yafuatavyo mkondo wake. Kwahiyo Taifa letu ni lazima liwe kama mti mchanga utakao kua na matawi yake kusambaa sehemu nyingine, utakao zaa matunda kwa faida ya ulimwengu wote. Mti mwema utakaozaa matunda mema kwa ulimwengu. Hili lazima liwe lengo letu.

Lakini ni lazima tubadili fikra zetu ili kulifanya taifa hili kuwa la haki na endelevu. Kuwa na umoja na utengamavu.

Ni lazima tupande mti huu katika sehemu nyevu nyevu na sio kavu ili ulete matunda. Ushupavu wetu

ni lazima uwe katika kutenda haki na katika yaliyo sahihi. Hatutaweza kuendelea kwa kufanya makosa iwe mmoja mmoja miongoni mwetu, katika familia au katika Taifa.

Ni lazima tufuate mkondo ulio sahihi na kufanya maamuzi sahihi wakati wote ili taifa letu listawi na liwe endelevu. Ni lazima tubadilishe mwelekeo wa taifa letu kwa kujenga msingi mpya wa maadili na nidhamu, wa upendo na mshikamano.

Hii ndio njia pekee itakayo tuondoa kwenye umaskini kwa kufanya yaliyo sahihi na kutenda haki hakuna njia nyingine yeyote.

Ni lazima tujenge taifa ambalo litawafanya watu wa mataifa mengine wawe wema. Hili ni aina ya taifa ambalo ni lazima tulijenge kwa nguvu zetu zote. Ni lazima tuwe mlango kwa mataifa yote.

Mataifa yote ni lazima yawe mema kupitia sisi. Taifa la namna hii ni lazima lijengwe. Tutabadilisha roho na fikra za watu wetu kuwa bora.

Hatutaweza kubadili mataifa mengine bila sisi kuwa watenda haki na wema. Kwahiyo ni muhimu sana kwetu kuwa mfano kwa mataifa mengine.

Tunauwezo wa kujenga taifa hili katika misingi imara ambayo haitotetereka misingi ya haki na wajibu miongoni mwetu, huu ni mwelekeo ambao ni lazima tuwe nao, tutakuwa na nguvu pale tu tutakapo zingatia misingi ya haki na uhuru wa watu wetu.

Taifa linaweza kuwa taifa dogo linalozingatia haki na lililo tayari kukua na kuchukua nafasi yake katika

dunia. Bila mtazamo huu chanya kwa taifa letu itakuwa vigumu sana kwetu kuendelea.

Ni lazima tuamini tunaweza kutoka hapa tulipo na kujenga taifa imara la watu wenye mshikamano na wenye nia moja na dhamira moja ya kuendelea.

Watu ni jinsi wanavyofikiri. Kama tukifikiri kwamba hatuwezi basi hatutaweza, ni lazima tuamini tunaweza kutoka hapa tulipo na kujenga taifa imara na litakalo kuwa mfano kwa mataifa mengine. Kazi hii ni jukumu letu ambalo tunapaswa kulifanya kizazi hadi kizazi katika mtazamo ule ule chanya, wa kuwa tunaweza kujenga taifa hili kuwa bora na imara.
Ni katika jitihada hizi za kutaka kuona jamii zetu zikiimarika na nchi yetu ikikua tutaweza kuondoa umaskini, ujinga na maradhi.
Mambo ambayo juhudi za pamoja na kujitolea kunahitajika kuyamaliza ili tutoke hapo tuelekee kwenye maendeleo ya juu zaidi.

Kama tukitengeneza siasa zetu katika misingi imara na bora yenye mlengo chanya ya ujenzi wa taifa letu na kama viongozi wetu wakibadilika na kuweka maslahi ya taifa mbele kuliko yale ya binafsi tunaweza kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Mambo haya yote yanahitaji viongozi shupavu na wenye kujitolea kwa maendeleo ya nchi.

Matatizo tuliyonayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na uongozi mbovu na usio makini. Viongozi ambao wameenda kwenye siasa kwaajili ya kupata maslahi binafsi badala ya yale maslahi mapana ya taifa.

Kwa kuangalia maslahi yao zaidi wameacha mambo mengi yahusiyo maendeleo na ukuaji wa taifa hili.

Tunahitaji viongozi sasa wataojali na kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu ambao watakuwa tayari kujitolea kwaajili ya ukuaji wa taifa hili.

Uongozi sasa hivi umekuwa ni kutafuta umaarufu, maslahi na madaraka tu, na sio maendeleo ya jamii yetu na taifa kwa ujumla.

Rushwa na ufisadi vimefanya taifa letu kuwa na mgawanyiko katika jamii na katika vyama vyetu vya siasa, kutokana na viongozi wanaotafuta madaraka kwa rushwa na kwa kugawanya watu kwa makusudi kwaajili ya faida binafsi.

Matokeo yake nchi sasa hivi imegawanyika katika makundi. Hili ni tatizo ambalo tunakabiliana nalo sasa hivi kama taifa. Tatizo hili linahitaji kiongozi asiye na ubinafsi na mwenye busara ya kutosha kulitatua.

Tatizo jingine la umaskini uliopitiliza linachangia katika mgawanyiko katika taifa kwa walionacho na wasionacho na jukumu tulilonalo sasa hivi ni kuweka uwiano kati ya maskini na matajiri kwa kuwapunguzia ugumu wa maisha watu wa maisha ya chini. Amani ya nchi yetu haitokuwepo kama kutakuwa na kundi kubwa la watu maskini ambao wanashinda njaa na kundi dogo lenye utajiri wa kupindukia.

Kwa kufanya hivi tutajenga taifa letu katika misingi imara, hatutaweza kujenga taifa hili likawa imara kama tutawasahau maskini na kuwakumbatia matajiri. Ni lazima tujenge taifa lenye matumaini kwa wote. Taifa ambalo kila mtu ataamini kesho atafanikiwa kwa kujenga mazingira ya watu wetu

kufanikiwa katika nchi yao. Ni katika mazingira haya tutarudisha uzalendo kwa taifa.

Ni lazima tujenge serikali ambayo inawathamini wananchi, ambayo wananchi wataweka matumaini yao kwao. Kwa kuunda serikali inayotenda haki kwa wote na inayowajibika kwa dhati kwa wananchi.

Lakini tusidhani kama tutafanikiwa kama tukiwachagua viongozi ambao tunawajua ni waovu na kuwaweka madarakani. Hawataweza kutusaidia kutuletea maendeleo katika nchi, zaidi ya kujitajirisha wenyewe. Ni muhimu kuangalia hili ni jambo la msingi sana.

Ni wakati sasa kwa watu wenye nidhamu na maadili mazuri kuingia kwenye siasa ili kuleta mabadiliko kwa kufanya hivyo tu ndio mwelekeo tulionao sasa kama taifa utabadilika na taifa letu litakuwa zuri. Uongozi unahitaji ushupavu, nidhamu na maadili ya kutosha kuleta mabadiliko katika jamii.

Kwahiyo jukumu la kimsingi kwa sasa katika taifa letu ni kuleta taifa letu pamoja ambalo limegawanyika. Hatuna mtazamo mmoja kama taifa tuna mivutano ambayo haina tija. Ingekuwa mivutano ambayo yenye mantiki juu ya namna gani tuliboreshe taifa letu ingekuwa ni ya maana sana, lakini mivutano mingi ni isiyo na tija na mengine ni mivutano ya magenge yanye maslahi binafsi.

Mivutano yote hii ukiangalia kwa ukaribu haina maslahi kwa taifa bali ni kwa maslahi binafsi ya watu na vikundi vya watu. Umoja wa nchi ni jambo muhimu sana kwa taifa lolote kupiga hatua kimaendeleo.

Kuna huku kutokuridhika kwa wananchi juu ya serikali yao ambayo wanaona wameichoka. Wangependa waibadilishe kwa kutokana na kutotimiza mahitaji yao na ufisadi. Watanzania wana haki hiyo ya kuitoa serikali yeyote na kuiweka nyingine ambayo itakidhi mahitaji yao. Lakini lazima wafanye uchunguzi kwa makini kama kuiondoa serikali moja na kuiweka nyingine maisha yao yataboreka. Kwamba serikali itakayokuja italeta maendeleo na matumaini kwa wote.

Kwa asili ya siasa na wanasiasa mara zote wamekuwa waongo na wanaowapa watu matumaini ya uongo na mara wanapoingia madarakani unakuwa huwezi kutofautisha kati ya wale walioondoka na walioingia. Ni muhimu sana kuangalia kwa umakini tabia za viongozi na vyama hivi ili tunapofanya uamuzi usitokane na hasira au kuchukia bali utokane na uchanganuzi yakinifu na kufanya maamuzi sahihi.

Hili ni jambo muhimu sana kwasababu mimi binafsi bado sijaona chama chenye unafuu miongoni mwa vilivyopo. Ambacho kitajenga jamii nzuri ambayo tutajivunia. Wengi wao wameunda vyama hivi kwa maslahi binafsi. Hali hii inahitajika kubadilika. Kwa faida na mustakabali wa taifa letu.

Wananchi ni lazima watambue viongozi wengi wa sasa wanagombania uongozi kutokana na faida inayopatikana kutokana na uongozi, umaarufu na mamlaka na sio dhamira ya dhati ya kunyanyua maisha ya watu na ujenzi wa jamii zetu. Vurugu nyingi zinazotokea ukiangalia kwa umakini ni vurugu zisizo na tija na zenye kujitafutia umaarufu na kutafuta mamlaka kwa manufaa binafsi na sio maslahi ya taifa kwa upana wake.

Kwa watu wasio makini wengi hudhani wanatetewa na kwamba viongozi wana dhamira ya dhati mioyoni mwao kwa taifa. Hali hii imepelekea taifa letu kuwa lenye mgawanyiko. Nakufanya pia vijana wengi kuingia kwenye siasa wakidhani kwa kuingia huko watatajirika haraka haraka na watapata umaarufu, Kutukanana kwa wanasiasa, vurugu na fujo, hakutokani na dhamira ya dhati ya kuhudumia wananchi bali ni ulafi wa kutafuta madaraka na umaarufu. Ni lazima tuangalie mambo yote haya yaliyotufikisha hapa hasa katika kipindi hiki kigumu cha utandawazi.

Wote sisi tunaounda taifa hili ni lazima tutambue mustakabali wa taifa hili unatutegemea sisi. Ni lazima tufikiri kuhusu kiazi chetu kijacho.

Taifa linaundwa na vipande tofauti ambavyo ni lazina viwekwe pamoja kwa namna yoyote kama kitu kimoja ili taifa liende, hasa kwa asili ya taifa letu ambalo lina watu wa makabila mengi na dini kuu mbili. Taifa hili halitofanya kazi kama vipande hivi havitokuwa kitu kimoja ili taifa hili lifanye kazi na ni lazima viwe chini ya serikali moja ambayo inafanya kazi kwa ufanisi kuviunganisha na kuvifanya vifanye kazi katika utii na utengamavu kama kitu kimoja.

Juhudi zozote za kuvitenganisha ni kusambaratisha nchi. Taifa huwa kitu kimoja kutokana na utamaduni na matendo ya mara kwa mara ya kufanya liwe moja. Kutokana na sheria ambazo zimetungwa kuhakikisha vipande hivi vinaendelea kuwa vimoja.

Lakini pia kutokana na kutenda haki miongoni mwa vipande hivi vinavyounganisha taifa. Chuki miongoni mwa vipande hivi huvifanya vitengane na kuzua vurugu na vita ni muhimu kufanya kila jitihada vipande hivi viendelee kuwa vimoja kizazi baada ya

kizazi ili kile kinachoonekana kama ni vipande kiwe kitu kimoja kamili.

Ni kwakuwa wamoja kwetu ndio tutafaidika, kama mtu mmojamoja na kama taifa na ndipo tutaendelea kwa uharaka zaidi. Ni muhimu kwa serikali kuhakikisha taifa hili linaendelea kuwa moja kwa kutumia busara na sheria kali ili taifa liendelee kuwa moja na watu wake wawe wanaopendana.

Ni lazima kila kipande kimoja kimtambue mwenzake kama ni sehemu yake, kama gari na sehemu zinazounda gari. Kwamba bila kiungo kimoja katika gari halitoweza kuendelea na sisi kama watanzania tutaendelea haraka zaidi kama tutakuwa wamoja kuliko tukitengana kwa kuangaliana kwa dini au ukabila bali tukiangaliana kama watanzania, itakuwa jambo jema na lenye manufaa zaidi kwetu sote.

Ukisikia taifa limeshindwa ni kwa hivi vipande vinavyounda taifa kuanguka na kila kimoja kupigania kubaki peke yake na sio hali nzuri sana. Kwa Taifa changa kama Tanzania, hali hii inaweza kutokea kama serikali haitokuwa makini katika utendaji wake wa kila siku kuhakikisha taifa hili linaendelea kuwa moja.

Kwahiyo ni lazima hivi vipande vitii serikali ambayo inakaa kama kiunganishi cha hivi vipande katika kutoa haki na kuleta maendeleo kwa wote bila kupendelea upande wowote.

Ili kuhakikisha umoja na uwepo wa taifa letu kwa vyovyote vile ni lazima kuwepo na usalama wa taifa ulio imara kwa wakati wote ambao lengo lake ni kuhakikisha umoja na usalama wa taifa letu. Hii yote inahitaji kiongozi imara ambaye macho yake yote

yako katika ulinzi na uendelezaji wa taifa hili kwa faida ya ujumla.

Jeshi letu la polisi ni lazima liwezeshwe kuweza kufanikisha kazi yake ya ulinzi na usalama kwa raia na kulazimisha utii wa sheria na taratibu za nchi, kwa njia hii pekee na kwa kuhakikisha jamii yetu inafuata na kutii sheria, nchi yetu itabadilika, nidhamu itarudi na haki itakuwepo.

Ukiunganisha malezi na makuzi ya watoto wetu katika familia, elimu bora na jamii inayoshiriki kwa pamoja katika malezi, tutasaidia sana polisi katika kufanikisha kazi yake na katika kujenga jamii bora.

Vinginevyo tutaipa kazi kubwa polisi na mahakama na watu wetu wengi pamoja na vijana wataishia gerezani ikiwa wazazi hawatozingatia maadili mema kwenye nyumba zao na jamii isiposhiriki kwa pamoja.

Hii yote inahitaji kiongozi hodari na makini kuileta nchi yetu kwenye utaratibu na mpangilio kwa sababu bila mpangilio na utaratibu hatutaweza kuendelea.

Wala hatutakuwa na nidhamu kwenye bunge wala kwenye taasisi zetu. Kwa utaratibu huu itamwia urahisi sana kwa kiongozi kutawala kama kila mtu na kila taasisi ikitimiza wajibu wake kwa faida ya taifa.

Tukijenga nidhamu hii na mpangilio na utaratibu katika familia na jamii yetu. Tutapata nguvu kazi nzuri. Na hata jeshi letu ambalo kazi yake ni ulinzi na usalama wa taifa letu watafanya kazi hiyo sio kwasababu ni ajira bali ni jukumu la dhati la kulinda jamii yao.

Hisia hii ni muhimu sana. Hisia hii ya undugu na utaifa inapotoweka kila mtu hufanya kwaajili ya

pesa na taifa huangamia. Ni lazima tujenge umoja huu. Ni wakati sasa wa kuwa wa kweli wa dhamira na kuzungumza ukweli ili tujenge taifa.

Ni wakati wa kuweka maslahi ya jamii mbele. Kwa kufanya hivi pekee ndio tutaweza kufanya kazi kwa pamoja na taifa letu kuendelea. Ni wakati sasa wa kuacha ubinafsi na kuangalia maslahi mapana ya taifa.

Wajibu huu kwa jamii ndio msingi haswa wa jamii iliyostaarabika. Ni lazima tujenge vijana wanaowajibika kwa jamii na kwa taifa. Ni lazima tujenge familia imara zitakazo unganika na kuunda jamii yenye malengo mapana ya pamoja.

Ili kufanikisha hili pia ni lazima polisi wetu wawe na uelewa mkubwa ili wajue wanachotenda ili kulinda utaratibu na sheria. Ni lazima tuwe na dira kama taifa. Watu wengi wanaenda polisi na jeshini kwasababu wamekosa sehemu nyingine ya kwenda hii sio sahihi ni lazima huu uwe ni wajibu na watu wetu hawa waheshimiwe kwasababu wanashiriki kujenga jamii. Kwani wajibu wao kulinda haki na kusimamia sheria na kufanya yale yaliyo sahihi wasiwe wao chanzo cha uvunjaji wa amani na sheria za nchi.

Nidhamu ni muhimu sana katika ujenzi wa taifa lolote lile duniani, taifa lolote lisilokuwa na nidhamu halitoendelea ni muhimu kusisitiza hili ili liingie kichwani kwa faida ya nchi.

Ni lazima pia tuwe na wanasiasa wanaojitambua na wanaojua wanafanya nini. Ni lazima tubadilike kwenye siasa sio sehemu ya kwenda kutafuta pesa. Siasa inahusu maendeleo na haki za watu ni muhimu kuzingatia hili ili tujenge jamii bora.

Tukiisha jenga jamii inayowajibika itakuwa rahisi sana kwetu kuendelea. Tatizo la umaskini wetu liko hapo kwenye uwajibikaji. Uwajibikaji kwa familia, jamii na kwa Taifa. Tukiwa na jamii inayowajibika itachagua wabunge wanaowajibika bungeni kutoka kwenye jamii yenye utaratibu na mpangilio kwenda kuwawakilisha na tutakuwa na bunge linalowajibika. Ujenzi wa Taifa hili ni wa kila mtu katika sehemu yake.

Serikali ili kuweza kutawala vizuri isikubali ujenzi holela usio na utaratibu, itakuwa vigumu kutawala watu ambao wanaishi ovyo ovyo. Ni lazima makazi ya watu yawe kwenye mpangilio sio kuacha tu kila kitu ovyo ovyo. Hili ni muhimu sana ili kuweka nchi katika mpangilio. Ni lazima tujitambue sasa. Ni lazima tujue ni nini kimetuunganisha kama taifa. Ni lazima tujitambue mmoja mmoja kwa kuutambua utaifa.

Dhana ya utaifa ni kusanyiko la watu, makabila au dini wenye malengo mamoja. Watu wanaoishi katika taifa fulani huitwa raia. Wana haki na pia wana wajibu kwa taifa.

Familia ina haki ya ukuaji wake na kuwa na mali zake yenyewe na kujitambua yenyewe kama familia, lakini hii familia lazima itambue uwepo wake pia taifa, ambalo linampa faida zote anazozipata na kuendelea.

Ni dhahiri kwamba binadamu hawezi kuendelea akiwa peke yake kama akiishi katika jamii. Faida nyingi anazozipata binadamu ni kutokana na kuishi na jamii, ni kutokana na kuwepo katika Taifa.

Ambapo kwenye taifa kuna mgawanyo wa kazi ambao husaidia kila mmoja kujijenga na kujiendeleza. Kwa mfano; Daktari akitaka kujenga nyumba yake ni lazima atahitaji towashi. Hataweza kujenga wakati huo huo akitibu na wakati huo huo akitengeneza thamani kwaajili ya nyumba yake.

Kwahiyo kila mtu anamtegemea mwenzake ili kutengeneza kitu kilicho kamilika. Huu ndio umuhimu wa mtu kuishi katika taifa, umuhimu wa watu kuishi pamoja kama taifa. Faida zote tunazopata ni kwaajili ya sisi kuishi kama taifa.

Kwaajili hii ndio maana taifa huendelea. Maendeleo ya taifa ni jukumu la kila mmoja anayeunda taifa. Tusingekuwa na barabara, magari au hospitali kama tusingekuwa tunaishi kama taifa.

Huu ni muunganiko ambao unajenga kitu kimoja. Kwahiyo ni muhimu kutambua umuhimu wa taifa na kuheshimu. Kwa mtu mmoja mmoja tusingeweza kufanikiwa hivi.

Kama tukiongelea kuhusu biashara pia ni lazima zijengwe katika misingi ya utaifa. Ili biashara hizi ziwe ni zenye faida kwa taifa badala ya hasara.

Ni muhimu kuzingaia hili sana kwa maendeleo ya taifa. Tusifanye biashara bila kuangalia maslahi ya taifa na ya jamii ambayo faida zote tunazipata humo.

Ni lazima kuwepo sheria nzuri zitakazo zingatia misingi ya kibiashara ambayo haitapokonya uhuru wa watu. Ni lazima tujenge jamii ambayo haina rushwa na ambayo kila mmoja anawajibika kwa mwenzake kama ni sehemu yake ya mwili. Masuala haya ni ya msingi sana kwa ukuaji wetu kama taifa.

Sioni sababu ya taifa hili kuwa maskini isipokuwa kutokuwa wamoja kwetu katika malengo na kutokuwa na dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo yetu wenyewe. Ni muhimu kuzingatia haya iwe kwenye elimu au kwenye maliasili zetu.

Katika elimu inaonekana kabisa haija tengenezwa ili kuleta maslahi mapana ya taifa bali ya mtu binafsi, nidhamu upande wa elimu yetu ni ndogo mno kwa walimu na kwa wanafunzi.

Kuna hitajika udhibiti katika elimu yetu ili kuleta nidhamu. Na ni lazima ijengwe ili kuleta maslahi mapana ya taifa na sio yale ya mtu binafsi. Ni lazima tujenge uzalendo kwa wanafunzi katika ngazi zote. Akili za wanafunzi lazima zielekezwe katika mwelekeo wa utaifa.

Elimu yetu ni lazima iundwe kumfanya mwanafunzi kujitegemea, msingi wa elimu ya kujitegemea na kubaliana na Baba wa taifa.

Taifa litengeze mfumo wa elimu utaomfanya aelimike, awe na ufahamu mpana wa kuanzisha maisha yake mwenyewe bila kutegemea serikali na huo ndio msingi wa elimu.

Ni kumpa maarifa ili maarifa yamfanye ajitegemee, asiwe tegemezi tukiwa na elimu ya namna hii itakuwa rahisi kwetu kuendelea. Watu wetu watakuwa na faida sana kwa nchi na mchango mkubwa kuliko wale wanaosubiri ajira. Na kwa mwelekeo huu tutajenga taifa imara na la watu wabunifu. Ni lazima tutengeneze nguvu kazi iliyoelimika na uliyojazwa na ufundi stadi.

Mwelekeo uwe sasa mtu mmoja mmoja atalifanyia nini taifa na sio taifa limfanyie tu kila kitu mtu. Ni

muhimu tukabadili fikra hizi ili taifa hili lipige hatua. Mantiki ya elimu kwakweli ni ukombozi wa fikra. Serikali inawajibu wa kutoa elimu bora itakaowafanya wajitegemee na kuajiri wachache, kwaajili ya utumishi wa umma.

Ni lazima tuwafunze watu wetu kujitegemea na kuwa wazalishaji mali hodari bila kutegemea serikali kwa kila kitu, Kujitegemea huku kwa mtu ndio msingi wa maendeleo ya taifa.

Kwakuwa na mfumo wa elimu wa namna hii utakaowafanya watu wajitegemee na wawajibike tutapiga hatua, serikali itaongeza mapato yake ya kodi kwakuwa uzalishaji utaongezeka na nchi itakuwa na tija.

Pamoja na hayo yote muungano wa mtu huyu na serikali yake lazima uwe pale pale. Isiwe kama kitu kinachojitegemea bali ni kama sehemu ya taifa.

Ambapo atafahamu hataweza kufanikiwa pasipo taifa na pasipo serikali ambayo itatengeneza mazingira mazuri kwa yeye kufanikiwa. Ni dhana hii ya uhuru wa mtu chini ya serikali yake ndio itakayofanya taifa hili liendelee na kujitegemea. Na sio kuwa na watu wanaosubiri kuajiriwa. Ni lazima tutengeneze vijana wanaojitambua. Hili halitowezekana pasipo elimu iliyo bora.

Kwahiyo ni vigumu kuzungumzia uchumi pasipo kuzungumzi masuala haya ya msingi kuhusu jamii. Tutakapokamilisha mambo haya mengi niliyozungumzia nina uhakika uchumi wetu utaimarika na taifa letu litapata maendeleo.

Lakini kwanza ni kwa jamii zetu kuwa na nidhamu, mpangilio na utaratibu. Maendeleo kama

maendeleo ni matokeo ya kazi na hakuna maendeleo pasipo kufanya kazi. Kama tutawapanga watu wetu vizuri katika kila nyanja nina uhakika tutapata maendeleo kwa haraka zaidi. Hatutaweza kuzungumzia maji vijijini, umeme na udhibiti wa maliasili zetu bila kuzungumzia mambo ya msingi niliyoyazungumzia. Ambayo kwa uhakika ndio yatakayoleta haya mengine na ambayo yatakayojenga jamii iliyostaarabika.

Bila dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko kwa upande wa wananchi na kwa serikali taifa letu halitopiga hatua kimaendeleo.

Bila kujitambua kwetu safari yetu ya kuleta maendeleo itakuwa mbali sana. Lakini chombo pekee kitakacholeta mabadiliko kwa haraka ni elimu iliyotengenezwa katika ubora na ambayo lengo lake kunufaisha jamii kwa ujumla na sio mtu mmoja mmoja. Kama jamii yote ikielimika ni lazima tutapiga hatua kimaendeleo kwasababu kila mtu atakuwa anajitambua.

Kwa hali iliyopo sasa hivi, Taifa letu linahitaji kiongozi ambaye yuko makini sana katika ukuaji na maendeleo ya kijamii kutokana na huu utandawazi. Udhibiti unahitajika ili ukuaji wa watoto wetu ujenge maadili na nidhamu itakayochangia kuimarisha taifa letu. Kama nilivyosema nidhamu hii ni muhimu sana kwa taifa letu.

Bila nidhamu hii hatutaweza kupiga hatua yeyote kubwa ya kimaendeleo. Nidhamu hii inahitajika nyumbani, shuleni, kazini na katika serikali yetu. Hili dhahiri kabisa kuna tatizo hili la nidhamu katika taifa letu.

Ni lazima taifa letu tulirudishe katika nidhamu na utaratibu ili kuleta heshima katika taifa. Ili kuleta umoja na mshikamano kwa watu wetu wote. Bila nidhamu hii taifa letu halitaweza kuendelea kuwa moja.

Haya ni mambo ambayo tunahitaji kuyaangalia kwa umakini sana. Taifa letu lina watu wa dini mbali mbali na makabila tofauti, nidhamu hii inahitajika ili watu wetu waendelee kuwa kitu kimoja. Kuvumiliana katika jamii kunatokana na nidhamu hii. Na mashirikiano yetu katika jamii yatatokana na nidhamu lakini pia kuendeshwa na fikra sahihi.

Ni jambo la msingi kutengeneza taifa ambalo linangalia maslahi mapana ya jamii badala ya yale ya kibinafsi, kwa kufanya hivi tutalilinda taifa letu na kulifanya liwe endelevu.

Migawanyiko mingi katika jamii inatokana na watu kuangalia maslahi binafsi badala ya maslahi mapana ya kijamii. Huu ni msingi ambao ni lazima tuujenge. Kabla ya kufanya kitu chochote ni lazima tuangalie maslahi ya jamii na kuyalinda.

Kutokuangalia maslahi ya jamii kwanza na kuweka ubinafsi mbele ni sawasawa na kukata mti tulioukalia, tutaanguka wote.

Lakini suala la kulinda maadili pia ni suala la jamii nzima. Watu kufanyabiashara bila kuangalia maadili, mila na tamaduni, bali kuangalia maslahi binafsi ni kosa. Lazima tujue tunaua jamii yetu wenyewe na taifa letu kwa kufanya hivyo.

Uchu wetu wa kupata faida usitufanye tuangamize taifa, ni lazima taifa letu lilindwe katika kila nyanja na kwa ujumla wake. Ni lazima tuamke sasa na

tutambue umuhimu wa jamii na tuwajibike. Taifa hili tutalijenga na kulilinda wenyewe lakini pia tutaliua wenyewe, tusipokuwa makini katika ujenzi wake.

Mataifa mengi yameharibiwa kwa uchu huu unapoingia, na kusahau jamii bali kufikiria kujiingizia pesa tu hata kama njia hizo zitakuwa na madhara kwa jamii na kwa taifa.

Matatizo yote haya ya ufisadi na rushwa yana madhara makubwa kwa jamii na mwisho wake ule umoja na mshikamano wa watu hutoweka na mwisho kabisa watu huingia katika vita.

Ni muhimu watu wetu kujizuia na ndio maana nasema nidhamu hii ni ya msingi sana ili tujenge taifa ambalo ni la amani na endelevu.

Ili mambo haya yaimarike ni lazima kila mtu amwangalie mwezake kabla ya kujiangalia yeye, aingalie jamii kwanza kabla hajaangalia maslahi yake binafsi.

Kwa kufanya hivi tutajenga jamii imara na endelevu na ndipo tutakapo pata amani ya kweli. Kwa mtazamo huu wa kumwangalia mwenzako kwanza na jamii kabla hujajiangalia mwenyewe, tutafanikiwa kuwa na utulivu na amani ya kweli.

Hii ni sheria ambayo ipo na ambayo itatupunguzia uovu katika nchi yetu. Ni katika mazingira haya ya ujenzi wa taifa letu katika haki na nidhamu tutapiga hatua na kuheshimiana. Hatutaweza kujenga taifa hili katika matazamo wa ubinafsi alafu tukaendelea na kuwa na amani.

Kwa huu wajibu wa kila mmoja kwa mwezake ni muhimu sana katika ujenzi wa taifa bora na imara

lakini pia lenye furaha. Mivutano yote katika jamii inatokana na haya mambo. Ni muhimu sana kujiangalia upya. Kwasababu kwetu sisi ni muhimu kujenga jamii yenye furaha. Na furaha hii haitokuwepo pasipo upendo miongoni mwetu.

Umaskini wa taifa hili utaondoka pale tu tutakapofanya kazi kwa pamoja na kwa kuangalia maslahi ya jamii na ya taifa badala ya kuangalia yale ya kibinafsi kwanza.

Kutokana na kuangalia maslahi ya kibinafsi kwanza na uchu, tumesababisha kuwa na matabaka katika taifa letu kati ya matajiri wachache wanaofaidi matunda ya nchi na maskini wengi, na katika hali ya namna hii mara zote amani ya taifa huwa hatarini.

Kama serikali isipoangalia maskini na kuwakumbatia matajiri tu, wajitayarishe kwa vurugu nchini na pengine mapinduzi. Maskini ni rahisi kudanganyika na kutumika kufanya uasi, vurugu na fujo. Mtu mwenye njaa hana matumaini. Ni muhimu na ni lazima tujenge jamii yenye matumaini kwa watu wote.

“Kulikuwepo na vijana wawili watafutaji mali na marafiki. Wote walikuwa na ndoto ya maisha mazuri. Wajenge nyumba nzuri waoe na watunze familia zao, katika harakati zao za kutafuta maisha wakakutana na na mzee mmoja akawahadhia kuhusu meli moja iliyoanguka miaka mingi iliyopita iliyokuwa na dhahabu ndani yake, kutokana na hadithi ya mzee huyo wakaamua kwenda kutafuta hiyo mali.

Wakajitayarisha wakaenda kutafuta mali hiyo chini ya bahari wakafanikiwa kuiona na kuona dhahabu zilizokuwepo ndani yake. Wakaanza kupakia moja baada ya nyingine kadiri walivyokuwa wakipakua na kuweka kwenye mtumbwi wao, tamaa

zikawaanza kuwaingia mmoja baada ya mwengine na kutokuaminiana miongoni mwao. Mmoja akaanza kumtuhumu mwenzake anaiba, chuki ikaiingia.

Sasa dhahabu zilikaribia kuisha na mmoja wao alikuwa bado yuko chini ya bahari na mwingine bado alikuwa ameisha fika kwenye mtumbwi, kwa kutaka kumdhulumu mwenzake aliiwasha mashine ya boti na kuondoka kwa kasi, wakati mwenzake akitoka chini ya bahari aliona mwenzake ndio anaoondoka, alitaharuki kwa woga na wasi wasi ulimwingia, kutokana na kasi na kukosa umakini kijana aliyekimbia na mtumbwi aligonga mwamba na mtumbwi kupasuka dhahabu zote kurudi tena majini. Papa walikuwa karibu wakafanya sherehe ya kumtafuna. Mwingine baada ya kukaa muda mrefu majini alichoka na kufariki dunia''

Watu hawa walikuwa na ndoto moja, kutokana na tamaa na ubinafsi waligawanyika na kile walichokuwa wakiota kukipata kikatoweka. Kwetu sisi ni lazima tuwe na maono ya kujenga taifa bora na la watu wamoja na sio wabinafsi kama vijana hawa. Taifa letu litakuwa kama tutakuwa wamoja kwenye dhamira na malengo yetu. Ni lazima tujenge taifa zuri na na kutamanika. Kwa jitihada zetu, umoja wetu na maarifa yetu kwanini tusifike tunapopataka? Kama tukiwa na hali na moyo wa kujiletea maendeleo yetu wenyewe?

Akili za vijana wetu katika taifa hili ili kwa pamoja tulijenge pawe sehemu nzuri ya kuishi kwa vizazi vyetu. Sio vibaya kushawishika kama tabia wanazoiga ni zenye manufaa kwetu kama taifa, lakini imekuwa ni kinyume chake.

Ni lazima tujenge ustaarabu wetu na namna yetu ya kujiongoza wenyewe katika njia tunayotaka wenyewe

kwenda. Ni lazima tujenge kizazi cha wachapa kazi na shupavu kinacho jithamini. Ni lazima tujenge uchumi wetu wa ndani na kujitegemea.

Mimea hukua kulingana na asili ya udongo uliopo, udongo wenye rutuba huzaa mazao yaliyo bora. Ni muhimu kwetu kujenga mzingira bora kwa kizazi kijacho ili kikute mazingira bora kuliko tuliyonayo sisi, kuliko tunayoyaishi sasa hivi.

Ni lazima kazi hii ifanyike ile kuleta umoja, upendo mashirikiano katika ujenzi wa taifa letu. Tujenge taifa watu wake wawe hawana wasiwasi wa baadae ya kesho kwa kuwatengenezea mazingira mazuri kwao kuendelea.

Ni lazima watu wetu waendelee kiakili, kiroho na kimwili awe binadamu aliyekamilika, na baadae maendeleo ya kimali. Bila vitu hivyo hatutaweza kujenga jamii yenye utengamavu.

SURA YA 7

BUSARA

Katika maisha yote kutoka karne nyingi busara ndio imekuwa kiongozi na mlinzi wa vizazi vingi. Mataifa mengi yalijengwa, kukuzwa, kulindwa na

kuongozwa na busara. Na pale busara inapotoweka baadae ya vizazi huwa hatarini. Busara ni uwezo wa kufanya chaguzi bora ambazo zitafanya jamii na taifa kuendelea.

Taifa letu kwa kipindi hiki limeondokewa na hii busara ambayo ni muhimu sana katika kufanya maamuzi yenye tija kwa taifa na katika kuleta watu pamoja.

Ni dhahiri sasa baadae yetu iko matatani kama hatujabadilisha mwelekeo wetu kama taifa na kuchagua njia nyingine kuwa mapito yetu. Watu wenye maono ni muhimu katika Taifa lolote pasipo maono Mataifa huangamia na kupotea kabisa. Na sisi kama Taifa tuna changamoto hiyo.

Tuna changamoto kubwa ambazo viongozi wengi wa Taifa hili sidhani kama wanazifikiria pengine wanafikiri nchi hii itajiongoza yenyewe bila maono. Taifa hili linahitaji mwelekeo na mwelekeo huu utakuwepo pale tu watu stahili watakapoingia madarakani na wale waliopo madarakani kuwaachia kapteni anayeweza kuongoza meli kuipeleka katika nchi sehemu istahiliyo na kuzuia mawimbi yaliyopo sasa hivi.

Katika Taifa hili ni lazima tuelewe kwamba sio kila mtu anastahili kuwa kiongozi. Uongozi ni jukumu kubwa sana, na yeyote yule anayetaka kuongoza watu lazima ajue ni wapi anataka kuipeleka jamii yake na Taifa lake, ni aina gani ya Taifa analotaka kulijenga na ni jinsi gani ataunganisha watu wa makabila tofauti na dini tofauti waje pamoja katika lengo moja la ujenzi wa Taifa letu kuelekea sehemu fulani.

Sasa hivi katika nchi yetu uongozi umekuwa ukigombaniwa kama pipi jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali kwa taifa letu. Katika taifa lolote watu wakiwa wanautaka uongozi tena kwa nguvu ili mradi tu wawe viongozi basi taifa la namna hiyo huwa na hali mbaya, taifa ambalo watu wake wanaugopa uongozi na kuwapa watu wake bora wawaongoze wana nafasi kubwa sana ya kuendelea.

Ni muhimu watu kuangalia hili suala kwasababu uongozi unahusiana na haki pamoja na uhai wa watu na baadae ya taifa lolote lile inastegemea ubora wa viongozi walionao. Nchi bila viongozi bora na imara wenye na maono huyumba.

Uongozi si jambo la kutaka kwenda kupata utajiri au umaarufu wa kuwa kiongozi. uongozi ni kuleta mabadiliko ya watu. Bila busara hii taifa letu halitoweza kupiga hatua kimaendeleo.

Ili tuendelee lazima tujue ni wapi tunataka kwenda. Hatujawa taifa ili tutafute mkate tu, Tumekuwa Taifa ili tufikie kilele fulani cha mafanikio na hili haliwezi kufanikiwa kama hatutaweza kuunganisha vipande vinavyote-ngeneza Taifa hili.

Bila kuelewana sisi kwa sisi na kuwa na lugha moja kamwe hatutaweza kulijenga Taifa hili. Ni lazima tutambue kwanza sisi ni ndugu na tuthaminiane na kuheshimiana.

Ni lazima tutambue kwamba tuna majukumu ya pamoja ya ujenzi wa Taifa hili na vizazi vyetu vijavyo vina tutegemea sisi ili kujenga mazingira mazuri kwao.

Ni lazima tujenge upya familia zetu katika misingi imara, ni lazima tujenge upya mahusiano yetu

kama tunataka Taifa hili liendelee. Tutakapo kuwa na mpangilio pamoja na utengamavu katika jamii yetu ni hatua ya kwanza kwa Taifa letu kuendelea.

Wajibu kwa familia ni msingi imara wa ujenzi wa Taifa bora. Ni jinsi gani tunawalea watoto wetu katika Utaifa na maadili bora? Familia zetu hazijajengwa katika misingi ya utaifa. Watoto wetu wanajikulia kama uyoga bila malezi bora ya kuheshimu utaifa wao na uzalendo, bila maadili na nidhamu.

Ni muhimu kuwa na wajibu wa pamoja katika maendeleo ya Taifa hili, tukifahamu kwamba tunatengeneza baadae ya watoto wetu. Taifa hili tutaliendesha kwa akili zetu na busara zetu na tutaliua pia kwa ujinga wetu.

Ni lazima turudishe akili zetu na tuanze kufikiria. Tunahitaji mabadiliko ya fikra na moyo. Tunahitaji kupendana na kuthaminiana. Tunauwezo wa kukaa pamoja na kutengeneza baadae ya Taifa letu kama watu wenye akili timamu. Taifa letu halina maadili hakuna utaratibu. Hatutaweza kuendelea bila ya vitu hivyo viwili.

Wote tunashuhudia jinsi Taifa hili linavyo mong'onyoka. Ni dhahiri tunahitaji juhudi za makusudi ili kuleta watu wetu pamoja wa dini zote na kabila zote na matabaka yote ili tuwe na lengo moja la ujenzi wa Taifa letu. Ambalo ni muhimu sana kwetu.

Mimi binafsi silijui Taifa lingine lolote zaidi ya hili. Nimekula na kukuzwa na chakula kinachoota katika ardhi hii na nina amini katika Taifa hili, na bado nina matumaini tunaweza kubadilika. Ninaamini Taifa hili linauwezo wa kuwa kama Taifa lolote lingine kubwa. Ni umoja wetu na nia yetu ya kutofifia ya kuleta mabadiliko ya maisha yetu.

Ni muhimu wazazi wa taifa hili kuwa wamoja na kutilia mkazo jinsi tunavyowakuza watoto ambao ndio viongozi wa baadae. Baadae ya taifa hili iko chini ya vizazi vijavyo pia. tukijitayarisha Taifa hili nina uhakika lina uwezo wa kuwa miongoni mwa mataifa makubwa. Ni kujipanga tu na jitihada zetu. Ni lazima tuwe Taifa la watu wenye Malengo.

Ni lazima tufuate njia iliyo salama njia hii hapana tutapigana wenyewe kwa wenyewe. Amani ya nchi ikitoweka ni vigumu kuirudisha. Furaha haitokani na wingi wa mali alizonazo mtu akizungukwa na maskini kibao bali furaha ya Taifa hutokana na mafanikio ya pamoja.

Tunauwezo wa kuwa Taifa imara kama tukipendana na kuchukuliana kama ndugu ambao hatma yao ni moja.

Ni lazima tunyanyuane wenyewe kwa wenyewe. Roho ya Taifa hili lazima inyanyuke upya. Kama sisi ni Taifa sisi ni ndugu. Enzi za utawala wa kisultani wa kutawala kwa kujinufaisha lazima uishe ije enzi ya kutumikia, enzi ya uongozi na heshima. Enzi za viongozi na wananchi kuwa kitu kimoja.

Taifa hili linahitaji mabadiliko makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kama nilivyoongea katika maandiko yangu mengi kuhusu familia naipa nafasi kubwa sana katika uwezo wake wa kujenga Taifa imara.

Kama wazazi wakiwa na uwezo wa kutawala nyumba zao na kuweka nidhamu kwa watoto wao na kama wao wenyewe kwa wenyewe wakiwa na mahusiano mazuri na mashirikiano tutakuwa na uwezo mkubwa wa kutengeneza baadae yao kwa pamoja ili baadae na

wao wawe na majukumu ya kutengeneza baadae nzuri kwa wanaokuja. Ni lazima tujue kwamba familia ni sehemu ndogo ya Taifa. Uongozi mbovu unatokana na familia mbovu tulizo nazo. Watoto wetu wanakuwa kama uyoga bila nidhamu. Taifa hili ni kama mbegu zilizomwagwa shambani bila mpangilio, mazao yakakua ovyo ovyo. Taifa haliwezi kuendelea hivyo.

Ni lazima tuanze na mabadiliko ya watu. Ni lazima tuanze na fikra na maadili ya watu. Ni lazima tuzingatie umuhimu wa familia na mpangilio pamoja na utaratibu katika jamii. Watu wanafikiri kwamba pesa ni kila kitu. Wanatafuta hata kwa njia zisizostahili hata kama zitatugawa na kuweka rehani baadae yetu kama Taifa.

Kama tutakuwa na fikra hizo Taifa hili halitokalika kama tukifikiri kwamba utu wa mtu unatokana na mali alizonazo hatutakaa pamoja kutakuwa na mihangaiko isiyoisha tutapigana tu, ujambazi utaongezeka na uuzaji wa madawa ya kulevya.

Tukifikiria kuhusu vitu kwamba thamani ya mtu hutokana na vitu alivyonavyo. Ni muhimu thamani ya mtu itokane na yeye alivyoleta mabadiliko katika jamii yake. Tunauwezo wa kupambana na rushwa tukiwa na mtazamo tofauti. Hatutaweza kujenga jamii zetu katika misingi ya uovu.

Ni aibu kwa kiongozi kuwa mwizi badala ya kuleta mabadiliko katika taifa lake. Au kufikiri kwamba nafasi ya uraisi au uongozi mwingine ni nafasi ya umaarufu usio na tija na kufanya anasa.

Mtu anayefikiri akipata Urais amepata nafasi ya kufanya anasa ni lazima atapoteza mwelekeo wa uongozi wa Taifa, atajihatarisha mwenyewe na taifa

lake lote. Huwezi kuleta utaratibu na amani katika Taifa kama unapenda starehe.

Akili ya kiongozi lazima iwe makini wakati wote ni muhimu viongozi kujiepusha na starehe za aina zote. Akiendekeza starehe kuna hatari ya watu anaowaongoza kuwa watumwa wake, badala ya kuwatumikia, ataliongoza taifa katika macho ya ubinafsi wa kujiridhisha yeye na watu waliomzunguka. Nidhamu itapotea na taifa litajaa ufisadi badala ya mpangilio, utaratibu na haki.

Kutokana na kukosekana kwa uongozi wenye maono sasa hivi na kukosekana kwa maadili kwa vijana waliopo na kama hatua thabiti hazitachukuliwa na kama watu wenye maono na busara hawatapewa nafasi natabiri uongozi wa baadae utakuwa katika hali ngumu kuwaleta watu pamoja.

Ni wakati sasa wa kubadili fikra zetu na aina ya maisha tunayoishi. Tufikirie Utaifa na sio ubinafsi. Ili tulilete taifa katika umoja na mwelekeo sahihi tunaopaswa kupita kama taifa.

Historia ni mwalimu mzuri sana anatufundisha mambo kutokana na makosa binadamu waliyowahi kuyafanya na kupata madhara. Tusipozingatia historia madhara yatatupata.

Mataifa mengi yaliangamia baada ya kuacha yale mambo ambayo yamewaunganisha watu kama taifa na kuingia katika ubinafsi. Watu kujiangalia wenyewe badala ya kuliangalia taifa lao na kulijali. watu kutaka kuwa juu ya wengine badala ya kujishusha kuwatawala na kuwaongoza katika njia zinazofaa. Kuwa wamoja na wananchi badala ya kujitenga na kuwatumia pale tu unapowahitaji wakati

wa uchaguzi, kisha baada ya kuchaguliwa unawaswaga kama ng'ombe.

Haki za watu lazima zisikilizwe na utawala wa haki lazima uimarishwe. Watu lazima wawe wamoja na wenye muelekeo mmoja. Lakini bila ya uwepo wa haki jamii na taifa haliwezi kuwa moja. Uongozi wa kutumikia watu ndio msingi wa maendeleo. Hatuchagui serikali ili wawe mabwana wetu bali watutumikie, walete maendeleo yetu na wasimamie haki ili kuleta utulivu na amani. Hakuna maendeleo katika taifa lolote kama misingi ya haki haisimamiwi.

Kama taifa tunatakiwa tuwajenge raia waaminifu ambao watatimiza majukumu yao kwa uaminifu na kujitolea ili kuona taifa lao likiendelea. Na kuwa na viongozi wasio na choyo watakaotimiza majukumu yao bila hiyana kuona taifa hili likiendelea na watu wetu maisha yao yakiboreka, wakiwa na afya nzuri ya kiakili, kimwili, kiroho pamoja na utulivu kisha maendeleo ya mali. Kwasababu maendeleo ya mali bila utulivu wa hivyo vitu vitatu sio maendeleo.

Ni muhimu kutumia busara katika kufanya maamuzi yetu ili taifa na kizazi chetu kiendelee kuwepo na tupate maendeleo. Ni muhimu kwa vijana wetu na watu wetu wengine kutokukimbilia uongozi. Mpaka hapo kwanza watakapojenga nidhamu ya kutosha na maadili ya kuweza kuongoza watu. kwasababu kiongozi lazima atayarishwe kuwa na nidhamu, busara na hekima ya kuongoza watu. Awe na uwezo wa kulinda maneno na matendo yake, ayaongoze vyema kwenye muelekeo ambao utalifaidisha taifa.

Mtu mwenye akili haombi watu naomba niwaongoze, bali watu wenyewe huona mtu bora anayefaa kuwaongoza kwasababu wanamuamini kupitia yeye watapata haki zao na atakuwa mwamuzi bora kwao

na watafikia maendeleo yao kama yeye akiwa kiongozi wao . Anajua wajibu wa uongozi ukoje. Anajua amebeba matumaini ya watu walio wengi. Maendeleo yao, haki zao na hata hatma ya taifa lake kwa kiasi kikubwa inamtegemea yeye.

Amani na usalama wa taifa lake unamtegemea yeye na anayajibika kujitolea kila kitu chake kwaaajili ya ulinzi, amani na maendeleo ya taifa lake. Anawajibika kutimiza wajibu huu pasipo hofu kwa moyo wake wote.

Lakini hawezi kufanikisha hili pasipo kupenda watu wake. roho yake lazima isiwe na choyo na akili yake lazima isiwe na mashaka.

Dhamira yake nzuri kwa watu wake huboresha taifa. Mapenzi kwa taifa na kwa familia ni wajibu wa kila mtu anaotakiwa aukamilishe kwa akili yake yote, nafsi yake na roho yake. Raia wa nchi yoyote ile wanawajibika kulipenda taifa lao na kulitumikia.

Kama tusipolipenda taifa letu hatutakuwa na uwezo wa kulijali. Tunajali vitu tunavyovipenda. Ni lazima tuje kwenye uelewa huu; kwamba hili taifa ni letu wote na kwa pamoja tunawajibika kulijenga, kulitunza na kuliboresha. Hatuwezi kutimiza hili kama sisi wenyewe kwa wenyewe hatupendani au kama kuna migawanyiko. Ni lazima tuangaliane wenyeweb kwa wenyewe kama ndugu. Raia mwenzako ni ndugu yako.

Kiongozi yeyote anayekimbilia uongozi hafai. Mara nyingi kiongozi bora ni yule asiyetaka uongozi, hufuatwa kutokana na matendo yake ambayo yanaonekana ni mfano kwa jamii hasa ushupavu wake, busara yake na matendo yake ya haki. Huo ndio uongozi unavyokuwa. Wengine wote ni watu wa

maslahi na ni chui waliovaa ngozi ya kondoo. Matendo yako ndio ambayo yakufanye watu wakuhitaji uwe kiongozi wao.

Kukimbilia uongozi kunatokana na uovu, mtu bora yeyote hatokimbilia uongozi. Mara nyingi huonekana wakati taifa lina matatizo makubwa mpaka inakuwa hamna njia nyingine kwa jamii yake kuokoka pasipo yeye kuingia kwenye uongozi.

Nasema hivi kwasababu mazingira yaliyopo ya sasa hayamvutii kiongozi yeyote bora kutaka kugombea uongozi kutokana na aina ya siasa iliyopo. Siasa ambazo zinakosa hoja za msingi zaidi ya kushambuliana, kejeli, fitna, hila na kukashfiana na wakati mwingine kutukanana.

Kwasababu kiongozi anahusika na mahusiano ya watu busara kwake ni kitu cha muhimu kuliko kitu kingine chochote. Hakika hatoweza kufanya maamuzi yeyote ambayo yatawaleta watu pamoja kama hatakuwa na busara.

Kuwaleta watu wa mitazamo tofauti ya kiimani au kiitikadi kuwa kitu kimoja na kuishi kwa amani sio kitu cha mchezo. Ni busara ya hali ya juu inahitajika. Ni busara hii ambayo ikikosekana huweza kuligawa taifa.

Pale viongozi wanapojisahau na kuwa wafanyabiashara badala ya kuangalia mahusiano ya kijamii katika taifa husababisha migawanyiko.

Taifa letu linapitia katika majaribu makubwa mno kwasasa, inahitajika akili zilizokomaa na zenye busara na hekima kusuluhisha mengi ya matatizo yetu ya kijamii na kisiasa. Matatizo haya yote yanatokana na

watu kukimbilia uongozi sababu ya mali na kutokuwepo na busara kiuongozi.

Ikifika wakati ambapo watu wanatafutwa ili waongoze jua hapo tutapata viongozi bora sio hivi sasa watu wanakimbilia na kujipeleka kuwa viongozi. Hapa namaanisha watu wanatafutwa miongoni mwa watu wao bora na kuombwa kuingia kwenye uongozi badala ya kujipeleka kugombania. Kwasababu taifa lazima liwe na viongozi wawe wabaya au wazuri.

Watu ni lazima wapende kufanya kazi zao wenyewe na waachiwe wale ambao kweli wana karama ya uongozi ambayo inaonekana dhahiri miongoni mwa watu. Hii ni kwa faida na amani yetu wenyewe. Uongozi ni jambo gumu na hatari. Ni jambo linalohusu uhai wa watu.

Ni lazima tutafute dereva bora ambaye atafikisha safari yetu salama na sio bora dereva. Watu hutafuta dereva bora ambaye watakuwa na uhakika wa safari yao na sio dereva yeyote.

Taifa hili likiendelea kuchagua watu ovyo kwa rushwa na bila kuzingatia maadili ya mtu watambue kwamba baadae ya taifa hili iko hatarini. Baadae na amani ya taifa hili italala kwenye umahiri, ushupavu, hekima na busara za viongozi.

Ili watu wawe viongozi ni lazima watu wawe na karama hizo za uongozi sio kama sasa hivi watu wanaacha kazi ambazo ni muhimu kwa taifa kama uprofesa na kukimbilia kwenye siasa, naamini kila mtu anaweza kutoa mchango wake kwa taifa huko huko aliko.

Na kwa kufanya hivi taifa letu litaendelea zaidi. Watu wengi huingia kwenye siasa sababu ya uchu wa

madaraka na fedha bila ya kuwa na karama ya uongozi. Na karama hizo ni kuwa mtenda haki, mwenye busara na shupavu. Vitu hivi vitatu ni muhimu mno kwa kiongozi yeyote yule. Kwa haki atawaunganisha watu pamoja, kila mtu atapatastahili yake. Kwa busara atafanya maamuzi sahihi kwa wakati sahihi.

Na kwa ushupavu atailinda nchi. Kwa hivi vitu vitatu atatawala na kuliongoza taifa katika ustadi mkubwa. Kwahiyo udhaifu wa nchi yeyote ile asili yake ni udhaifu wa viongozi wake na kinyume chake pia ni sahihi. Busara bila ushupavu kwa kiongozi atakuwa bado hajakamilika kutokana na uasili wa binadamu kuwa waovu na ili haki iendelee kuwepo ni lazima kiongozi awe jasiri wa kufanya maamuzi yatakayoleta amani na utaratibu katika nchi.

Mara zote haki huletwa na ushupavu, busara hufanya maamuzi sahihi bila kumuonea mtu. Jambo jingine ni hekima, uwezo wa kuona mbali na kuweka mipango ya baadae kwa taifa.

Ni lazima tuwe na kiongozi anayeona zaidi ya leo na kuweka mipango ya baadae kwaajili ya kizazi kijacho. Kiongozi anayeweza kuyaona matendo tunayofanya leo na madhara yatakayotokea kesho na kuyarekebisha mara moja au kama ni bora kuyaboresha.

Kutoweka kwa busara na hekima katika taifa huleta vurugu na fujo na baadae ya taifa huwa hatarini. Taifa lolote linapokosa maono watu huangamia, ni lazima tufuate njia sahihi kwa kufanya maamuzi sahihi wakati wote kama taifa kwa ushupavu bila ya uoga. Kwa kufanya hivi taifa letu litapata dira na mwelekeo.

Kiongozi bora ni yule anayejua kuwapanga watu wake. Anayejua kutumia nguvu kazi ya nchi yake vizuri kuleta uzalishaji. Mwenye uwezo wa kuwaleta watu wake pamoja katika dhamira ya pamoja. Kiongozi mwenye ushawishi huu ndie atakaye litoa taifa letu kutoka hapa lilipo.

Katika taifa letu kuna kutokuridhika kukubwa miongoni mwa wafanyakazi wa serikali tunahitaji kurudisha mori na mapenzi yao kwenye kazi na taifa. Bila mapenzi haya kwa taifa hatutaweza kupiga hatua ya kimaendeleo.

Mambo yote haya ya kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati wote yanahitaji akili zilizo komaa na zilizo tayari kujitolea kwa faida ya jamii na taifa kwa ujumla. Hatutaweza kuacha ukweli na kukumbatia uongo tukapiga hatua kimaendeleo, na wala hatutaendelea kwa kukumbatia potovu na kuacha adili aende zake.

Wakati wenzetu wanahangaika kutafuta usuluhishi ndani ya nchi zao kutokana vita na kutoelewana ni lazima sisi tujifunze kutoka kwao na kuchukua hatua ili tulilinde hili taifa. Sidhani kama tungependa tufikie hatua hiyo wakati tuna nafasi kubwa ya kukabiliana na changamoto zinazotukabili kama ndugu na kufikia muafaka juu ya mambo mengi yanayotuhusu.

Ni vizuri kuwa makini sana na jinsi tunavyoendesha taifa letu tu, ili tusisababishe matatizo kwa kizazi kingine ambacho wao watakuwa hawana makosa. Angalau tufanye hivi kwa ajili kizazi kijacho. Ni lazima tulipokeze taifa hili kwa kizazi kingine katika hali bora. Sio katika hali mbaya ambayo itabidi sasa wahangaike kulirekebisha kutoka katika udini, ukabila na ubaguzi wa kimatabaka.

Tulikabidhi taifa hili likiwa kwenye utengamano na likiwa moja.

Ni lazima tuwe wamoja hili ni jambo la muhimu sana, ili taifa letu liendelee. Ni muhimu tuwe na haya maono ya utaifa. Kwamba sisi ni watu ambao mwisho wetu ni mmoja na kufanikiwa au kushindwa kwetu ni ku moja. Ni lazima tufanye kazi sasa ili kuliendesha hili taifa ni lazima tulipende na kulitumikia.

Tabia ya kulitukana na kulikashifu wakati ni taifa letu wenyewe ni lazima iishe. Ni lazima tuwe na mtazamo chanya kuhusu taifa letu. Ni lazima sasa tuwe na mawazo chanya yatakayo saidia kulijenga taifa hili. Hatuko wamoja katika mawazo yetu ndio maana hatuendelei, tumekata tamaa juu ya taifa letu. Tunalalamika, kila mtu analalamika. Tunalilaani kwa midomo yetu wenyewe.

Lakini ni wajibu wetu wa kugeuza fikra zetu na kuwa na fikra za pamoja za kujenga taifa hili na kuliendeleza, hili ni jukumu la kila mmoja wetu. Ni lazima tulipende taifa letu kwakuwa pasipo kufanya hivyo tutakuwa hatuna nguvu ya kulijenga.

Tabia tulizokuwa nazo za wizi na kutojali mali za umma ni lazima ziishe, tuzingatie umuhimu wa utaifa. Kwasababu tabia hizi ni za hatari na hazina faida kwetu kama taifa. Ni muhimu kubadilisha mwelekeo wetu kama tunataka kujenga jamii bora na endelevu.

Jambo hili la uzalendo kwa taifa letu halitaletwa na jeshi la kujenga taifa. Bali mahubiri ya mara kwa mara na msisitizo juu umuhimu wa taifa hili kwetu na kwa viongozi wetu kutenda yaliyo ya haki na sahihi kwenye macho ya jamii.

Kwa kuonyesha kwao mfano kwa uzalendo taifa letu litarudi kwenye uzalendo wake. Na uzalendo huu utaonekana kwa kujali maslahi ya umma kwanza kabla ya yale ya kibinafsi. Kwa kuangalia nguvu kazi yake kwa ukaribu kwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi sio kujiongezea maslahi kwa viongozi. Huu sio mfano mzuri kwa umma ikiwa viongozi wanajirudikia maslahi na ufisadi viongozi ni lazima waache huu unafiki kama wanataka uzalendo urudi katika taifa.

Kiongozi ni kama mwendesha farasi akiwa bora atamwendesha farasi katika mwelekeo maalumu lakini akiwa hajui kumweka sawa farasi atayumbishwa ni lazima ajue kumshika vizuri farasi na kumwelekeza sehemu ya kwenda. Kiongozi mbovu husababisha farasi kukosa mwelekeo.

Wananchi wanapokosa viongozi wazuri hukosa mwelekeo kama taifa. Nchi hukosa utaratibu na mpangilio. Matumaini ya waliowengi hupotea.

Ni lazima siasa zetu ziendane na mantiki pamoja na dhamira ya dhati ya kulisongesha taifa letu mbele na sio porojo. Wanasiasa wetu wawe wazalendo na kuamua yale yaliyo bora kwa manufaa ya taifa. Pale tu siasa zetu zitakapokuwa na mantiki watu wetu wengi watarudisha hisia za uzalendo kwa taifa lao na watakuwa tayari kwa kulitumikia.

Siasa ni chombo pekee ambacho kitatusaidia kuharakisha maendeleo yetu. Pale siasa inapokuwa nzuri katika nchi, maendeleo ni lazima yaje. Ni siasa pekee inayowaunganisha watu katika malengo mamoja ya utaifa na kuleta mwelekeo. Inapokuwa nzuri huwa na tija kwa wanachi wote. Lakini inapokuwa mbaya huleta fujo na mgawanyiko.

Ni kweli kwamba mawazo yetu hujenga na kukusanya, lakini pia hubomoa na kutawanya, kwa kila neno linalotoka mdomoni mwanadamu ni lazima awajibike nalo kwani lina madhara au faida.

Kwahiyo kujitambua kwa wanasiasa ni muhimu sana. Kujitambua wanajenga nini na kudhibiti kauli zitakazoleta mgawanyiko. Kuna nguvu kubwa katika maneno yetu ni muhimu wote kutambua.

Kwahiyo kiongozi mzuri ni yule anayechagua maneno yenye faida na yanayojenga taifa, anayejua kuelekeza katika njia iliyo sahihi, anayeongea masuala ambayo yataonekana dhahiri ni yenye mantiki katika macho ya raia. Mwelekeo wa taifa hautapatikana kama viongozi wetu hawatokuwa na mwelekeo na kujua ni nini wanajenga na ni nini cha kuongea. Mkondo wa mawazo ya viongozi mara nyingi huwa mkondo wa wananchi. Wananchi hukosa dira pale viongozi wanapokosa dira.

Mawazo ya wananchi ni lazima yaelekezwe katika mwelekeo fulani, kazi ya kuelekeza mawazo haya ni kazi ya viongozi, bila raia kuelekezwa katika mkondo fulani wa mawazo hakika hatutaweza kupata mafanikio, ikiwa mawazo ya wananchi wetu yakiwa yametawanyika na bila kuwa na mwelekeo fulani.

Ni muhimu kutambua hili taifa ni lazima liwe na malengo. Malengo haya ni lazima yapandikizwe katika kila moyo na akili za mwananchi. Wajenzi wa taifa hili ni wananchi, viongozi wasifikiri watawaletea maendeleo wananchi bila wananchi kushiriki katika ujenzi wa taifa lao wenyewe.

Wakumbuke wao viongozi ni waratibu tu lakini kazi kubwa ya ujenzi wa taifa hufanywa na raia wenyewe.

Na ulinzi wa maliasili na wa taasisi zao ni jukumu lao. Ni lazima wajengewe wajibu huu kwa taifa lao. Ni lazima wahisi hili ni taifa lao. Na jukumu la kulipeleka taifa hili mbele ni la kila mmoja.

Wakiisha jengewa wajibu huu na kuufahamu kisha kujielewa kwanini tuko taifa na kwa faida gani, wanawajibu gani kwa taifa na kwa jamii, itakuwa rahisi kwao kulinda mali za umma na kuzipenda taasisi zao zinazo wahudumia.

Wakijitambua itakuwa rahisi sana kushinikiza sheria ili kulinda utaratibu. Hisia hii ya raia kwa taasisi zao ni muhimu, hisia ya mapenzi na kujitolea ili kuona taasisi zinazohudumia raia zikiendelea.

Pasipo kujitambua huku na elimu hii ya uraia tutawafunga wengi na wizi na ufisadi utaendelea. Wajibu huu wa mtu kwa jamii yake na taifa lake, ni muhimu sana. Wakielewa taasisi hizi ni mali yao na zipo kwa faida yao na kwa vizazi vijavyo nafikiri mtazamo wao utabadilika.

Ni lazima wajue taasisi zote sio mali ya serikali ni mali yao. Wana wajibu wa kuzilinda na kuziendeleza. Tujenge wajibu huu katika jamii yetu. Binadamu ni lazima awajibike kwa jamii yake. Kutoweka kwa nidhamu hii ndio chanzo cha mambo mengi. Na taifa letu limekosa pia utaratibu sababu ya nidhamu hii kutoweka.

Haya ni mambo ambayo ni lazima tufanye ili taifa letu lirudi katika mstari. Ni kwa kuwajibika huku kwa jamii ndipo tutakapojenga jamii iliyobora. Kukikosekana kuwajibika huku hatutafika mbali kama taifa.

Kukiwepo na kuwajibika huku hakuna mtu atakayemuuzia mwenzake bidhaa bandia mfano; hata kama kukiwepo basi kutakuwepo kwa kiwango kidogo katika jamii ya watu wanaotambua wajibu wao au kutokuchukulia maanani majukumu aliyopewa na jamii katika nyanja mbali mbali. Iwe mwalimu, daktari au mhandisi. Tukiisha wajengea wajibu huu watu wetu.

Itakuwa rahisi kwao kufuata sheria. Pasipo elimu hii, raia wetu watakuwa waoga tu wa sheria lakini wakipata nafasi ya kufanya uhalifu watafanya. Kwahiyo ni muhimu kujenga na kutoa elimu hii ya uraia kwa watu wetu ili wajitambue na kutimiza wajibu wao. Serikali haiwezi kufanya kazi peke yake bila ushiriki wa dhati wa wananchi kulinda na kuliendeleza taifa lao na bila wananchi kutimiza wajibu wao.

Bila kuwafanya raia wa nchi yetu kuwa wenye kutimiza wajibu wao bila kusukumwa hatutafika. Na hili linahitaji nidhamu ambayo tunapaswa kuwajengea. Kwahiyo elimu ya uraia ni muhimu sana ili kuwafanya watu wa taifa hili kujitambua kuelekea kwenye utaifa wao kutoka kwenye ubinafsi.

Ni lazima tufahamu ujenzi wa taifa ni wajibu wa raia wote, taifa huimarika pale raia wote waposhiriki katika ujenzi wa taifa lao, uedelezaji wake na ulinzi wake. Taifa hili litaendelea kuwepo ikiwa watu wote watashiriki katika ujenzi wake kwa kujitambua.

Watu wenye mawazo bora ni lazima washiriki katika kufanya taifa hili liwe bora zaidi na la kuvutia. Ni kwa mawazo chanya pekee ndipo tutakapo lijenga taifa hili.

Ni kwa watu ambao wanajadili njia za kutatua matatizo yaliyopo sasa hivi ili kuleta maendeleo ndio watakao linyanyua taifa hili, sio watu wanaojadili kila wakati matatizo ya taifa. Ili tulijenge taifa hili kwa ustadi ni lazima tulipende. Upendo huu kwa taifa ndio utakaotufanya tuwe na juhudi zaidi na ubunifu zaidi kusudi lipendeze.

Ni lazima tusahau yaliyopita na tuangalie ya mbele sasa hivi, tujenge taifa zuri zaidi kwa kuwa na mawazo mazuri zaidi na chanya juu ya taifa letu.

Ni lazima tusahau mgawanyiko wetu na kuleta umoja katika malengo. Ni lazima tukusanye mawazo yetu na tuyaekeze katika mkondo uliobora zaidi wa kufanya taifa hili liwe zuri. Tunaweza kufanya hivi kwasababu mawazo yetu ndio yanayojenga. Ubora wa mawazo yetu ndio ubora wa taifa.

Ni muhimu kufahamu kama taifa letu lina magugu ni kutokana na fikra na mawazo yetu mabaya. Fikra na mawazo mazuri hutengeneza taifa zuri. Tunachohitajika sasa hivi ni kubadilisha fikra na mawazo yetu ili tujenge taifa imara na lililobora.

Taifa ambalo mtu atafikiria jamii kwanza kabla hajafanya kitu chochote. Tukifika huko tutakuwa tumekomaa kiakili na tutajenga taifa imara la watu wanaoshirikiana kuleta maendeleo yao wenyewe.

Kubadilisha fikra hizi na kuleta fikra mpya na chanya juu ya taifa letu kunahitaji juhudi kubwa na kazi ambayo tunahitajika kuifanya bila kuchoka ili kizazi kijacho wakute taifa la watu wenye mtazamo uliobora kuhusu taifa lao. Kwa kuwajengea aina hii ya mtazamo juu ya taifa lao itakuwa hatua kubwa kwetu ya maendeleo.

Lakini pia kwa kujenga taasisi za kijamii imara na zinazowajibika ili kudai haki za wananchi kila mara pale zinapokiukwa. Kwasababu pasipo raia kupata haki katika taifa lao hawatoweza kuwa na mtazamo ulio sahihi kwa taifa. Taasisi hizi ni lazima ziwe za watu wanajitambua na wazalendo na sio taasisi za watafutaji.

Taasisi ambazo zitaweza kuwahudumia wananchi vizuri kwa wakati, kwa maadili na nidhamu. Taifa lisilokuwa na ndihamu ni taifa la watu wasiokuwa na dira ya wapi wanapotaka kufika kama taifa. Chochote kile tunachokihitaji kama taifa hatutaweza kukifanikisha kama hatuna nidhamu.

Ujenzi huu wa jamii imara hautakuwepo tusipofanikiwa kuiondoa rushwa ambayo ndio kikwazo kikubwa cha maendeleo na utoaji wa haki kwa watu.

Mabadiliko yeyote makubwa katika jamii yetu hayatopatikana pasipo kuiondoa rushwa. Sheria zozote hazitokuwa na maana wala kuleta mabadiliko kama rushwa itatamalaki. Na malengo yetu ya kuibadilisha jamii yetu itakuwa ni kazi bure. Kwahiyo misingi ya haki ni muhimu kuimarishwa ili taifa letu liendelee. Juhudi zetu za kuondoa rushwa na ufisadi lazima ziimarishwe.

Kusimamia yote haya inahitaji kiongozi shupavu na mwenye nidhamu na maadili ya kutosha ili kuleta nchi katika mstari. Ili kuleta heshima katika nchi yetu, heshima hii ni muhimu sana kwa wananchi. Kama tutapuuzia maisha haya ya kijamii na kuendekeza rushwa na ufisadi ambao kwa uhakika unagawa taifa, sisi kama jamii hatutaweza kuwa na furaha ikiwa tutapuuzia misingi hii ya haki.

Malengo yetu ni lazima yawe kujenga jamii bora na yenye utaratibu hatuwezi kufikiria kuhusu uchumi pasipo kujenga mambo haya ya msingi ambayo yatapelekea kupata dira na utaratibu katika nchi na matokeo yake yatasaidia kujenga uchumi uliobora na jamii yenye mpangilio.

Kama tukifanikiwa kupanga na kuratibu nguvu kazi yetu vizuri ili ifanye kazi kwaajili ya manufaa ya nchi itakuwa hatua kubwa kwetu. Ni katika jitihada hizi pekee ndipo taifa hili litafanya kazi. Jitihada hizi pekee za pamoja zitalisongesha hili taifa ikiwa kila mtu atawajibika ipasavyo, ikiwa tutafanya kazi kwa pamoja kama gari na kila kifaa chake, gari hutembea ikiwa kila kifaa ndani yake hufanya kazi ipasavyo.

Katika kizazi chetu tuna wajibu, wajibu huu mkubwa wa kulisongesha taifa hili mbele. Tutalisongesha ikiwa tutakuwa wamoja na ikiwa tutaweka jitihada zetu kuona taifa hili likinyanyuka. Ni katika roho hii ya kujitolea ya kuona jamii zetu zikikua na kuendelea, tutaweza kutoka hapa tulipo.

Bila uzalendo hatutaweza kulinyanyua taifa hili, bila kutambua sisi ni wamoja na mwisho wetu ni mmoja kama taifa hatutaweza kutoka hapa tulipo.

Bila ya kujenga taifa la watu wanaowajibika kwa jamii na kwa taifa ni vigumu sisi kuendelea. Taifa hili kamwe halitojengwa katika ubinafsi bali katika jitihada za pamoja, katika upendo na katika juhudi zisizofifia za kuona maisha ya binadamu yakiboreka na taifa letu likinyanyuka kutoka hapa lilipo. Ni katika tumaini hili pekee taifa letu litapata uhai wake.

Tubadilishe hizi tabia ambazo zimemea miongoni mwetu kizazi hadi kizazi. Tubadili mtizamo wetu kutoka katika ubinafsi kuja katika utaifa. Bila raia

kujitambua kwenye utaifa wao na kujua malengo yao na madhumuni yao ya kuwa taifa hakuna maendeleo makubwa tutakayofikia. Muda umefika sasa wa kuweka taifa mbele na kuacha ubinafsi. Tutaendelea ikiwa tu tutafanya kazi pamoja kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

Hakuna nguvu kubwa kama nguvu ya umoja, kama nguvu ya jamii iliyoamua kuleta mabadiliko. Kama nguvu ya jamii iliyochoka na na matatizo na kuamua kutumia nguvu, akili na maarifa kupambana kuleta mabadiliko. Ni katika mtazamo huu na roho hii tutalisongesha taifa hili.

Ni lazima tuwe na ndoto hii kwamba tunauwezo wa kubadili taifa hili, kwamba ufunguo wa maendeleo ya taifa hili uko mikononi mwetu na ni wajibu wetu kufungua au kufunga mlango wa maendeleo. Kazi hii ya ujenzi wa taifa hili ni kazi ya kizazi baada ya kizazi.

Kama tukitia juhudi kizazi baada ya kizazi, kama tukiwa na dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko mafanikio yatakuwa yetu. Mambo haya yanahitaji ukweli wa nafsi na dhamira ya dhati ya kutaka kuona taifa letu likibadilika.

Ni katika mwelekeo huu wa mawazo taifa letu litapiga hatua. Hakuna kitu chochote kitakachotuletea maendeleo zaidi ya umoja wetu na utayari wetu wa kuleta mabadiliko. Kila mtu ni lazima afanye kazi kwa bidii, ili kuleta mabadiliko ya maisha yake na yale ya taifa. Roho hii ya uzalendo tusipoijenga hatutofika popote kama taifa.

Lazima iwe mwisho kwa taifa hili kuwa la mashaka, kwa taifa hili kutokuamini, kwamba tuna nguvu ya kuleta mabadiliko kama tukifanya jitihada, kama tukitoa jasho, kama tukiwa wamoja katika

jitihada zetu kupambana na ujinga, maradhi na magonjwa, na kwenda mbele zaidi kuleta maisha ya ushindi na matumaini, kulifanya taifa hili liwe bora na kubwa duniani. Ni juhudi zetu tu ndizo zitakazo fanikisha hili. Ni lazima tufanye kazi kwa bidii.

Ni lazima tuamini ni lazima tuwe taifa latu watu wanaoamini, tunaweza kufanya kitu katika uso wa dunia. Tuna nguvu hii ya kuleta mabadiliko. Hakuna mlima ambao hautasazishwa ikiwa tutakuwa na nguvu hii ya kuamini. Kuna nguvu katika uwezo wa akili ya binadamu ikienda sambamba na imani yake kwamba hakuna kitu chini ya jua binadamu atashindwa kama akidhamiria.

Hata kama hatutaiona kesho tutaendelea kuamini kama kuna jitihada na kama kuna dhamira kutoka katika mavumbi taifa letu litanyanyuka. Ni lazima tudhamirie ni lazima tufanye hii dhamira kuendelea kuwa hai. Dhamira inapokuwa kubwa hadi binadamu kutokujali kifo ili mradi afanikishe malengo yake, na ikiwa malengo yake ni yenye haki na adili, ingawaje hata kama akifa hajafanikiwa, taswira ya dhamira yake itampa matumaini siku zote pamoja na furaha.

Tumechoka kuzungumzia matatizo kizazi hata kizazi, ni wakati sasa wa kuongelea suluhu ya matatizo na kutenda. Matatizo hayatoondoka kwa kuongea tu, yatatoka kwa kufanya kazi, kwa kufanya jitihada wote kama taifa ili kuona jamii zetu zikiendelea.

Sisi kama taifa hakuna njia ya mpito kuelekea katika maendeleo. Ni lazima tuhenyeke, ni lazima tupate tabu, ni lazima tuvumilie lakini tukiwa na matumaini na kutia juhudi katika kila nyanja ili kuleta maendeleo yetu wenyewe.

Tufanye kazi mara tatu ya watu wengine wafanyavyo duniani. Kama tunahitaji kukua kama taifa ni lazima kuwepo na kujitolea huku. Hakuna sehemu yeyote duniani ubinafsi ulijenga taifa. Uzalendo ulijenga mataifa, dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo ilisukuma mataifa mengi kunyanyuka kutoka katika matope kufikia kwenye kilele cha mafanikio. Ni lazima tujenge taifa wafanyakazi hodari. Ni lazima tubadilishe tabia za watu wa kizazi hiki kuwa za watu wenye nidhamu na jitihada katika kazi.

Tujenge kizazi cha watu wasio wababishaji, wakweli, wavumilivu katika utafutaji maarifa na kufanya kazi. Iwe kazi ya mikono au kazi ngumu za kutumia akili.

Kwa nchi yetu ambayo ni maskini ni muhimu kutokuwa na muda wa kustarehe bali wa kufanya kazi. Na serikali ni muhimu kujenga mazingira bora kwa kazi hizo kupatikana.

Inaonekana kama kwenye taifa hili hatuoni njia ya kupita kama taifa. Kila mtu analalamika, hakuna anayeonyesha njia. Kulalamika ni dalili ya uvivu uwe wa kimwili au kiakili. Watu wanaotaka maendeleo hutenda badala ya kukaa na kulalamika. Watu wanataka kuona hatua zikichukuliwa ndio faraja yao.

Kuna maendeleo ambayo yapo; sisemi kwamba hakuna maendeleo ambayo yamefikiwa, lakini tungeweka jitihada zaidi kwa pamoja tungefika mbali kuliko hapa tulipo. Tatizo letu tumegawanyika katika mawazo yetu. Viongozi wetu wanafanya kazi nzuri wanajitahidi lakini tunahitaji maendeleo zaidi ya hapo tulipo kwa hivyo tunalazimika kuongeza jitihada na kuhamasisha watu kujiletea maendeleo yao wenyewe na kujenga umoja wan chi.

Ni lazima tuhamasishe jitihada hii shuleni, vyuoni na kwa wananchi. Wajue wanawajibu kwa nchi. Taifa hili litaendelea ikiwa tu kila mtu atatia juhudi katika kufanya kazi na ikiwa kila mtu atakuwa mzalendo. Ni lazima tuwe na akili hii ya utaifa. Bila roho hii ya uzalendo na utaifa hatutoendelea.

Ni lazima tujitambue tujue tunafanya nini, wote sisi tunajenga nyumba moja kila mtu atanyanyua tofali moja katika ujenzi wa taifa hili. Taifa hili litakuwa bora ikiwa tutafanya kazi kwa pamoja na ikiwa tutashirikiana. Ikiwa watu na taasisi zao watashirikiana na kujua kwamba sisi ni watu wamoja na mwisho wetu ni mmoja.

Taifa hili tunahitaji kukua kiakili na kufanya yale sahihi na bora kwetu na kizazi chetu kijacho. Haya yote hatutaweza kufanikiwa pasipokuwa na familia bora, jamii bora na serikali bora. Pasipo kuwajibika sehemu zote hizo. Pasipokuwa na nidhamu sehemu zote hizo hakutakuwa na maendeleo.

Jamii iliyo pangiliwa vizuri taasisi zake hufanya kazi vyema na kwa faida ya umma. Jamii hii ambayo watu wanawajibika miongoni mwao na wana malengo mamoja waliunda taasisi za kuwahudumia.

Ikiwa kwenye jamii zetu kuna rushwa na ufisadi ni lazima turudi kwenye jamii. Ni lazima turudi kwenye jamii yetu inavyofikiri na mahusiano yao.

Ni lazima tubadilishe mwelekeo wetu wa mawazo kuhusu ubinafsi, na tuweke mbele jamii, tuunde upya mfumo wetu wa kijamii ambao utakuwa nguvu kubwa ya maendeleo yetu kama taifa. Bila kupangilia jamii yetu hatutaweza kupata maendeleo.

Familia zetu ni lazima zijengwe katika utaifa na katika uzalendo. Katika kila nyumba kwenye taifa hili ni lazima watambue wanaishi chini ya kivuli cha utaifa. Wanawajibika kwa taifa. Ni lazima turudishe wajibu huu. Hatuwezi kuendelea kuwa na jamii inayodai tu pasipo kuwa na wajibu. Lakini pia hatuwezi kuwa na serikali isiyowajibika ipasavyo kwa wananchi.

Hatuwezi kuendelea kuwa na serikali inayokumbatia ufisadi na rushwa na kuchochea kupotea kwa utaratibu katika jamii. Taifa hili litasonga mbele ikiwa tu kutakuwa na utaratibu katika nchi. Ni muhimu kwa nidhamu hii kurudishwa.

Bila kujenga jamii inayowajibika na wazazi wanaowajibika hatutaweza kuwaachia kizazi kijacho nchi hii ikiwa katika hali nzuri.

Ni muhimu kujenga upya wajibu huu wa kijamii. Ni ngumu bila ya kuwepo kwa raia ambao akili zao zimepevuka ambao wanaona mambo katika upeo mkubwa zaidi ya ule wa ubinafsi ule wa kulinda jamii na kuhakikisha inaendelea na kupokeza nchi hii kwa kizazi kingine ikiwa salama. Vijana na watoto wetu hii nchi ni mali yao ni lazima wajue hivyo. Pasipo kufahamu hivi hawatoweza kuilinda, kuiendeleza na kuitetea.

Kizazi hiki kitalipokeza taifa hili kwa kizazi kijacho, lakini bila juhudi hii ya kulilinda na kuliendeleza hatutafanikiwa. Bila kujenga wajibu huu sidhani kama taifa letu litakuwa salama. Ikiwa hatutajenga vijana wanaowajibika kwa taifa. Ni lazima wafahamu sisi ni familia moja kubwa. Ni wanachama wa familia kubwa ya watanzania.

Kama wanachama wa familia moja tumekumbwa na matatizo yaliyo igawanya familia tuna wajibu wa kuyasuluhisha ili kuleta taifa kwenye mstari. Kila mtu anajua jinsi gani ufisadi na wizi ulivyosambaratisha taifa hili.

Hatuwezi kusuluhisha matatizo haya kwa kupigana wenyewe kwa wenyewe bali kwa kuangalia chanzo cha matatizo yote haya yaliyopelekea ndugu kusalitiana. Tunataka kujenga jamii isiyokuwa na rushwa na ufisadi ni lazima tuanze upya.

Ni muhimu kutambua hatuwezi kuwa wote matajiri, ni lazima baadhi ya watu wawe watumishi wa umma na wajitolee kutumikia umma. Wajibu huu ni lazima uwepo ili taifa letu liende.

Haiwezekani mtu awe mwalimu wakati huo huo awe mjasiriamali, hatoweza kuweka akili yake yote kwenye utumishi wa umma, hivyo hivyo kwenye taaluma nyingine. Kama mtu anachagua kuwa mfanyabiashara ni lazima afanye biashara na wengine ni lazima wajibu wao uwe kutumikia umma.

Tutakapoacha wajibu huu kwa umma nani atafanya? Hili sio suala la mshahara tu bali ni suala la wajibu kwa jamii. Taifa hili litasonga mbele ikiwa tu tutafanya kazi kama kitu kimoja kila mtu katika sehemu yake. Ni lazima tujitambue na ni lazima tuwajibike kwa jamii.

Naamini kabisa kama serikali ikidhibiti mapato yake na kufanya matumizi mazuri ya pesa itokanayo na kodi, na kama watu wetu wakifanya kazi kwa bidii, serikali itakuwa na uwezo mkubwa sana wa kuwalipa wafanya kazi wa umma vizuri ili wafanye kazi kwa bidii na ufanisi. Taifa hili litafanikiwa kama tutafanya

kazi pamoja. Kama tukizalisha zaidi tutatoka hapa tulipo.

Ni lazima hili tumaini lirudi, tumaini kwa taifa letu pamoja na baadae yake. Naona uwezekano wa taifa hili kukua ikiwa tutarekebisha baadhi ya mambo yatakayotufanya tukae sawa kama taifa na kupata mwelekeo. Ni katika kujitolea huko pasipo ubinafsi kwa taifa letu ndipo tutapiga hatua kama taifa.

Ni muhimu kwetu kurudisha uzalendo kwa taifa. Pasipo uzalendo watu hugawanyika kila mtu akifuata la kwake, uzalendo huu unapokuwepo popote pale watu huwa wamoja katika malengo na dhamira. Na ni nguvu hii pekee husukuma mataifa mengi kuleta maendeleo. Bila nguvu hii taifa letu halitoweza kupiga hatua kimaendeleo.

Kwahiyo dhamira ya dhati ya watu kuona taifa lao likiendelea ndio ufunguo wa taifa lolote kupiga hatua. Sisi katika taifa letu hatujali hilo. Tunaongozwa na ubinafsi na dhamira za ubinafsi. Popote pale penye ubinafsi hakuna uzalendo. Uzalendo maana yake fanya kwaajili ya mwenzako fanya kwaajili ya taifa.

Ni lazima tujenge taifa ambalo raia wake wanajaliana popote pale walipo duniani. Ni umoja huu pekee utakaotufanya tufanye kazi pamoja kuliendeleza taifa letu na tupigane pamoja kulilinda.

Lazima tutambuane kama raia na kama ndugu. Tuwe na hisia sawa kama ndugu wa damu moja tukijenga jamii inayounganishwa na haki kwa wote. Haki hii inapokuwepo nchi huwa moja na inapotoweka nchi huwa vipande vipande. Uzalendo ni maana halisi ya kuliweka taifa pamoja katika dhamira moja na akili moja.

Kujitambua kwa taifa ni hatua ambazo taifa hupitia kufikia ufahamu wake. Kujijua wao ni kina nani na kujitofautisha na mataifa mengine. Ni tabia ambazo zimeundwa kwa watu wa taifa husika. Zinazotofautisha taifa moja na taifa jingine. Fikra na mtizamo wa taifa moja dhidi ya taifa jingine, ambazo zimelala kwenye tamaduni, mila na desturi za jamii husika. Ambazo zimemea kwenye akili na roho za jamii husika na kujenga tabia, matendo na maamuzi yao. Ni kufikia ufahamu wa pamoja kwenye utaifa.

Mfumo wa elimu ambao watu wa jamii husika hukuzwa na kulelewa iwe nyumbani au shuleni na kujenga tabia za watu na tabia ya taifa. Tabia ya taifa hutokana na mkondo wa mawazo wa jamii na taifa husika ambao hujengwa kupitia elimu pamoja na makuzi. Elimu na makuzi hufanya watu kuwa na tabia za aina fulani na imani ya namna fulani ambayo huumba tabia ya nchi kwa pamoja.

Ili taifa libadilike watu wake lazima wabadili mkondo wa fikra zao ambao hujenga taratibu, mila na desturi. Kwahiyo ni muhimu kujenga sasa fikra za watu wetu kuelekea kwenye utaifa na sio mbali na utaifa kwenye ubinafsi.

Hii yote huanza kwenye fikra. Roho ya taifa ni fikra, itikadi au imani inayotawala taifa kwa kipindi husika na kujenga mfumo wa maisha na taratibu katika nchi na hata sheria zinazowalinda na kuwaongoza. Na hii itikadi na imani ndio hutofautisha taifa moja dhidi ya jingine. Mambo wanayoyakubali au kuyakataa kama taifa, mila na desturi zinazowaongoza kufanya maamuzi kama taifa. Vitu vinavyowaunganisha kwa pamoja na kujiita taifa. Bila ya vitu ambavyo vinawaunganisha pamoja kama imani na itikadi ya pamoja, mila na desturi taifa haliwezi kujiita taifa.

Huu ni mchakato ambao taifa hupitia kufikia kujitambua kwake. Wakati akili za raia zinapokuja pamoja kwenye utaifa na kuwa na dhamira na malengo yanayofanana. Raia wanapojitambua kuelekea kwenye utaifa na sio mbali na utaifa; ndipo taifa hufanyika. Wanapokuwa na malengo ya aina moja na mikakati ya aina moja.

Hatua ya raia ya kujitambua wao wenyewe na kujitambua kwao kwenye utaifa wao, ni hatua kubwa na muhimu katika ukuaji wa taifa lolote. Muelekeo wa akili za watu kwenda katikati kwenye utaifa na sio kutoka kwenye utaifa na kwenda kwenye ubinafsi, ndio hufanya mataifa kuwa makubwa.

Kama binadamu anavyokuwa na roho kila taifa lina roho na nguvu ya taifa hupatikana pale raia wanapijikusanya kuelekea kwenye utaifa na sio mbali na utaifa kuelekea kwenye ubinafsi.

Na bila kuwa wamoja kwetu na wazalendo hatutajitambua, hatutafikia hatua ya kujitegemea na bila kujitegemea huku na kuwa kitu kimoja nakuwa na ufahamu mmoja na mwelekeo mmoja kamwe hatutafanikiwa.

Ni kama mbwa bila moyo, bila ini, bila utumbo hawezi kufanyika mbwa mzima anayetembea na kubweka. Ni kwa kujitambua huku kwa wananchi na serikali yao kuelekea kwenye utaifa ndiko kunakofanya taifa kuwa kitu kamili.

Ni kwa kujitambua huku mahusiano yao kati ya raia na serikali yao, ndipo taifa hufanya kazi kama kitu kimoja. Bila raia kujitambua wenyewe kwa wenyewe kama raia wa taifa moja na bila kujitambua wanaunganishwa na taifa moja na serikali moja iliyoundwa kuwatumikia hili taifa halitofanya kazi.

Ni muhimu sasa wananchi na serikali kuacha ubinafsi na kuangaliana kama watu wamoja kama raia wa taifa moja ambao mwisho wao ni mmoja na malengo yao ni mamoja ya kufanya jamii zetu ziwe bora.

Ni lazima tuwe tumeunganishwa na kitu kimoja kama taifa na hicho ni lazima iwe kujenga jamii bora kwetu na watoto wetu na kujilinda dhidi ya uharibifu wowote. Ni lazima tujenge raia wanaowajibika kwa jamii yao na kwa taifa. Kuna matumaini ya kujenga taifa bora na imara ikiwa tutajipanga.

Kwa busara inayoongozwa na uzalendo ni lazima tutafika sehemu fulani. Ikiwa dhamira zetu zitakuwa kutumikia jamii na sio ubinafsi. Ikiwa mawazo yetu yote tutayaelekeza kwenye kujenga taifa hili tutafanikiwa. Uraia ni jambo bora, ni ile hisia ya umoja ni hisia mimi ni wa jamii fulani. Ni lazima tujenge hisia hii ya utanzania. Lazima ijengwe nyumbani, shuleni na mtaani.

Tutakapo uona bendera yetu ikipepea ni lazima tujivune. Tusimame wima na kusema mimi ni mtanzania, nina matumaini na nchi yangu.

Nina imani tutafika mbali ikiwa tutakuwa wamoja na wenye dhamira moja na ikiwa ni wakweli wa nafsi. Kutoka mavumbini tunauwezo wa kulijenga taifa hili zaidi ya unavyofikiri. Inapokuwepo roho hii ya uzalendo hakuna kinachoshindikana pale raia wanapolipenda taifa lao hakuna kitakacho wazuia kuleta mabadiliko, kizazi hadi kizazi ni lazima tule kiapo, Kiapo cha juhudi zizisizofifia za kulinyanyua taifa hili, tutalinyanyua taifa hili kama tutafanya kazi pamoja.

Mkubwa kwa mdogo, wanawake kwa wanaume, wote tumeunganishwa na taifa moja na ni lazima mwisho wetu uwe mmoja kama taifa. Ni wakati umefika sasa kwa taifa letu kubadilika. Na kufuata dira iliyo sahihi. Huu ni wito wa utaifa, huu ni wito wa uzalendo. Huu ni wito wa kulisongesha taifa mbele. Hakuna msitu, hakuna mto, hakuna mlima utakaotuzuia kama tutakuwa wamoja na wenye dhamira moja na kama kila mmoja atakuwa tayari kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote.

Huu ni wito wa uzalendo maana halisi ya kuliweka taifa pamoja tayari kwa mapambano. Hii ni vita hatuwezi kuichukulia kwa akili ya kivivu wakati kila siku watu wetu wanaangamia sababu ya ujinga, wakati kila siku wetu wanakufa sababu ya maradhi, na wakati kila siku watu wetu wananyong'onyea sababu ya umaskini.

Kwa maskini ni lazima tuwaambie wanyanyuke wasisubiri, na kwa serikali ni lazima watengeneze mazingira ya kila raia kuendelea. Ni lazima kwa kila maskini awe na matumaini ya kwamba wakati utafika kwa kila raia wa nchi hii kuweka kifua mbele, wakati taifa litakapopata ukombozi dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini.

Wakati huu utakapofika wakati taifa hili litakapo kuwa moja, siku moja tutakusanyika litakapokuwa kubwa kuliko unavyofikiri, na kusema kwa uwezo wa Mungu tumeweza. Tutakumbuka jasho tulilotoa kulijenga na kujivunia na kila kiongozi atalijenga taifa hili kwa nguvu ile ile na roho ile ile.

Taifa kubwa linakuja na lazima lije. Kama tutasema haliwezi kufanyika basi halitoweza, na kama tutasema tutaweza ni lazima tutaweza, Ni jinsi tunavyofikiri tu na juhudi na jitihada zetu. Ili kile kinachoonekana

kama ndoto kiwe kitu kamili, lakini hili haliwezi kufanyika pasipo jitihada za pamoja.

Ni juhudi hii itakayo lifanya taifa hili kupata mwelekeo wake na kuendelea. Kama tutaelekeza fikra zetu katika masuala muhimu na kama tutafanya jitihada naona uwezekano huu. Ni fikra zetu zitakazo jenga taifa hili lakini pia ni juhudi zetu zitakazo jenga taifa hili. Ikiwa juhudi na fikra zitaunganishwa nina uhakika taifa hili litanyanyuka. Ni lazima na ni muhimu kujenga mwelekeo wa pamoja kama taifa, kwasababu bila umoja huu hatutafanikiwa.

Historia inaonyesha mataifa makubwa yaliyoendelea yalianza kwa kujenga misingi ya kimaadili na kinidhamu kwa watu wake, misingi ambayo iliwaunganisha na kuwafanya kuwa kitu kimoja na dira moja, na kuanguka kwa kubomoa misingi hiyo kwa kuwa wabinafsi kwa kila mtu kuangalia njia yake kwasababu hiyo umoja ule ulitoweka na malengo yao yalisambaratika.

Watu ni lazima wawe wamoja ili waendelee. Taifa pasipokuwa na malengo ya pamoja haliwezi kukua. Ni kweli bila mashaka ufalme **uliogawanyika wenyewe kwa wenye hauwezi kusimama.**

MWISHO